ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.

14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae

30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
33.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni

53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Tano – Tarehe 22 Januari, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha hati mezani Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Utangazaji Zanzibar, Kazi, Majukumu na Utawala wake pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Salim Abdalla Hamad (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Utangazaji Zanzibar, Kazi, Majukumu na Utawala wake pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 43

Kuboreshwa kwa Huduma za Zimamoto

Mhe. Ussi Jecha Simai – Aliuliza:-

Katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 hadi 2015, imeahidi kuimarisha na kuboresha huduma za Zimamoto na Uokozi kwa kuongeza na kuanzisha huduma hizo katika Wilaya zote.

- Je, Mhe. Waziri utekelezaji huo wa Ilani ya CCM umefikia wapi.

- Ni vituo vingapi vimeanzishwa na kupatiwa huduma za zimamoto na uokozi tangu kuanza kutumika Ilani hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 43 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, katika ilani ya uchaguzi ya chama tawala (Chama cha CCM) ya mwaka 2010 hadi 2015 ni kweli kwamba imeahidi kuimarisha na kuboresha huduma za Zimamoto na Uokozi kwa kuongeza na kuanzisha huduma hizo katika wilaya zote Unguja na Pemba.

- Utekelezaji wa Ilani hiyo ya mwaka 2010 – 2015 umefikia katika hatua za kuridhisha ambapo vituo kadhaa vipya vya huduma za zimamoto katika ngazi za Wilaya vimeanza kujengwa na kupatiwa magari pamoja na vifaa vyengine ambapo jumla ya magari saba (7) ya kuzimia moto na magari mawili (2) ya kubebea wagonjwa yamenunuliwa.

- Jumla ya vituo vitatu (3) vimeanzishwa na kupatiwa huduma za Zimamoto na Uokozi. Vituo hivyo ni Mwanakwerekwe Wilaya ya Magharibi Unguja, eneo la Bandarini Unguja na eneo la Bandarini Mkoani Pemba. Kituo cha Bandari ya Mkoani kwa sasa pia kitakuwa kikitoa huduma za Zimamoto na Uokozi katika Wilaya ya Mkoani na majirani zake. Aidha, hatua za ujenzi wa kituo cha Marumbi Wilaya ya Kati zimeanza. Kadhalilka, taratibu zinaendelea za kupatikana eneo katika Wilaya ya Wete pamoja na Wilaya nyengine ambazo huduma hizo bado hazijafika.

Nam. 47

Ukosefu wa Huduma za Benki Mkoa wa Kusini Unguja

Mhe. Mussa Ali Hassan – Aliuliza:-

Kwa vile Benki ni huduma muhimu kwa jamii hasa vijijini na ili kupunguza msongamano wa watu kwenda masafa makubwa kufuata huduma hii ya Benki. Na kwa kuwa Wilaya yetu ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja hatuna huduma hiyo muhimu ya Benki.

Je, ni lini tutapatiwa huduma hiyo muhimu ya Benki.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 47 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kuwa huduma zinazotolewa na Benki ni huduma muhimu kwa jamii, pia nataka nikubaliane naye kuwa Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini, Unguja hawana Benki, hivyo wananchi wa Wilaya hiyo kukosa huduma za kibenki ambazo ni muhimu kwa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi pamoja na wananchi kwa ujumla, kuwa kuanzisha tawi la Benki katika eneo lolote lile lazima kwanza ifanywe tathmini ili kubaini kuwa huduma za kibenki zinahitajika katika eneo hilo na kuwepo kwake hakutaleta hasara kwa benki. Aidha, matokeo ya tathmini hiyo, lazima yawasilishwe Benki Kuu ya Tanzania (*BoT*) kwa ushauri na mazingatio, baada ya hapo ndio kituo hufunguliwa kwa kuzingatia matokeo ya tathmini hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa umefika wakati kuangalia kwa kina mahitaji ya huduma za benki katika maeneo mbali mbali ya Zanzíbar ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Kati. Hata hivyo, kwa upande wa Wilaya ya Kati, kwa kuanzia tumeiomba Benki ya Watu wa Zanzíbar (PBZ) kuweka mashine ya ATM katika maeneo ya Chuo Kikuu cha Taifa Tunguu. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi mitatu (3) ijayo na baada ya hapo itafanyika tathmini ili kuweza kufahamu eneo la kuweka kituo cha Benki katika Wilaya ya Kati kwa lengo la kuwapatia huduma za Benki ambazo ni muhimu kwa jamii. Mhe. Mwenyekiti, kwasasa namuomba Mhe. Mwakilishi avute subira.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nimefurahia sana jibu lake lakini nataka kujua kwa ATM peke yake haitoshi. Je, suala la benki yenyewe litaanza lini.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nimesema katika kipindi cha miezi mitatu tutaweka ATM ili kupunguza makali ya kutokuwa na benki katika eneo lile. Lakini baada ya hapo tutachukua muda wa kuanza kufanya tathmini ya kubaini eneo gani tuweke benki na baada ya tathmini hiyo ndio itayotuonesha kwamba benki inahitajika katika Wilaya ya Kati, sina mashaka kuwa benki inahitajika lakini itatusaidia kutuonesha katika eneo gani tuiweke benki hiyo, kwa sababu wilaya ya Kati ni kubwa. Kwa hivyo, namuomba tena Mheshimiwa avute subirá na hili tulisimamie mimi na yeyé kwa pamoja.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri katika swali lake mama alisema mpaka iwepo tathmini, sasa nataka nimuulize hii tathmini ni ya watu au ni kigezo. Na ikiwa ni watu ni kiasi gani cha watu kiwepo ili iweze kuwekwa hiyo benki.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, taratibu za kibenki kwasasa hazihitaji kufanya tathmini ya watu kwa sababu sensa imeshakamilika. Lakini kinachofanyika ni mzunguko wa pesa na biashara katika eneo lile ili kuweza kujua kwamba hawa watu mzunguko wao wa pesa ni mkubwa na badala ya kusafirisha pesa zao kutoka katika eneo lao kufuata benki hivyo pale zinahitajika benki na biashara za pale. Kwa hivyo, hiyo ndio tathmini ya kiuchumi kiujumla itakayofanywa katika eneo lile ili kuweza kubaini kwamba benki ni kweli inahitajika. Kwa sababu biashara ya benki ni biashara ya kuweka na kukopa pesa.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hakuna uwezekano wa kufungua matawi kila eneo kwa nini PBZ hawaanzishi *system* ya *internet bank* au benki kupitia simu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe sijamsikia vizuri kidogo arudie.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, nimeuliza kwa kuwa hakuna uwezekano wa kufungua matawi kila eneo katika Zanzibar, kwa nini PBZ hawaanzishi *system* ya *internet bank* au benki kupitia simu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza katika bajeti niliyoisoma mwezi wa sita lengo la benki yetu ni kuifanya iwe ya kimataifa. Wazo la Mhe. Mwakilishi túnalo na tunalifanyia kazi na ndio benki itakapokuwa benki bora kuendana na hali halisi ya kileo. Mimi namuomba na yeyé avute subirá kidogo tumo katika kulishughulikia suala hili.

Nam. 101

Kupanda kwa Gharama za Vifaa vya Ujenzi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Bei ya vifaa vya ujenzi hapa nchini imepanda sana kiasi cha kuwafanya wananchi wengi kushindwa kuvinunua na hivyo kuendelea kubaki kwenye makaazi duni. Hali hii inakwenda kinyume na malengo ya Mapinduzi ya mwaka 1964 ya kuwapatia wananchi makaazi bora.

- Je, serikali ina mpango gani wa kuondoa VAT kwenye vifaa hivyo ili bei iweze kupungua kwa wananchi wamudu kununua vifaa hivyo.

- Je, inakuaje vifaa vinavyotengenezwa hapa nchini kwa kutumia mali ghafi ya hapa nchini kama saruji, chokaa, vyuma bado ni ghali kuliko vile vinavyoagizwa kutoka nje.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 101 lenye sehemu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

- Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kodi ya VAT pamoja na kodi nyengine ndizo zinazotumika kwa kugharamia shughuli mbali mbali za serikali. Kwa maana hiyo, serikali haina mpango wa kuiondoa kodi hiyo kwa sasa. Mpango wa serikali ni kuimarisha hali za wananchi kwa kuwaongezea mishahara kila hali inaporuhusu, kuhakikisha kuwa wanapata elimu ili kuweza kujiajiri kwa ufanisi zaidi pamoja na kuhakikisha wanapata fursa za mikopo nafuu kwa lengo la kumudu maisha yao. Vile vile kuwapatia huduma mbali mbali za kijamii karibu na maeneo yao kwa lengo la kuwapunguzia gharama za usafiri.

- Mhe. Mwenyekiti, zipo sababu nyingi zinazopelekea baadhi ya vifaa vinavyotengenezwa nchini kuwa na bei kubwa kuliko vile vinavyotengenezwa nje ya nchi. Baadhi ya sababu hizo ni kama zifuatavyo:-

    - Matumizi ya teknología duni

    - Matumizi ya nguvu kazi ya binaadamu ambayo huchukua muda mkubwa kutengeneza bidhaa kidogo.

- Kupanda kwa gharama ya umeme na mafuta.
- Uchache wa mali ghafi huchangia kuongeza gharama za usafirishaji.
- Uzalishaji usiozingatia matokeo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri será ya chama na serikali ni kuwapatia wananchi makazi yaliyo bora.

- Je, serikali inasaidia vipi na inakusudia vipi mfumko wa bei za vifaa vya ujenzi.

- Pamoja na serikali kupandisha mishahara kwa watumishi wake bado kiwango cha shilingi laki moja hamsini kidogo sana Mhe. Waziri. Je, wananchi atawasaidia vipi ili wakae katika makazi bora.

- Serikali hii isingekuwepo bila ya kuwepo wananchi na wananchi wana haki hii katika serikali hii, leo serikali inawalazimisha wananchi kujenga nyumba zao kwa kutomea wakati kutomea ni ghali zaidi kuliko kutumia tofali. Je, unatoa kauli gani kuhusu suala hilo wakati wengine wanaruhusiwa kujenga kwa matofali huoni ni ubaguzi huo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza juzi tulizungumza kwa kina katika Baraza la Biashara mpango wa serikali wa kuanzisha umeme wake jambo ambalo litasaidia sana ingawa si kwa kiwango kikubwa kupunguza gharama za umeme. Hii itasaidia bidhaa zinazotengenezwa ndani angalau kuwa na bei nafuu, vile vile itasaidia kupunguza mfumko wa bei.

Lakini vile vile Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika sasa hivi yuko katika hatua za kutoa mikopo kwa vikundi mbali mbali vya ushirika ili kuwawezesha wananchi waweze kuzalisha na kufaidika na nguvu zao na kuweza kupata kipato kitakachoweza kuwasaidia katika mambo mbali mbali. Hii itasaidia vile vile kupunguza ukali wa bei za bidhaa zilizomo ndani ya maeneo.
Kwa upande wangu pia nasema tu kwamba, wananchi wa Zanzibar wajitume zaidi ili kuweza kupata tija zaidi na kuweza kumudu vifaa ambavyo vinaagizwa kutoka nje na vile vinavyotengenezwa kutoka ndani ambavyo ni vya ujenzi.

Pili, Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba mshahara kima cha chini cha shilingi laki moja na hamsini ni kidogo. Mimi kama ni waziri mwenye dhamana ya fedha napenda kuahidi wananchi wetu kila hali itakaporuhusu serikali itaongeza mishahara. Tunafanya hivyo makusudi kwa sababu tunawajua wananchi wetu ndio wajenga nchi yetu, kila hali itakaporuhusu tutaongeza mishahara, ninachoomba ni kushirikiana tu na wananchi wetu ili tuweze kujenga nchi yetu kwa pamoja.

La tatu Mhe. Mwenyekiti, nitamuomba sana Mhe. Mwakilishi será za ujenzi unatumia bidhaa gani, unatumia rasilimali gani ili uweze kujenga haziko chini ya ofisi yangu. Nitamuomba swali lake alipeleke kwa wizara ambayo wanasimamia será hiyo ili waweze kumsaidia. Ingawa serikali tunafanya kazi kwa pamoja, lakini ni dhahiri na nijibu mbele ya Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti, kwamba waziri mwenye dhamana ataweza kulijibu kwa ufanisi zaidi swali lake la bidhaa gani za kujengea na gani zisiruhusiwe kuliko hata mimi ambaye kazi yangu kubwa ni kutafuta pesa tu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana aliyotoa Mhe. Waziri naomba kuuliza kwamba, makazi ni jambo muhimu sana kwa maendeleo ya jamii na taifa lolote. Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Marehemu, Mzee Abeid Amani Karume waliwapatia wananchi wake sio kuwawezesha, waliwapatia wananchi wake makaazi ya Michenzani pamoja na zile nyumba zilizoko vijijini tena kwa masharti nafuu sana na dhamira hii ilikuwa endelevu. Je, kuendelea kuwapandishia kodi wananchi wetu kama ilivyoulizwa katika swali la msingi za vifaa vya ujenzi wananchi wetu si kukwamisha dhamira nzuri ya marehemu Mzee Abeid Amani Karume na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, dhamira nzuri ya marehemu Mzee wetu Abeid Amani Karume iko palepale na itaendelea kudumishwa na Serikali ya Mapinduzi inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, wala hatutabadilisha dhamira hiyo na kuendelea kutoza kodi haina maana kudumaza dhamira hiyo. Kodi lazima serikali itoze ili kuweza kuwapatia huduma muhimu wananchi wetu, bila ya kodi hakutapatikana huduma za maji, afya wala elimu. Katika maeneo yote hayo kwa kiwango kikubwa serikali ndio inayohudumia. Kwa hivyo, kodi itaendelea kutozwa na dhamira nzuri ya kuwapatia makaazi wananchi wetu bado itaendelea kuwepo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu a na b.

- Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi la Mhe. Jaku Hashim alionesha kwamba mbinu kubwa serikali wanayoitumia ni kupandisha mishahara kwa wafanyakazi wa serikali. Lakini anasahau kwamba waajiriwa wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni karibu 0.003 ya Wazanzibari wote. Je, hawa Wazanzibari ambao si waajiriwa wanafidiwa wapi kupata gharama za ujenzi ili kutoa haki ya makaazi kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na kwa mujibu wa matangazo ya Umoja wa Mataifa.

- Tumewahi kuambiwa kwamba wamejitokeza wawekezaji mbali mbali hapa Zanzibar ili kujenga kiwanda cha saruji, lakini serikali haijaamua kuwapa kibali. Je, ni kwa nini wanawazuia wazalendo kuweka viwanda vya saruji na badala yake wakawaruhusu wafanyabiashara kwenda kuchukua saruji nje ya nchi huku si kuwaonea Wazanzibari kupata fursa ya ajira na kuweza kumudu makaazi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: (a) Mhe. Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi nimetoa mifano mitatu, nimetoa kupandisha mishahara, kuimarisha elimu ili waweze kujiajiri na vile vile mikopo nafuu. Kama Mzanzibari hajaguswa na

mishahara ataguswa na kupandisha elimu pamoja na elimu ya ujasiriamali au ataguswa na mikopo nafuu. Kwa hivyo, nimehakikisha kwamba Wazanzibari wote katika eneo hili limewagusa sio wale ambao wanaopata mishahara tu.

- Nikweli wamejitokeza baadhi ya wawekezaji kutaka kuwekeza kiwanda cha saruji hapa Zanzibar. Serikali suala hilo túnalo, serikali suala hilo tumelijadili kwa kina, tunaangalia kama kisiwa na jinsi malighafi anavyoitoa tutafaidika vipi na tutaathirika vipi kimazingira. Nadhani serikali itakapokamilisha tu tutaweza kumuarifu mwekezaji kama suala la kuweka kiwanda cha saruji Zanzibar ni *feasible* au sio *feasible***.** Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi kama una mawazo ya ziada basi naomba unisaidie na mimi wakati tunaendelea kulijadili suala hili.

Hivi sasa tumelipeleka kwenye kamati ili itusaidie kuangalia jiolojia ya Zanzibar kwa sababu hawa wanataka kuchimba jasi, kuangalia hali yetu ya mazingira na mengineyo, kuangalia mfumo wetu wa maji ambao tunautumia wa ardhini, yote hayo tumewapa wataalamu wayaangalie na baadae kuweza kuishauri serikali.

Nam. 19

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Kikosi cha KMKM

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mwaka 2010/2011 imeeleza kuwa kuna wastaafu katika Kikosi cha KMKM wanaendelea kulipwa mishahara na kusababisha hasara ya 18 Milioni kila mwezi.

- Je, serikali imechukua hatua gani kwa watu waliohusika na kitendo hicho.

- Kwa kuwa Watumishi wote wa Serikali wamo katika kumbukumbu za utumishi inakuwaje mishahara ya wastaafu iendelee kutoka na kulipwa wahusika wakati tayari wamemaliza utumishi wao Serikalini.

- Serikali ina mpango gani wa kuhakiki Askari wa Vikosi wanaoendelea na utumishi pamoja na wastaafu ili kupata ukweli juu ya matumizi ya mishahara na pencheni inayolipwa kila mwezi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijajibu swali naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana baadhi ya wastaafu wa KMKM ambao nawaona pale juu kwa kuja kututembelea katika Baraza letu tukufu wakiwemo Makamanda ambao waliwahi kukiongoza kikosi hiki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 19 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa suala hili lilikuwa ni miongoni mwa hoja halali za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Taasisi husika, ambayo inahitaji kupatiwa maelezo, na kwa kuwa hadi sasa hatuna taarifa ya jinsi hoja hiyo ilivyojibiwa. Nadhani Mjumbe atakubaliana na mimi kwamba, hivi sasa ni mapema kutoa maelezo ya hatua ambazo serikali imezichukua kwa wahusika. Taratibu zinatutaka tutoe nafasi kwa taasisi husika kutoa maelezo ya kujibu hoja hiyo kabla ya kuchukua hatua. Aidha, Kamati ya PAC ina wajibu wa kufuatilia hatua zilizochukuliwa na taasisi husika juu ya hoja zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, na kutoa ripoti ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anafanyakazi zake kwa mujibu wa Sheria. Kwa vyovyote vile, hoja anazozitoa hazina budi kupatiwa maelezo ya kina. Tunataraji taasisi husika itatekeleza wajibu wake na kujibu hoja hizo ipasavyo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, si jambo la kawaida na hairuhusiwi Kisheria kwa mishahara ya wastaafu kuendelea kutoka na kulipwa wahusika wakati tayari wamemaliza utumishi wao serikalini, hasa kwa kuwa watumishi wote serikalini wanatakiwa wawemo katika kumbukumbu za utumishi.

(c) Mhe. Mwenyekiti, Kazi ya Uhakiki wa Watumishi wa Umma ni miongoni mwa majukumu ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Kamisheni ya Utumishi wa Umma yaliyowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya mwaka 2011. Utekelezaji wa jukumu hili unafanyika kila inapojitokeza haja ya kufanya hivyo na kutegemea uwezo wa serikali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri yaliyokidhi swali la msingi, kwa kuwa ripoti nyingi za ubadhirifu zimekuwa hazifanyiwi kazi ikiwemo wahusika kufikishwa katika vyombo vya sheria, kuna sababu gani za Mkaguzi au Mdhibiti Mkuu wa Serikali kuendelea kuwepo na kufanya kazi yake.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo.

Kuwepo kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni matakwa ya Katiba na Sheria za nchi hii ya Zanzibar. Na si kweli kabisa kwamba ripoti nyingi au hoja nyingi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali huwa hazifanyiwi kazi. Ni ushahidi kwamba kila mwaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anapoleta ripoti zake huwa zinakuwa *table* hapa Baraza la Wawakilishi.

Maana ya kuwa *table* hapa Baraza la Wawakilishi, maana yake Kamati ya PAC kama nilivyoeleza kwenye jibu langu mama kwamba inatakiwa yenyewe sasa ifuatilie hoja zile. Hilo ni moja.

Lakini la pili kila taasisi iliyohusika na hoja ambazo zimeulizwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, inachotakiwa yenyewe kwanza waangalie ile hoja iliyotoka, kama kweli walihusika basi wajikosoe kwanza.

La pili wawachukulie hatua za kinidhamu wale ambao wamehusika na kadhia ile.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza swali Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa mbali ya kikosi cha KMKM kama lilivyo kwenye swali la msingi lakini vile vile kuna maelekezo kuwa kikosi cha Mafunzo nacho kina tatizo kama hili la kuwa watu wengi wanaolipwa mishahara na ambao hawapo kazini, kuna wale wengine waliofukuzwa na wengine walijiachisha kazi wenyewe.

Bahati mbaya kwamba hili halimo kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, sasa inaonekana kwamba tuna tatizo kubwa la matatizo haya katika vikosi vyetu.

Sasa kama hivyo ndivyo wizara yako ina mkakati gani wa kufanya tathmini halisi ya wafanyakazi katika vikosi vyetu hivi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kwanza wizara yangu kama nilivyoeleza inao wajibu huo wa kufanya uhakiki wa watumishi na mishahara ya watumishi kisheria. Kwa hivyo kwa kuwa amenipa taarifa hiyo basi wizara yangu itachukua hatua ya kwenda kufanya uhakika huo katika kikosi ambacho amekitaja.

Hata hivyo, wizara yangu ilishafanya uhakiki na ndio maana ikagundua hoja ambayo imeelezwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kufika hapa katika Baraza lako hili tukufu kwa mintarafu ya kupanga mipango yetu ya taifa letu.

Nitamuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Jee, Mhe. Waziri anajua kwamba vikosi vyetu hivi katika mtiririko wa kupokea mishahara mtu hajui kima gani anachokatwa na kima gani anachobakia nacho, anatilishwa saini tu. Kama anajua wizara yake kwa sababu ni wizara ambayo ya utawala bora na inashughulikia watumishi wa serikali hii, jee atafanya nini ili kuhakikisha kama ni kweli ili kuboresha namna ya kupokea mishahara kwa vikosi vyetu hivi. Hilo la kwanza.

Swali la pili, jee, atakubaliana na mimi kwamba kuna haja hivi sasa ya kuangalia vikosi vyetu vyote ambavyo utekelezaji na wengine wanajitahidi katika utekelezaji mheshimiwa kuangalia ni maslahi ya namna gani na mshahara mtu anayepata kiasi ili kumtia moyo yule mfanyakazi ambaye anayewajibika kwa vikosi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa yako nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo.

Kwanza natambua kwamba suala la watumishi kutokujua kima halisi cha mshahara lilikuwepo huko nyuma kabla ya Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora haijafanyakazi zake kwa mujibu wa sheria iliopo.

Lakini baada ya wizara hii kuwepo wafanyakazi wote wa vikosi vya SMZ wanajua ni kiasi gani kima chao cha mshahara wanacholipwa na kiasi gani katika mshahara wao wanachokatwa kwa mujibu wa taratibu ambazo wameekeana wao wenyewe.

Swali la pili ni vipi serikali itachukua hatua ya kuwapa motisha ya wafanyakazi wa vikosi vyetu. Nataka nimfahamishe Mhe. Mwakilishi pamoja na Baraza lako Tukufu kwamba hata tulipofanya marekebisho ya mishahara kwa watumishi wa umma wote, wafanyakazi wa Idara Maalum walipewa kima cha chini cha mshahara tofauti na wafanyakazi wa taasisi nyengine za kiraia.

Hii ni kuonesha kwamba serikali imeona uzito na uwezo wa askari wetu ili kuwapa motisha zaidi waweze kuwa na moyo wa kufanya kazi zao kwa ujasiri na kwa uzalendo zaidi.

Nam. 52

Upatikanaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu

Mhe. Mohammed Haji Khalid – Aliuliza

Mhe. Mwenyekiti, naomba nifanye marekebisho madogo na baadae ndio swali langu lilijibiwe.

Naomba kuondoa swali nambari (c) hivyo naomba nijibiwe swali langu nambari (a) na (b)

Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wanafunzi wanaoomba mikopo kwenye Bodi ya Mikopo ya Zanzibar na ile ya Tanzania, kuwa baadhi ya waombaji wamepata mikopo hiyo kutoka Bodi zote mbili.

- Jee, kuna ukweli wowote ule kwenye malalamiko hayo
- Kama ni kweli ni waombaji wangapi wa Zanzibar wamepata bahati hiyo
- Jee, hakuna mwombaji hata mmoja amepata mikopo kutoka kwa Bodi zote mbili.

Mhe. Mwenyekiti: Utajibu swali nambari (a) na (b), swali nambari (c) mwenyewe ameliondoa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 52 vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa baadhi ya wanafunzi hutuma maombi yao ya mikopo katika Bodi zote mbili; Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bodi ya Mikopo ya Zanzibar. Kufanya hivyo ni haki yao kwani vyombo vyote vina wajibu wa kuwahudumia hasa kwa vile wanafunzi hawana uhakika wa kujua atapata wapi mkopo kutokana na chombo gani.

Hata hivyo, sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar hairuhusu kumkopesha mwanafunzi ambaye tayari ana mkopo mwengine wa ufadhili wa masomo yake. Hivyo wanafunzi wanaochaguliwa kupata mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Jamhuri ya Muungano anapoteza sifa ya kupatiwa na Bodi ya Mikopo ya Zanzibar.

Baadhi ya wanafunzi wanaopata mikopo wa Bodi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wao wenyewe huandika barua na kufuta maombi yao ya mikopo kwa SMZ. Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa wapo waombaji mikopo walioomba mikopo katika Bodi za Mikopo zote mbili. Kwa mwaka 2012/13 Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar ilibaini wanafunzi 236 wapya waliopendekeza kupata mikopo kutoka Bodi zote mbili.

Hivyo Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Zanzibar iliwafuatia mikopo wanafunzi wote hao na nafasi zao zikajazwa na wanafunzi wengine ambao hawakupata mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Zanzibar.

Kuwaruhusu wanafunzi kuchukua mikopo kutoka kwenye bodi zote mbili athari zake ni kuwapa mzigo mkubwa wa kulipa madeni wakati mmoja, pia wanafunzi hao kuzuia nafasi kwa wanafunzi wengine ambao wamekosa mkopo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa pamoja na majibu mazuri Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali moja dogo tu la nyongeza.

Lakini kabla ya hapo naomba niziipongeze serikali zetu hii ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kuweza kuwa na hii bodi ya mikopo na kuwasaidia Watanzania wote katika kupata taaluma.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wanafunzi kwenye vyuo vyetu vikuu wanastahiki kunufaika na jasho lao, yaani fedha hizo za mikopo wanastahiki kunufaika nazo bila ya kujali chuo gani anasoma au wapi anatoka.

Baada ya maelezo hayo naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali lifuatalo ni kwa sababu gani wanafunzi wa Chuo Kikuu Huria hususan waliopo hapa Zanzibar inakuwa shida na hamuwapatii, yaani hizi Bodi haziwapatii mikopo ni kwa sababu gani ya msingi

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ya Zanzibar ina mipango yake na utaratibu wake hasa kutokana na hali halisi ya fedha kidogo ambazo tunazopata na maombi ya wanafunzi wetu inakuwa ni mengi.

Mara nyingi hatutizami ni chuo gani hususan vyuo vyote vya ndani ya Zanzibar au Tanzania Bara tunawapa mikopo, lakini inategemea ni fani gani ambayo anachukua muombaji. Kwa hivyo fani ambayo anayochukua muombaji ikiwa ni katika Chuo Kikuu Huria au vyuo vyengine, ikiwa haipo katika fani ambazo zimepewa kipa umbele na serikali, hapo Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kutoa mkopo.

Nam. 53

Walimu Walioshiriki katika Usahihishaji wa Mitihani Zanzibar

Mhe. Mohammed Haji Khalid – Alijibu

Walimu pamoja na maafisa mbali mbali walioshiriki kwenye usahihishaji wa mitihani ya madarasa ya 7 (STD VII) na kumi (Form II) kwa mwaka 2011 walikuwa ni 845 kati ya hao 818 sawa na asilimia 96.80 walitoka Unguja na 27 sawa na asilimia 3.19 walitoka Pemba, hii inasemekana ni kutokana na ufinyu wa bajeti.

Jee, kwa mwaka huu wa 2012 Wizara yako imejiandaa vipi ili kupunguza tofauti hii kubwa mno ya walimu kwenye usahihishaji wa mitihani hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 53 kama hivi ifuatavyo.

Kabla ya kujibu naomba nitoe maelezo ya utangulizi

Kazi ya usimamiaji, utungaji na usahihishaji wa mitihani ni kazi zinazopaswa kuwasilishwa kwa makini na uadilifu mkubwa. Uteuzi wa walimu na wafanyakazi wengine kushiriki katika kazi ya usahihishaji ya mitihani kunategemea mambo mbali mbali yakiwemo uwezo wa kielimu, uzoefu, umakini wa walimu na utunzaji wa siri na pia kuzingatia gharama.

Katika utendaji wa kazi hizo, walimu wa sehemu mbali mbali ziliopo katika skuli zetu hupata fursa ya kushiriki katika kazi hizo. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika mwaka wa fedha 2011/12, walimu waliochaguliwa kushiriki katika kazi za usahihishaji wa mitihani ya darasa la saba, kumi, wengi wao walitoka katika skuli za Unguja na hasa katika Mkoa wa Mjini/Magharibi ambapo ndio wenye idadi kubwa ya walimu na wanafunzi wanaofanya mtihani.

Jumla ya walimu na wafanyakazi 765 walishiriki katika kazi hizo. Walimu na wafanyakazi 739 walitoka katika skuli za Unguja sawa na asilimia 96.6 ya wasahihishaji wote na walimu na wafanyakazi wengine 26 sawa na asilimia 3.4 walitoka katika skuli za Pemba.

Idadi ndogo ya walimu walioteuliwa kutoka skuli za Pemba inatokana na gharama kubwa ya shughuli ya mitihani ikilinganishwa na uwezo wa kifedha. Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, katika

mwaka 2011/12, Wizara ilitenga bajeti ya bilioni moja, milioni mia tatu na thamanini na mbili kwa ajili ya shughuli zote za mitihani darasa la saba, kidato cha pili na kidato cha nne.

Fedha zote hizi zilipatikana lakini kiwango hiki ni kidogo ukilinganisha na gharama halisi ya ufanyaji wa mitihani. Kwa mwaka 2011/12, wizara inadaiwa shilingi milioni mia nne na thalathini na nne, mia tisa na tisini na Baraza la Mitihani la Tanzania kwa malipo ya ada ya mitihani ya wanafunzi wa kidato cha nne.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Walimu na wafanyakazi walioteuliwa kushiriki katika kazi ya mitihani 803, kati yao walimu na wafanyakazi 714 walitoka katika skuli za Unguja sawa na asilimia 88.9 ya wasahihishaji wote.

Walimu na wafanyakazi 89 waliteuliwa kutoka skuli za Pemba ni sawa na asilimia 11.1.

Aidha bajeti ya shughuli za mitihani iliongezeka kutoka bilioni moja nukta tatu kwa mwaka wa fedha 2011/12 hadi kufikia bilioni moja nukta tano kwa mwaka wa fedha 2012/13.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize swali dogo sana Mhe. Naibu Waziri.

Walau tunapongeza kwa hatua hiyo ya kutoa walimu milango ishirini hadi kuingia milango ya thamanini ni kitu cha kupongeza.

Lakini inasemekana walimu hawa waliowekwa siku kumi hawakulipwa posho. Jee, Mhe. Naibu Waziri suala hili ni kweli na kama ni kweli wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba walimu hawa wanyonge wanalipwa posho zao kwa haraka.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli walimu hawa hawalipwi posho lakini walilipwa *sitting allowance* ile ya kazi yao za usahihishaji. Mhe. Mwenyekiti, unakumbuka kama kazi hii sasa tulipitisha sheria hapa za kuanzisha Baraza la Mitihani za Zanzibar na Baraza hilo la Mitihani la Zanzibar ndio ambao tumewapa kazi ya kuratibu na kufuatilia na kufanya shughuli zote za mitihani.

Kwa hivyo na wao sasa walifuata mfumo wa wenzetu ambavyo wanafanya Tanzania Bara wafanyakazi wao wanapofanyakazi hizi huwa hawalipwi posho kawaida, wanawalipa ile *sitting allowance* ya ile kazi ambayo wanayofanya.

Kwa hivyo ni kweli kama hatukuwalipa posho na hakuna mpango wa kutoa posho kwa sasa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kwa kuuuliza swali hili la nyongeza.

Naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja lenye vitoto viwili (a) na (b).

Mhe. Naibu Waziri kwa muda mrefu sasa au miaka mingi sana walimu ambao wanaochukuliwa kwa ajili ya usimamizi wa mitihani huchukua muda wa mwaka mmoja au mwaka ulioanza na kumalizia katika mwaka mwengine bado hawajapewa posho la usimamizi wa mitihani.

(a) Jee, wasimamizi waliosimamia mtihani wa mwaka 2012 wameshalipwa posho lao.

(b) Mhe. Naibu Waziri kitendo cha kuwachelewesha walimu wazalendo ambao wanasimamia mitihani ya taifa ya Zanzibar huoni ni kitendo cha kuwavunja moyo walimu hao na inawafanya baadhi ya walimu kutokuwa waaminifu kutokana na kucheleweshwa kwa posho hilo na kazi ngumu ambayo wanaifanya.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, aliposema kama tunachelewa kuwalipa walimu wetu posho, ijapokuwa tunajua kuwa kila mwaka mitihani inafanyika na posho inatakiwa, lakini pia na sisi inategemea ni namna gani ya zile fedha ambazo tunatiliwa na Wizara ya Fedha. Lakini huwa tunahakikisha kabla ya mitihani mwengine basi tunalipa posho hiyo.
Kama nilivyozungumza nilivyomjibu Mhe. Omar Ali Shehe kwa sasa ile posho tumeiondoa na walimu ambao watashiriki katika kazi hii watalipwa ile sitting allowance yao tu.

Nam 34

Matukio ya Udanganyifu katika Dini

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza

Katika miaka ya hivi karibuni matukio ya udanganyifu wa kidini na kuritadi yamekuwa yakijichomoza mara kwa mara hapa Zanzibar. Tukio la hivi karibuni ni tukio la kijana mmoja aliyeidanganya Mahakama ya Kadhi kwa kwenda na mwanamke kwa madai ya kusilimu ili wafunge ndoa. Baada ya hatua yao hiyo Mahkama iliamua kuwafungisha ndoa na hatimae ilibainika wazi kuwa wamedanganya na mwanamke kujitangazia kuwa sasa amebadilisha dini na kuwa Mkristo, pamoja na jitihada za familia ya mwanamme kuomba msaada wa serikali wa kumnusuru kijana huyo bado sheria haijachukua nafasi yake.

- Jee, baada ya kujulikana kuwa wamedanganya bado ndoa yao hiyo ipo.
- Katika Mahkama za Kidunia (secular) ni koa la jinai kuidanganya Mahkama ya Kadhi sio kosa na kama ni kosa nini adhabu yake
- Jee, serikali yetu imefanya utafiti na kugundua ni kwa nini wimbi la kuivamia Zanzibar kidini linaongezeka na kwa nini Mahkama zetu za Kadhi zinachezewa.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 34 kama ifuatavyo.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, naomba ieleweke kuwa katika sheria za Kiislamu ndoa ya Sunna yenye umuhimu mkubwa na ina utaratibu wake kisheria. Utaratibu huo unawapa uhuru mwanamme na mwanamke kuoana wanapohitaji kwa taratibu za kisheria na kuachana inapobidi kufanya hivyo.

Kuachana wenyewe iwe ni kwa wema na hisani. Ingawa kuachana ni jambo lisilopendeza mbele ya Mwenyezi Mungu na inabidi lifanyike ikiwa hapana budi. Vile vile ndoa ya Kiislamu hufungwa baina ya Waislamu mwanamke na mwanamme.
Inapotokea mmoja kati ya wahusika wa ndoa hiyo au wote wawili wameacha Uislamu basi ndoa hiyo haiwezi kuwa ni ndoa ya Kiislamu. Pia napenda ifahamike kuwa ndoa yoyote ni mkataba, unapodanganya katika kukatibiana kitu hivyo unapotambulikana kuwa umedanganya basi mkataba huwa hausimami na hauwezi kukubalika kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, ni vyema pia ikaeleweka kuwa kila mtu anastahiki kuwa na uhuru wa mawazo, imani na uchaguzi katika mambo ya dini pamoja na uhuru wa kubadilisha dini au imani yake anavyopenda.

Mhe. Mwenyekiti, uhuru huu umo katika kifungu cha 19 (1) cha Katiba ya Zanzibar lakini kifungu cha 19 (2) cha Katiba ya Zanzibar inasema wazi kwamba dini na imani ya mtu kuamini anachotaka ipo nje ya mamlaka ya nchi. Kwa hivyo serikali haiwezi kumuingilia mtu katika dini yake au katika kuchagua imani yake anayopenda.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo.

Baada ya wahusika kujulikana kuwa mmoja wao au wote si Waislamu hiyo ndio haiwezi kuwepo kwa misingi ya dini ya Kiislamu. Hata hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa vile hatuna taarifa ya kutokezea kwa suala hilo ningelimuomba Mhe. Mjumbe atuletee vielelezo madhubuti vya kadhia hii kwa ajili ya kutaka kuwanasihi vijana hao ili katika Uislamu kudanganya ni kosa, iwe mtu amedanganya Mahakama au taasisi nyengine.

Kwa upande wa taratibu za Kimahakama iwe ya Kadhi au nyengine yoyote huwa ni kosa la kijinai, (*contempt of court*) na adhabu hutolewa na Hakimu au Jaji anayesikiliza kesi hiyo kutokana na uzito wa kosa lenyewe na ushahidi wa kosa liliopo.

Kwa vile Mahakama za Kadhi hazina mamlaka kwa kesi za jinai, inawezekana watu hutumia udanganyifu kwamba inakuwa vigumu kujulikana ili kutimiza mahitaji yao. Lakini kudanganya kwake huko kwa kupata haja yake hususan ya ndoa basi inapojulikana huwa makubaliano hayo si sahihi na ndoa hiyo huvunjika.

Serikali haijafanya utafiti wa aina hiyo na kwa upande mwengine ili kuzipa ufanisi zaidi Mahakama za Kadhi, wizara yangu kwa hivi sasa imeshirikiana na Wizara ya Ustawi wa Jamii,

Maendeleo ya Wanawake na Watoto na tumo katika hatua nzuri na ya matayarisho ya mwisho ya kuibadilisha au kuirekebisha sheria mpya ya Mahakama ya Kadhi ambayo mara tu hatua zitakapokamilika italetwa Barazani kwa michango na kupitishwa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, kwanza nimpongeze kwa kuamua kwamba ikiwa taarifa kama hii tumpelekee ili apate kuisimamia ingawa mimi naamini Mahakama yake ya Kadhi inajua tokeo hili.

Hata hivyo, mimi nitafanya bidii tuwasiliane ili nimkumbushe kwamba Mahakama gani kesi hiyo ilisimamia na wakadanganya na wakaiachia.

Lakini swali langu Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba wimbi la udanganyifu Zanzibar linaendelea siku hadi siku. Hivi karibuni vyombo vya habari vimenukuu mwanamke mmoja aliyejiita yeye ni Mtume na Masahaba maeneo ya Darajabovu.

Jee, naomba kujua serikali imechukua hatua gani kwa mwanamke huyu aliyedanganya taifa kwa kujiita Mtume ili wananchi wajue hatua ambayo serikali imechukua.

Na kwa nini vitendo hivi vya udanganyifu wa kidini viongozeke hapa Zanzibar siku hadi siku, kuna tatizo gani naomba kujua.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Mjumbe maswali yake mawili ya nyongeza kama inavyofuata.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo hata hayo makaratasi akiniletea yanaonesha udanganyifu au yanaonesha kwamba huyo mtu ametoka katika Dini ya Kiislamu na kuingia dini nyengine, basi serikali haiwezi kumlazimisha mtu kurudi katika dini hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 19(1) kinasema kila mtu ana uhuru wa kuamini dini anayotaka na kuwa na imani ya dini anayotaka. Kwa hivyo, si jukumu la serikali, lakini jukumu leo sisi kama ni visiwa takriban watu wengi ni Waislamu tunalo jukumu kwa upande mwengine la kumshawishi au kuzungumza naye, ili aweze kurekebisha au kujirekebisha katika dini hiyo na kuingia katika dini yake ya zamani. Jambo hilo linafanywa na wanaofanya haya mara nyingi huwa ni Afisi ya Mufti, Afisi ya Kadhi Mkuu pamoja na masheikh wetu katika ngazi hizo.

Sasa utakapoleta hayo makaratasi tutayachukua kwa misingi hiyo, lakini si kwa misingi ya serikali kwamba lazima imlazimishe arudi katika dini aliyokuwa nayo zamani na hilo litakuwa ni kinyume na Katiba.

Pili ni kweli kwamba hivi karibuni kuna mwanamke mmoja bibi Amina nafikiri kama hivi alikuwa anajiita ni mtume na alipita katika baadhi ya maeneo. Lakini kama nilivyosema serikali kwa upande mmoja ina chombo chake cha Mufti na Kadhi Mkuu.

Baada ya kuyapata hayo walikutana Mufti pamoja na Baraza lake la Maulamaa wakalizungumza na kuwaita watu ambao walikuwa tayari wameshaingizwa katika hiyo dini ya mtume huyo Amina.

Kwa hivyo, baada ya kukaa nao baadhi yao wamekubali kurudi kwa kuwashawishi wamekubali kurudi na huyu aliyekuwa akijiita mtume hivi sasa hayupo tena ameshaondoka kwa sababu hizo za kuzungumza na kuwapa mawaidha ya kidini na mambo kama hayo.

Kwa maana hiyo, hivi sasa suala hilo naamini halipo tena na kama limejitokeza baadhi ya mwahala kitu ambacho sifikirii basi tupatieni taarifa, ili niweze kulipeleka kwa Mufti pamoja na Kadhi Mkuu waweze kukaa tena na kuzungumza nao.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa ya mwisho ambayo ninayo ni kwamba huyu mtu tayari ameshaondoka na wale ambao walikuwa wameshakuwa-*converted* katika dini ya huyu mtu na wao wengine wamesharudi katika dini yao. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Nam. 64

Ushajihishaji wa Wananchi katika Kilimo cha Umwagiliaji Maji

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa mabadiliko ya tabia nchi, imepelekea ukosefu mkubwa wa mvua, jambo ambalo limeteremsha kwa kiasi kikubwa kipato cha wananchi kupitia kilimo cha kutegemea mvua.

Je, ni kwa kiasi gani serikali imewezesha pamoja na kuwashajiisha wananchi katika Kilimo cha Umwagiliaji Maji (*Irrigation*).

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake kama ifuatavyo:-

Wizara ya Kilimo na Maliasili inazingatia kwa uzito mkubwa ukosefu wa mvua na mabadiliko ya tabia nchi, serikali kupitia wizara hii ina mpango wa kutengeneza maeneo yote, ambayo yanafaa kumwagiliwa Unguja na Pemba. Hekta 8521, ambapo hadi sasa hekta 750 zimejengwa miundombinu ya umwagiliaji kupitia ufadhili wa Korea *Exim Bank*, jumla ya hekta 2000 zinatengenezwa miundombinu ya umwagiliaji maji na hekta 1200 kupitia msaada wa Marekani.

Wizara ya Kilimo na Maliasili kupitia *program* zake mbali mbali mfano *ASDPL*, ASSP zinaendelea na juhudi ya kuwakomboa wakulima kwa kuwapatia mafunzo na kuwashajihisha wakulima katika maeneo kubadilisha kilimo kutoka cha kutegemea mvua na kuwa cha umwagiliaji maji.

Wizara hivi sasa inaandaa miradi na programu nyengine za kupata fedha za kujenga miundombinu ili kutekeleza Mpango mkuu wa umwagiliaji maji.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja dogo kama ifuatavyo. Kwa kuwa mpango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa Kupunguza Umasikini Mkuuza kuna klasta ya *Poverty Reduction and Income Generative.* Kwa kuwa wakulima wa Jimbo langu la Wawi wanategemea sana kilimo katika kujipatia kipato na kupunguza umasikini kupitia kilimo cha umwagiliaji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa *ZAWA* wanakuwa wakali sana tunapotumia maji yao ya bomba katika kumwagilia mambo ya kilimo. Je, serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima katika kuvuna maji ya mvua na kuweza kuyahifadhi kama wanavyofanya wenzetu pale Tanganyika, wanapoyavuna na kutumia kwa mifugo na kilimo.

Kwa hivyo, ni lini Serikali yetu ya Mapinduzi ya zanzibar itawasaidia wakulima wa Jimbo la Wawi kuwapatia utaalamu wa kuvuna haya maji ya mvua na kuyahifadhi na kuweza kuyatumia kwa kilimo cha umwagiliaji badala ya kuyaachia kwenda baharini ovyo. Hilo la kwanza.

Pili ni lini Serikali ya SMZ itawasaidia wakulima kuchimba visima, *pump* pamoja na vile *spring killer* za kumwagilia maji kwenye vipando vyao. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kuna mradi unaofadhiliwa na *Exim Bank* kutoka Korea, mradi huu utajenga miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua na mradi huu tayari umeshatiwa saini.

Vile vile utekelezaji wa mradi huu utaanza mwezi wa Julai mwaka 2013. Suala lililobakia kwenye mradi huu ni kuwafuata wakandarasi na kuanza utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili naomba urudie kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri, kuhusu kuchimba visima aliuliza Mhe. Mjumbe.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, suala la kuchimba visima ni pia katika kuwashajihisha wakulima kuna mradi wa kuchimba visima. Kwa kweli mradi huu utakuwa sio Wawi tu peke yake hata Wilaya ya Kaskazini ‘A’ na mradi huu pia unafadhiliwa na *Exim Bank* na mradi huu tayari imeanza kununua *pump* mpya na unashajihishwa na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, pamoja na kuwashajihisha wakulima katika kilimo hichi cha umwagiliaji maji.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Kwa kuwa uhai wa binadamu na mimea ni kilimo.

Je, atakubaliana na mimi Mhe. Waziri kwamba imefika wakati wizara yake kutathmini kwa mikoa yote mitano wapi na wapi, mabonde gani ambayo yanastahili kumwagiliwa maji kwa ajili ya kilimo cha mpunga, ili ajue tathmini halisi ambayo itamuwezesha yeye pamoja na wizara yake kuhakikisha kwamba hapa na hapa ndipo panapotaka kumwagiliwa maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, tathmini hiyo napenda kumueleza Mhe. Mwakilishi pamoja na Baraza lako tukufu kwa jumla kwamba tayari imeshafanywa katika maeneo mbali mbali ikiwemo Cheju pamoja na maeneo mengine.

TAARIFA

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, sijajibiwa vizuri na wala sijaridhika kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, umemuuliza Mhe. Naibu Waziri juu ya utaratibu gani utafanyika na Mhe. Naibu Waziri amekujibu kwamba tayari utafiti umeshafanywa na maeneo ambayo yamefanyika utafiti huo pia amekutajia. Sasa sijafahamu nini cha ziada.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, nimeuliza kwa mikoa yote si kwa Cheju wala wapi na wapi, yaani kwa mikoa yote sasa amejibu kijuujuu tu kwa Cheju na nini basi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, hii miradi iliyotajwa ya *Exim Bank*, Marekani na *SPDL* imefanya kazi ya kufanya utafiti wa maeneo yote kwa mikoa yote mitano, kwa sababu ya kuhakikisha kwamba kilimo cha umwagiliaji maji na wala sio mpunga tu hata mbogamboga na kuna baadhi ya maeneo yameshaanza kazi ya kulima mbogamboga kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji maji.

Kwa hivyo, kazi hii tayari imeshafanywa tusubiri hii miradi iive, ili tuweze kuona utekelezaji wake unavyoelekea. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, natumai umefarajika.

Nam. 45

Kuvunjwa kwa Shirika la Magari

Mhe. Salma Mussa Bilali (Kny: Mhe. Shadya Moh'd Suleiman) – Aliuliza:-

Hivi karibuni katika Kikao cha Bajeti Mhe. Waziri wa Biashara alitamka kulivunja Shirika la Magari wakati bado Shirika hilo linajiendesha.

(a) Hebu Mhe. Waziri atueleze ni sababu zipi za msingi zilizopelekea shirika hilo kuvunjwa wakati kuna mashirika mengi bado yanaendelea kuwepo na wala hayawezi kujiendesha kwa faida.

(b) Ni ipi hatima ya wafanyakazi wa shirika hilo, ambao bado hawajastaafishwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 45 lenye kifungu (a) na (b) linalohusiana na azma ya serikali ya kulifunga Shirika la Magari kama hivi ifuatavyo:-

- Mhe. Mwenyekiti ni kweli katika bajeti ya mwaka 2012/2013 ilitangaza azma ya kulifunga Shirika la Magari, sababu kubwa zilizopelekea kufungwa kwa shirika hilo ni kama ifuatavyo:-
    - Shirika la Magari limeonekana kutofanya biashara ya magari, ambalo ndilo suala la msingi kuanzishwa kwa shirika hilo.
    - Biashara ya Magari kwa sasa imehodhiwa na Sekta Binafsi na hivyo shirika hilo kutoonekana kwenda kiushindani kama inavyotakiwa.
    - Shirika limekosa mtaji wa kutosha wa kuweza kufanya biashara hiyo ya magari.

- Mhe. Mwenyekiti, kuhusu khatma ya wafanyakazi wa shirika, serikali imepanga kuwastaafisha kwa kuzingatia misingi ifuatayo:-
    - Kuzingatia matakwa ya Sheria ya Utumishi Namba 2 ya mwaka 2011,
    - Kuzingatia matakwa ya Sheria ya Kazi namba 1 ya mwaka 2005
    - Kufanya malipo ya mafao ya wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kiinua mgongo pamoja na stahiki nyengine.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Waziri endapo shirika hili likeshavunjwa, je litaacha mali na majengo yenye thamani ya kiasi gani kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko tumeshafanya tathmini ya mali ambayo itaachwa endapo azma ya serikali ya kulivunja Shirika hili la Magari itaanza kutekelezwa.

Tathmini hii imefanywa zaidi katika majengo ambayo ndio mali isiyohamishika ya thamani kubwa. Kwa upande wa Unguja Mhe. Mwenyekiti majengo hayo ya Shirika hili la Magari yameonekana kuwa na thamani ya fedha za kitanzania shilingi bilioni 5.9. Kwa upande wa Pemba majengo ambayo yataachwa na shirika hili yatakuwa na thamani ya shilingi bilioni 2.6.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri amekiri kuvunjwa kwa shirika hili.

- Je, wakati wa kuvunjwa ni wafanyakazi wangapi ambao watahusika na kustaafishwa.

- Ni kiasi gani cha fedha ambazo zitatumika kwa kuwalipa wastaafishwa hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Magari kwa hivi sasa lina wafanyakazi 33, miongoni mwao wanane wakiwa ni wanawake. Jumla ya fedha ambazo wizara imeshazifanyia kazi katika kulipa mafao ya wafanyakazi hao endapo watastaafishwa kutokana na kuvunjwa na Shirika hilo la Magari ni fedha za kitanzania shilingi bilioni 1.15.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo. Ni kweli kuwa Shirika la Biashara la Magari linajiendesha kwa faida na linalipa kodi serikalini ni tofauti sana na mashirika mengi ya umma tuliyonayo nchini. Vile vile ni kweli kuwa shirika linakabiliwa na ushindani kutokana na sekta binafsi kwenye sekta ya biashara.

Lakini kwa kuwa serikali ina mahitaji mengi ya manunuzi hasa vyombo vya moto na mambo mengine, ambapo tumeshuhudia serikali hufanya biashara na wafanyabiashara ambao hata wakati mwengine hawalipi kodi serikalini kitu ambacho ni hatari sana kwa uchumi wa nchi. *(Makofi).*

Sasa kwa kuwa shirika hili lipo na lina uzoefu mkubwa tena ni shirika la serikali. Kwa nini serikali haifikirii kuliongezea nguvu shirika hili na hasa kwa vile shirika hili lina mtaji kama alivyoeleza Mhe. Naibu Waziri wa kuliwezesha shirika hili kupata mikopo, ili serikali ikalitumia shirika hili katika kufanya biashara zake au kwa nini katika hivyo haifanyi kulibadili angalau kikawa ni chombo maalum cha manunuzi kama kilivyo Tanzania Bara chombo cha *PPRA.*

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimueleze Mhe. Mjumbe kwamba kabla ya mimi kuwa viongozi ndani ya serikali nilikuwa ni Mwakilishi ambaye wa *backbencher* na miongoni mwa kamati tulizozifanyia kazi ilikuwa ni Kamati ya Fedha na Uchumi. Katika kutekeleza majukumu ya kamati basi tulikuwa tunalitembelea sana Shirika hili la Magari.

Vile vile nataka nimkumbushe Mhe. Mjumbe, kwamba tayari tumeshatoa mawazo hayo ndani ya kamati kwa muda mrefu. Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nimhakikishie kwamba shirika hili limeachiwa kwa muda mrefu, ili liweze kuonekana kama linaweza kufanya kazi hiyo na limewezeshwa kwa kukabidhiwa baadhi ya kazi ambazo hazikuwa zake tangu awali ikiwemo kutoka vibali kwa magari yanayoingizwa nchini, kuwa wakala wa mashirika ya bima, kwa ajili ya kujiongezea mtaji na kuweza kufanya biashara zao.

Lakini jambo lililoonekana ni kwamba hawakuweza na zaidi baada ya kufanya biashara huria ya kuingiza magari ndani ya nchi. Kwa hivyo, shirika hili halikuweza kukidhi kwenye ushindani huo. Matokeo yake shirika hili likajikita zaidi kwenye biashara za vespa likatoka huko linaingia kwenye biashara za vyarahani na baskeli ambalo halikuwa lengo la kuanzishwa kwake. *(Makofi)*

Kutokana na sababu hizo Mhe. Mwenyekiti, basi serikali kupitia Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko italeta mswada hapa baada ya kufanya tathmini yakinifu, ili tuone shirika

hili linavunjwa kama azma ilivyotangazwa kwenye bajeti ya mwaka 2012/2013 ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Nam. 81

Huduma za *ICU* Hospitali ya Mnazimmoja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Mwenyekiti, ahsante kabla kujibiwa swali langu naomba nifanye marekebisho kwenye kifungu cha (b) na uniruhusu kwa heshima ya hali ya juu niseme machache.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa heshima na taadhima kabisa ya hali ya juu nimpongeze Waziri dhamana wa wizara hii aliyewahi kujitolea muhanga kuwa pindipo isingejengwa *ICU* katika kipindi muafaka yuko tayari kupoteza uwaziri wake. Kwa kweli ni waziri wa kupongezwa na kupigiwa mfano. *(Makofi)*
Hili la pili ambalo alizungumza Mhe. Saleh Nassor Juma hivi juzi hata hili la chakula nafikiri kwa Waziri huyu halitomshinda kutokana na utendaji wake.
Hospitali ya Mnazimmoja ndiyo inayotegemewa sana katika nchi yetu kama Hospitali ya Rufaa na ndiyo kimbilio la wananchi wetu wanyonge na masikini. Kwa muda mrefu Hospitali hii imekuwa inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo ukosefu wa madaktari bingwa na wataalamu wa *ICU*.

(a) Je, hadi hivi sasa kuna wataalamu wangapi wa *ICU* katika Hospitali ya Mnazimmoja.

(b) Je, Serikali haioni kuwa ukosefu wa wataalamu wa *ICU* ni kupoteza maisha ya wananchi wetu ambao hawana uwezo wa kupata huduma hiyo nje ya nchi.

(c) Serikali ina mpango gani wa muda mfupi na muda mrefu wa kuongeza wataalamu katika kitengo cha *ICU* ili kunusuru maisha ya wananchi wetu masikini wanaopelekwa pale.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, tunaomba utupe maelekezo ya kujibiwa swali lako lijibiwe au liachwe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, swali lijibiwe ni la wananchi hilo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 81 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

- *ICU* Mnazi Mmoja ina daktari wawili, ambapo ni mzalendo mmoja na mgeni mmoja, kuna wauguzi 7 ambao wanaofanya kazi katika sehemu hii ambao nao pia wamepata mafunzo. Wafanyakazi wengine ni manesi waliosomea mafunzo, ambapo katika fani ya kutoa nusu kaputi na baadhi ya manesi wa kawaida ambao wamepata mafunzo mafupi wakiwa kazini "*On job training*".

Kwa hiyo, manesi hawa wote wanaweza kutoa huduma wakiwa *ICU* au wodini. Lakini wagonjwa wa *ICU* hawategemei daktari huyo na manesi hao tu, kwa sababu wao hawatibu maradhi ya mgonjwa ila wananusuru maisha ya wagonjwa wenye matatizo mbali mbali pale hali inapokuwa mbaya.
Kwa kawaida mgonjwa hutibiwa na daktari anayehusika na tatizo lake na daktari wake humpeleka *ICU* kwa msaada dharura inapotokea. Daktari huyo anapaswa kumfuatilia mgonjwa wake akiwa *ICU* kumuendelezea matibabu wakishirikiana na daktari huyo wa *ICU*, na hali inapotengemaa mgonjwa hutolewa chumba hicho na kupelekwa kwenye wodi aliyotoka kuendelea na matibabu yake.

- Mhe. Mwenyekiti, neno kutoa muhanga kwenye taaluma zetu za afya hakuna.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri, tayari Mhe. Mjumbe ameshafanya marekebisho. Kwa hivyo, ameelekeza kwamba tufanye marekebisho na iwe kupoteza maisha ya watu na sio kutoa muhanga tena na aliondoa neno hilo. Tuendelee Mhe. Waziri kujibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kama hakuna neno kutoa muhanga basi tutafute neno linalofanana na hilo, basi tunahatarisha maisha ya watu kwa mujibu wa swali lake lilivyokuwa.

- Sasa tunachokifanya katika *ICU* kwanza upungufu wa wafanyakazi haupo, kwa hiyo huko kuhatarisha maisha hakupo. Kwa kweli wafanyakazi tulionao bado wanajitahidi kuhakikisha wale wanaoletwa katika hali ya kuweza kunusuriwa wanapata huduma na wanatoka *ICU* wakiwa hai.

Kwa vile *ICU* ni kitengo chenye kutoa huduma ya dharura pale mgonjwa anapozidiwa, kwa hali yake mgonjwa inavyokuwa sio wasia kumsafirisha. Labda wenye mgonjwa walazimishe nao watashauriwa msubiri mpaka hali itengemae. Hayo yanafanyika kuhakikisha huko anakokwenda mgonjwa atafika akiwa hai. Lakini wenye mgonjwa waking'ang'ania basi hupewa mgonjwa wao na huambiwa kutia saini kwenye faili la mgonjwa kama ushahidi kwa pale lolote litakapotokea.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Wajumbe wa Baraza hili kwa taarifa hao wanaotaka wangojwa wao watolewe ICU na kuwasafirisha mara zote huwa ni wale wenye uwezo na sio wasiokuwa na uwezo.

Mhe. Mwenyekiti, wanafundishwa kila inapotokea nafasi mafunzo ambayo yanafanywa na madaktari bingwa kutoka Uingereza na Uturuki kila mwaka wanapokuja na pia wanasomeshwa nje ya Zanzibar. Hivi sasa kuna wafanyakazi wawili ambao wapo Muhimbili wanachukua Shahada ya Pili katika kitengo cha wagonjwa Mahututi, matumaini yetu kwamba wakimaliza watarudi.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kwa vile muda wa Maswali na Majibu umemalizika naomba sasa tuendelee na taratibu nyengine zilizobakia. Kabla sijamkaribisha katibu ningependa kutoa matangazo yafuatayo.

Kama ilivyokawaida yetu leo tumefikiwa na wageni kutoka Umoja wa Wanamaji wastaafu wa Zanzibar ikiwa ni jumla ya wageni 20. Wageni hawa wanaongozwa na Kepteni Feteh Saad Kilindo akiwa kama ni Mwenyekiti, pia wanasaidiwa na *Leading Siemen* ndugu Juma Khamis Juma ambaye anakuwa kama ni Katibu. Wote kwa pamoja wako hapa siku hii ya leo. Tunakukaribisheni sana hapa katika Baraza la Wawakilishi na nna imani kwamba mmefarijika, katika kipindi cha Maswali na Majibu, kama ambavyo mmeshuhudia.

Taarifa ya pili ni kwamba Waheshimiwa Wajumbe wote mnaarifiwa zoezi la uandikishaji kwa ajili ya vitambulisho vya Taifa bado linaendelea na leo linafanyika katika chumba cha Kamati Nam. 2 pamoja na chumba cha kusomea. Namna ambavyo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mlijaribu kuhudhuria jana mahudhurio yenu bado hayatii moyo katika suala zima la zoezi hilo. Kwa hiyo leo mnaombwa kuendelea na utaratibu huo. Asanteni sana.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Shirika la Meli ya Mwaka 2012,

(Kusomwa kwa mara ya pili)

(*Majadiliano yanaendelea)*

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nataka nianze kwa kuungana na wenzangu kwa kuunga mkono Mswada ambao umewasilishwa na Mhe. Waziri wa Miundombinu. Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, nimesimama baada ya kusikia mijadala ya jana ambayo imeonekana kwamba baadhi yao imenigusa, naomba kidogo nifanye uwasilishaji kwa kutoa maelezo ili na mimi niweze kumsaidia Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze kwa kusema kwamba historia ya Shirika la Meli kaka yangu jana Mhe. Ali Mzee amelieleza kwa kina. Ukirudi nyuma tokea wakati wa ukoloni Zanzibar kulikuwa kuna meli mbili, kulikuwa kuna moja ndogo moja kubwa kaka yangu angeweza kuzitaja hata majina hizo meli. Lakini wakati wangu mimi nimeanza kuiona MV. AFRIKA na MV. UHURU halafu baadaye kukawa na Mapinduzi na Maendeleo.

Nataka niseme tu kwamba tayari tuna maagizo kwamba shirika hili tulifanyie ukarabati mkubwa sana ili liweze kujiendesha kibiashara. Umetolewa mfano kama tulivyolifanyia kazi Shirika la Benki ya Watu wa Zanzibar. Nakubali na mimi nilikuwa ni miongoni mwa watu waliokuwemo katika timu ile. Kwa hivyo na Shirika la Meli tutalifanyia kazi hiyo vile vile na tutalifanyia mapitio makubwa. Kwanza kabla hatujaanza kulifanyia ukarabati hili shirika tutalifanyia *Audit* tuweze kuliona kwamba lina nini na linadaiwa nini. Ili pale tutakapoanza kulifanyia ukarabati tuweze kujua maeneo gani ya kuweza kuyaimarisha. Vile vile nakubaliana na wenzangu waliosema kwamba Shirika hili linahitaji kuendelezwa kitaaluma hilo nalo ni muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, wengi labda huwa hawafahamu au hawaelewi lakini jana Mhe. Ali Mzee aligusa hapa kidogo akasema haya mashirika yote mwenyewe ni Waziri wa Fedha. Mimi namshukuru kwamba amesema mwenyewe ni Waziri wa Fedha angesema mwenyewe Omar Yussuf ingekuwa kidogo matatizo. Ni kweli mashirika haya nadhani yako manane, Serikali yetu

haya mashirika yapo chini ya Wizara ya Fedha na sisi tuna wajibu wa kuyaangalia mashirika haya jinsi ya utendaji wake kazi. Hivi sasa sisi sote ni mashahidi tayari tumepitisha hapa bilioni 17.166 kwa ajili ya ununuzi wa meli mpya. Fedha hizo sio kwamba zinatosha kununulia meli mpya lakini ni sehemu ya kununulia meli mpya.

Tumekubaliana kwamba tutakuwa tuna *account* ya pamoja ili kutakuwa wapo wenyewe Shirika la Meli pamoja na Wizara ya Fedha ili kuona kwamba mapato yote yatakayoingia tuweze kuyaona na kufahamu matumizi yake. Lengo letu hili Shirika nalo liendeshwe kibiashara. Ni moja ya Mashirika kweli kama alivyosema Mhe. Ali Mzee ni moja ya mashirika ambayo mimi nimeya- *classify* tayari yapo ICU. Lakini ni moja ya Mashirika ambalo linaweza likakarabatiwa likafanya kazi na likazalisha.

Mimi nakubaliana na maoni ya Wajumbe kwamba Shirika hili liachiwe lifanye kazi zake tutawasiliana na Wizara mama ili basi wao waangalie zaidi sera badala ya kuangalia zaidi utendaji na kuwaingilia ingilia. Ili liweze kufanya kazi zake ni dhahiri kwamba linahitaji kupewa nafasi ya kujiimarisha na kuweza kutekeleza majukumu. Nakata niwahakikishie Mhe. Mwenyekiti, kwamba kwa upande wetu sisi kama Wizara tunaosimamia masuala ya fedha tuko tayari kwamba tutakapofikia wakati wa kuanza kulikarabati hili shirika kwa wale watakaostaafishwa tutaweka fedha za kutosha ili tuweze kuwapa haki zao. Na wale watakaobakia tutaangalia elimu zao na tuweze kuimarisha utendaji kazi wao ili shirika liweze kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa muono wangu nna imani kwamba shirika hili litaweza kufanya kazi vizuri zaidi. Hivi sasa imeelezwa jana kwamba wana meli ya mafuta ambayo inawategemea lakini meli hiyo ikifika mwezi wa Disemba nayo vile vile haitoruhusiwa kutembea, kwa sababu meli ya mefuta ni *single hull* ni utaratibu kuanzia mwaka wa kesho meli zote za Mafuta zinatakiwa ziwe ni *double hull* kwa hivyo meli yetu baada ya hapo itakuwa haiwezi tena kutembea. Kwa hivyo tuna wajibu vile vile kama ni nchi kutafutia meli ya mafuta nalo vile vile tunalo katika serikali na tunalifanyia kazi ili shirika hili liweze kufanya kazi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, tayari serikali imeshatupa maelekezo baada ya kukamilisha upatikanaji wa meli ya kwanza tuanze hatua za kutafuta na meli ya pili. Nimesema mwanzo historia ya Zanzibar kuwa na meli mbili mbili za abiria. Kwa hiyo na shirika hili halitokuwa nyuma, tutafanya juhudi baada ya kukamilika kwa meli ya kwanza na tunategemea meli ya kwanza itajengwa katika kipindi cha miezi 14. Kama wenzangu walivyochangia jana tunajenga meli mpya na ni ya kisasa kabisa na baadae tutajenga meli ya pili ambayo itakuwa ni ndogo ya hiyo. Ili shirika hili liwe na meli zake mbili kama kawaida.

Kwa hivyo kununuliwa kwa meli isiwe tena ndio mtaji wa watu kujinufaisha. Lazima tutaweka macho yetu pale ili tuweze kuangalia meli hii inafanya kazi kibiashara na fedha ambazo zimetolewa na serikali kwa ajili ya kununulia meli hii basi zinarudishwa ili ziweze kufanya kazi katika shughuli nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka nieleze hayo na nataka niseme kwamba nakubaliana na Mswada huu mia kwa mia na mimi nauunga mkono na naomba wajumbe wenzangu wote tutakapo pitisha vifungu basi tuunge mkono ili kutupa nafasi tuweze kuliunda hili shirika na

liweze kuwa ni shirika lenye kutia tija na liweze kuisaidia serikali katika bajeti yake kama mashirika mengine. Kama nilivyosema wakati tunapitia ripoti ya PAC na wakati tunapitia bajeti nilieleza Mhe. Mwenyekiti, kwamba mashirika haya tutayafanyia tathmini moja baada ya moja, yale tutakayoyaona kwamba wanaweza kujiendesha kibiashara basi serikali itawasaidia wajiendeshe na yale tutakayoyaona kwa kweli hayawezi tena kujiendesha kibiashara basi tutalazimika tuyafunge ili tunusuru fedha za umma.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, aliyetuwezesha waja wake ambae ni viongozi wa wananchi wa Zanzibar kuja nasi kutoa mchango wetu katika kuitakia nchi yetu hatima njema.
Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wenzangu wa jimbo la Chwaka kuunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja kwa mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, madhumuni makubwa ya Mswada huu ni kuhuisha na kushajihisha maisha ya Wazanzibari, waliowengi tukiamini kwamba ni wanyonge, wanaotegemea usafiri wa baharini kwamba ndio nyenzo yao kuu katika mnasaba wa kuona kwamba kama serikali lazima tuwe tuna chombo chetu ambacho kitaweza kusimamia pamoja na kuelekeza katika taratibu na mwenendo mzima wa shughuli za usafiri katika baharini.

Mhe. Mwenyekiti, nimeangalia na kusikiliza kwa makini sana michango ya mawazo na fikira za waheshimiwa wajumbe. Wengi kati yao wamejengeka hofu kutokana na pengine na historia ya Shirika la Meli na Uwakala, kutokana na kumbukumbu pamoja na matokeo mengi ambayo yametokezea. Naomba nichukue nafasi hii Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwahakikishia Waheshimiwa wajumbe pamoja na wananchi wote wa Zanzibar kwamba dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuona kwamba yale makosa ambayo yametendeka yanapatiwa ufumbuzi nao ni ufumbuzi wa kudumu.

Nataka kuwahakikishia wananchi katika harakati za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mipango yake ya kununua meli hii mpya kumekuwa na mipango mizuri na mipango ambayo kuwa ni endelevu likiwemo la kwanza kama vile Mhe. Waziri anayeshughulikia na Masuala ya Fedha alivyoeleza. Maelekezo ya serikali ni kuona kwamba ili kuweza kuwa na meli itakayoweza kudumu na kuwa endelevu. Ni lazima Shirika hili lifanyiwe upya mapitio na mpango wake wa kibiashara. Kazi ambayo tayari kama Wizara au Shirika tumeshaanza kuifanya ili kuona kwamba tunakuja na mpango na utaratibu mzuri wa kibiashara. Ili kuona kwamba shiriki hili linakuwa endelevu na lenye kuhuisha lakini pia lenye tija na faida na kulitoa huko liliko sasa hivi kwamba lipo katika hali mbaya na mahututi.

Mhe. Mwenyekiti, ili tufanye kazi vizuri ni jambo lililowazi kwamba tutalazimika kuwa na *restructuring* juu ya shirika hili. Tutatafuta kila namna ya kuona shirika hili linabadilika katika muundo wake, mfumo pamoja na utaratibu wa kufanya biashara ili kuipa fursa eneo hili nalo kuonekana kwamba ile tija na malengo yaliyokusudiwa yanapatikana. Katika azma hiyo ule mkato ambao aliokuwa anauzungumzia Mhe. Waziri wa Fedha kwamba utaletwa katika Shirika

hili kwa ununuzi wa meli lakini sio kwa mfumo wa *grant* utakuwa kwa mfumo kama vile kwa mkopo. Kwa maana kwamba lazima shirika hili lijiendeshe na fedha zile zitaonekana kwamba zinajirejea kwa maana kwamba zinazalikana nyengine ili kuweza kupata chombo kingine na uendelevu wa mtaji ule. Haitakuwa azma ya serikali wala malengo ya serikali kuona kwamba tuingize fedha hizi za wananchi bilioni 17 tununue meli iwe *grant* tusiwe na mfumo wa kurejea tena serikalini katika uzalishaji na harakati nyengine za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, aidha sehemu kubwa ya wajumbe waliochangia wameonesha hofu yao juu ya suala la uadilifu na uaminifu kwa watendaji na viongozi wa Shirika. Nalo hili pia ni jambo la msingi na hatuna budi kama watumishi wa serikali kila mmoja wetu katika nafasi yake, katika wajibu wake atalazimika kulivaa suala la uwadilifu na uaminifu kama ndio sifa muhimu na kielelezo muhimu na cha lazima kwa mtumishi wa umma ili kujenga imani kwa tunaowaongoza na tunaowatendea kazi.

Mhe. Mwenyekiti, limezungumzwa pia suala la nembo na alama ya shirika hili kwamba zionekane zenye hadhi inayostahiki. Napenda nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba tutajitahidi kwa kadiri ya uwezo wetu kuona kwamba nembo na alama itakayodizainiwa iwe inakidhi mahitaji na hadhi inayotakikana.

Aidha, limezungumziwa suala la ku *audit* kama alivyozungumzia Mhe. Waziri wa Fedha nalo hili serikali tutalifanyia kazi kwa kugundua madeni yanayodaiwa shirika hili lakini pia madeni yanayodai shirika hili ikiwa pamoja na uhaulishaji wa mali ambazo sasa hivi vinamilikiwa chini ya mamlaka ya Wizara ya Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine la msingi ninalotaka kuzungumzia katika Mswada huu ni suala zima la uwakala. Naomba nikiri naamini kwamba Mhe. Waziri atakapokuja atakuja na ufafanuzi mzuri zaidi kwamba katika eneo hili ndio roho ya shirika lenyewe. Kwa bahati mbaya kwamba sote tulipitikiwa hakukuwa na kifungu *specific* ambacho kina *exclusive* kwa maana kwamba biasahara ya uwakala iwe inafanywa na shirika hili.

Pili tukiondoa biashara hiyo ya uwakala shirika letu hili litayumba. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti atukubalie kukiingiza kifungu hicho kipya lakini pia atukubalie kupita Mswada huu ili kulipa shirika letu nguvu ya kufanya kazi za meli za usafirishaji lakini pia na shughuli za uwakala.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine limezungumzwa ni suala la kusomesha watendaji. Hili hatuna namna ya kuliepuka ili tuwe tuna chombo makini kilichoimara, ni lazima kusomesha watendaji na utaratibu huu ndio utakaotupa uendelevu na mategemeo ya maendeleo tunayoyataraji.

Mhe. Mwenyekiti, katika mnasaba huo wa kusomesha watendaji lazima tubadilike na muundo wa utumishi katika shirika hili. Kwa upande wa mabaharia lazima tufate ule utaratibu wa kimataifa unaotumika kwa mtindo wa ku- *sign on* na ku-*sign off* , hatutokuwa tuna shirika jema wala shirika lenye tija tukiendelea na utaratibu wa sasahivi wa kuwa na watumishi wa kudumu katika sekta au katika eneo hili la ubaharia. Lazima tuende na mfumo wa kusajili mikataba kwa muda maalum na baadaye kushuka watu katika meli na kwenda kufanya shughuli nyengine na

sio watumishi wa kudumu. Kwani kufanya hivyo kutapelekea tija na faida na yale matumizi yasiyokuwa ya lazima kwa upande wa shirika.

Suala jengine limezungumziwa ili kuwa na chombo imara ni vyema serikali kueleza mpango wa kupatikana bandari mpya suala hilo nalo tayari tumeshalieleza kwamba serikali tuko mbioni kutafuta wabia na washirika wa maendeleo katika haraka za kuona tunajenga bandari mpya ya Mpigaduri. Harakati za kwanza tumeweza kufanya MOU na kampuni wametuletea gharama, gharama ambayo kwa upande wa serikali imeona ni kubwa. Tunaendelea na utambuzi yakinifu baadae kwa kuweza kujua gharama na matarajio yetu kwamba watu ambao wamejitokeza na nia hii ya kutaka kujenga bandari yatasimama ili kuendana nasi katika makubaliano hayo kwa mjibu wa maelekezo ambayo tutaweza kupatiwa na wataalamu wetu kwa maeneo husika.

Mhe. Mwenyekiti, limezungumziwa pia suala la kuwa na watendaji ambao kuwa watakuwa na sifa. Imani yetu na matarajio yetu kwamba baada ya kuwasomesha watumishi hao na watendaji hao watakuwa wenye sifa zinazostahiki, ambayo malengo ya serikali ni kupata tija kutokana na shirika hili.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba madhumuni makubwa ya Mswada huu ni kuleta kwetu kama ni Wawakilishi kuweza kuupitia, kutafakari kifungu kwa kifungu na kwenye mapungufu mengi ambayo yameonekana yaliyokuwa katika *top graph* pale kwa maana kwamba masuala ya kiuwandishi tutakuwa tumeyapokea na tunaamini tutakapopitia katika vifungu tutapata fursa ya kuchambua kwa kina vile tofauti za maandishi na maono ya Waheshimiwa Wawakilishi ili kuweza kupata ufanisi uliokuwa mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache naomba nikiri tena kwa kurejea kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja kwa mia moja. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Wakati nataka kumkaribisha Mhe. Waziri niliwaomba wale wanadhimu wa vyama watusaidie wajumbe waweze kurudi humu ndani. Mhe. Waziri anapomaliza tuweze kupitisha vifungu, hatutoweza kufanya zoezi hilo bila ya wajumbe kukamilika humu ndani. Kwa hiyo kuchukua fursa hii kuwaomba tena wanadhimu wahakikishe watu wao wanarudi humu ndani na tuweze kumaliza kazi iliyobakia.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuweza kuleta majumuisho. Kwanza tunamshukuru Allah kwa kutupa uhai na uzima. Pili na mimi napenda nisisitize maneno uliyoyasema kwamba sasa hivi tunajaribu kupitia hoja moja baada ya nyengine na bahati ni kwamba wajumbe hawajakuwemo wa kutosha, kwa hivyo aliyekuwa ameshachangia na ameshajibiwa itakuwa ndio imeshamaliza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mwenyekiti, na Kamati kwa jumla ya Mawasiliano na Ujenzi kutokana mjadala wa kina ambao tuliufanya kwa ajili ya Mswada huu. Napenda niseme kwamba mapendekezo yao kama ambavyo yaliyooneshwa katika karatasi hii tunakubaliana nayo ili tuweze kufanya marekebisho katika Mswada wetu.

Baada ya hapo napenda niwatambue wote ambao walichangia Mswada huu wa Kuanzishwa kwa Shirika la Meli Zanzibar nao ni:

- Mhe. Marina Joel Thomas
- Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
- Mhe. Subeit Khamis Faki
- Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
- Mhe. Fatma Mbarouk Said
- Mhe. Hijja Hassan Hijja
- Mhe. Abdallah Juma Abdallah
- Mhe. Saleh Nassor Juma
- Mhe. Mgeni Hassan Juma
- Mhe. Asha Bakari Makame
- Mhe. Abdalla Moh'd Ali
- Mhe. Hamad Masoud Hamad
- Mhe. Waziri ya Fedha na Uchumi
- Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano

Mhe. Mwenyekiti, kama tulivyosema sisi tuyakubali mapendekezo yaliyotolewa kwa maandishi na Kamati hii ya Mawasiliano na Ujenzi ili kuweza kuweka sawa huu Mswada katika maeneo tofauti.

La pili kubwa ambalo alilitaja Mhe. Naibu Waziri ambalo ni mchango uliotokana na Mhe. Hamad Masoud kwamba kipo kipengele cha uwakala kimesahauliwa. Kwa hivyo sisi tunaungana na Mhe. Hamad Masoud Hamad ili kukiingize kipengele hicho ambacho kitaeleza kwa ufasaha kabisa Shirika na uhusiano wake na Uwakala wa Meli.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na baadhi ya wajumbe niliowataja. Mhe. Mshimba alipendekeza kwamba uwezo wa kutunga kanuni ni Waziri na sio Bodi. Tunasema kwamba marekebisho yatafanywa na ushauri alioutoa wa muhuri na nembo ziwe za kisasa ambazo zitakazokuwa sio rahisi kuigika. Ushauri huo umechukuliwa na kazi itafanywa. Kuhusu malipo yatakayofanywa katika shirika yanagawika maeneo mawili. Kuna malipo ambayo zaidi yanatokana na uwakala ambazo hizi ni meli za kigeni zinalipa kwa pesa za kigeni vile vile lakini malipo ya ndani yanafanywa kwa pesa za Kitanzania pamoja na adhabu. Hoja ya Mkurugenzi Mkuu kuwa na taaluma hili ni jambo ambalo limezungumzwa katika sheria. Kwa sababu anateuliwa na Mhe. Rais hakuna wasi wasi wowote kwamba wale wanaomshauri wanampa ushauri uliokuwa ni sahihi.

Mhe. Subeit Khamis Faki alitoa mchango kwamba serikali iliwezeshe shirika kujitegemea na kuweza kuhimili ushindani wa kibiashara. Moja kati ya kazi kubwa ya serikali ni kuweka mazingira ambayo hili Shirika litajitegemea na mojawapo ni hii tutayoanza sasa hivi ni kutunga sheria ambayo italifanya shirika liweze kujitegemea kuliko pale lilipokua. Kwa hivyo ni dhahiri kwamba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na serikali kuu kwa jumla ina muelekeo wa kulifanya hili shirika liweze kujitegemea na kuweza kuhimili ushindani wa kibiashara.

Mhe. Mahmoud ambaye leo ni Mwenyekiti, kifungu cha 3(2) d uwezo wa kuingia katika mikataba umewekwa kwa shirika na sio bodi. Uwezo wa kuingia mikataba ni uwezo wa shirika kwa hivyo shirika ndio taasisi yenyewe ambayo ndio yenye sifa ya kuweza kukopa na kushtaki na kushtakiwa. Aidha bodi inasimamia shughuli zote za Shirika, kwa hivyo inayopaswa hasa kuingia na mkataba ni shirika wenyewe.

Mhe. Fatma Mohammed Mbarouk baada ya kufunga hesabu zake alikuwa na hoja hiyo kwamba Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa ajili ya mapitio, ushauri umepokelewa kwani ndio utaratibu wa kawaida wa shirika, kwamba baada ya kukamilika kufunga hesabu zake kuziwasilisha kwa Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa ajili ya mapitio.

Mhe. Hija ambaye alisema kifungu namba 3(2) c neno kuhodhi libadilishwe na lisomeke kumiliki, pendekezo limekubaliwa na tunahakikisha kwamba neno kumiliki ambalo lina-*sound* vizuri zaidi litaweza kufanyika.

Mhe. Mwenyekiti, kuna hoja nyengine hapa kifungu cha 7 neno gharama nafuu lilipendekezwa liondoke na badala yake lisomeke kwa mujibu wa gharama zinazostahili. Limekubalika na marekebisho hayo yatafanywa. Kifungu cha 8 ‘c’ neno riba liondoke litafutwe neno jengine, tumewaachia kazi wanasheria ili waweze kutafuta neno ikiwa lipo zaidi ya hilo.

Hoja ya kifungu cha 9 hii itakuwa cha kulazimisha. Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki kilirekebishwa wakati tulipokuwa na mjadala na kamati. Kifungu chenyewe *marginal notes* ilikuwa uwezo wa kulazimisha, lakini tulipoitizama sheria ya kiingereza ilionekana kwamba hakukuwa na haja ya kutumia maneno haya kwa hivyo moja kwa moja ikarekebishwa na kufanywa kwamba Shirika litatoza nauli na malipo kwa huduma za meli. Kwa hivyo hakuna haja ya kuzunguka maneno mengi moja kwa moja tunakwenda kwa kile kipengele ambacho kwa bahati nzuri yalionekana wakati wa mjadala na kamati.

Mhe. Mwenyekiti hoja nyengine ilikuwa kifungu namba 13(11) d Bodi iwe na jukumu pia la kuwapatia adhabu wajumbe watakaohujumu pato la shirika. Hoja tayari imezingatiwa kwa mujibu wa sheria ya mitaji ya umma.

Mhe. Mwenyekiti hoja ya sita kwa hapo hapo ilikuwa namba 19 Kamishna aliyetajwa ni Kamishna gani, hapa anasema Kamishna ametajwa katika kifungu namba 2 cha ufafanuzi maana yake ni Kamishna aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 15 cha sheria ya mitaji ya umma namba 4 ya mwaka 2002. Hoja namba 7 kifungu namba 13(2) tunakubaliana na hoja yako kwamba neno linaweza liondoke na lisomeke litaanzisha.

Mhe. Abdalla Juma ninakushukuru kwa michango yako kifungu cha 11(e) uwezo wa utungaji wa kanuni za umma ni uwezo wa Tume ya Utumishi kwa nini uwezo huo umepewa Bodi. Jibu, Bodi zinapewa uwezo wa kutunga kanuni zao za utumishi kutokana na sheria ya mitaji ya umma.

Hoja nyengine ilikuwa kifungu namba 17(2) kioneshe miezi mitatu kabla ya kufunga hesabu ya mwaka ya fedha yawasilishwe kwa mkaguzi wa hesabu. Maelezo hayo tayari yameshaelezwa katika kifungu 17(1).

Mhe. Mwenyekiti nikiendelea na hoja ambazo zimetolewa na baadhi ya Wajumbe naingia kwa Mhe. Mgeni Hassan Juma hoja yake ilikuwa shirika liweze kuingia ubia. Hoja hii imepokelewa na kuzingatiwa lakini ni kwamba Shirika linatakiwa lijitegemee na kwa hivyo litakuwa na Bodi ambayo ndio itakayotoa maamuzi haya wakati wowote itakapoona kwamba hali inaruhusu.

Shirika litenge kiwango maalum kwa ajili ya maendeleo ya jamii hii ni kitu cha kawaida kwa hivyo inategemea sasa na uwezo wa shirika wenyewe. Lakini kama tulivyosema mwanzo kwamba sheria hii inalianzisha Shirika la Meli jipya kwa hivyo tunategemea kwamba litafanya faida na ikiwa halifanyi faida ina maana litakuwa halina uwezo wa kuchangia chochote. Kwa hivyo ni juu yetu kwa wizara na serikali kwa ujumla kuliona kwamba shirika linatengeneza faida na sio kutumia mtaji.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali kifungu cha 10(2) (d) Mjumbe kutoka wizara inayohusika na mambo ya meli aondolewe. Hii inafanywa kuitilia nguvu ile bodi yenyewe kwa sababu kama ambavyo wajumbe wengi walidai hapa kwa shirika sasa lijitegemee, shirika liweze kujiendesha, shirika lisiwe linamilikiwa na mtu binafsi. Sasa kutokana na *experience* ya nyuma ambayo mambo yaliyokuwa yakienda ni kwamba Mkurugenzi Mkuu ndiye mwenyewe peke yake yeye ambaye anaingia katika bodi. Sasa ili kuhakikisha kwamba lile shirika linawekwa katika hali nzuri basi anaingizwa huyu mjumbe kutoka wizarani, kuhakikisha kwamba *import* zake zinafanyika. Lakini itakumbukwa kwamba katika kifungu chengine ambacho ni muundo wa bodi ambapo ilipendekezwa na kukubaliwa katika mjadala wa kamati kwamba kutoke wajumbe wawili kutoka sekta binafsi kwa hivyo hii itatilia nguvu ule uwezo wa bodi wa kuweza kukiendesha chombo kwa ufasaha na kwa ufanisi zaidi.

Jengine ambalo lilitajwa katika michango ya Waheshimiwa Wajumbe mchango wa Mhe. Hamad Masoud kama tulivyoutaja mwanzo tumeupokea na marekebisho yale ya kifungu cha uwakala tumekubaliana nae kwamba yafanywe marekebisho ili kazi ile ya uwakala iweze kutajwa kwenye sheria hii.

Mchangiaji wa jana wa mwisho alikuwa Mhe. Ali Mzee, kwanza tunashukuru sana kwa kutupa historia ya usafiri wa meli hapa Zanzibar na utaratibu mzima wa uendeshaji wa Shirika hili la meli ambalo tunalitajia. Ni dhahiri kwamba uadilifu wa viongozi watakaochaguliwa uaminifu wa wafanyakazi kwa ujumla hali ya uajiri ndio mambo ambayo yatakayopelekea kuwa chombo kipo makini. Tokea mwanzo kama uajiri sio bila shaka hali haitowezekana. Kwa hivyo sisi kama wizara tutasimamia ile *restructuring* yaani kuliweka upya hili shirika, *staffing* yake itakuwa vipi, chombo hiki kiwe na wafanyakazi wangapi na kiwe na kada gani na uwezo gani.Sasa kutokana na hayo ndio ambayo yatapelekea uwajibikaji, kwa sababu ikiwa hakuna *structure* nzuri na uwajibikaji unakuwa hauji.

Shughuli za kuendesha shirika hili sasa hivi tofauti na miaka ya nyuma litakuwa linakabiliwa na changamoto kubwa ya ushindani wa kibiashara. Vyombo vingi vya kibinafsi sasa hivi na hasa Mhe. Mwenyekiti juzi tulipopitisha sheria ile ya miaka 15 ya chombo ina maana sana tunachechemua wale watakaoleta walete vyombo vizuri na kwa hivyo shirika hili pamoja na kuwa la kiserikali lakini litakabiliwa na changamoto kubwa ya ushindani. Ninaamini kama halijaendeshwa vizuri haliwezi kuchukua siku nyingi litalala, kwa hivyo ni kazi ya wizara na serikali kwa jumla kuona kwamba hili shirika linapambana katika ushindani huu wa kibiashara.

Lakini niseme kwamba kuwepo kwa meli katika serikali kunasaidia sana kuweka *stabilization* ya mambo mengi ni kama *regulatory board* kwamba hali ya usafiri kibei kwanza ndio kazi yake ndio muhimu sana kuhakikisha kwamba bei zinakuwa ni za wastani ukilinganisha na usafiri mwengine. Kwa sababu wananchi wetu wengi wapo katika hali ya chini. Sasa serikali kuwa na meli zake ni kwanza kuweka *stabilization* ya bei lakini pia kuweka hali ambayo wakati wa dharuba wakati bahari zinachafuka, kuwa na vyombo vilivyokuwa na muamana ya kusafiri baina ya visiwa vyetu na baina ya hapa na Dar es Salaam na kwengineko. Kwa hivyo tofauti na vyombo vya kibinafsi ambavyo hutegemea zaidi ile faida, kwa hivyo vyombo wanavyochukua ni vile ambavyo haviwezi kuhimili hali nzito ya bahari.

Lakini pia nasema kwamba ninamshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa ufafanuzi alioutoa kuhusiana na mustakbali wa Shirika hili la Meli kama nilivyosema mwanzo kulifanyia uanzishwaji wake wa muundo wake na hali yake ya ajira na pia juu ya suala la upatikanaji wa meli hizo zitakazokabidhiwa hili shirika kwa njia ile ambayo sio ile iliyozoeleka; ni njia ya kibiashara na njia ambayo itaweza kuhakikisha kwamba meli zile fedha ambazo wananchi walitoa zinarudi mikononi mwa wananchi na shirika linapata faida na kuliendesha.

Mwisho napenda nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa mchango wake alioutoa naomba sana Waheshimiwa Wajumbe waupitishe mswada huu ili hicho ambacho kilikuwa kinazungumzwa sana humu kwamba tupate shirika lenye uwezo ambalo haliendeshwi kibinafsi liweze kupatikana.

Kwa haya machache Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

UTARATIBU

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Mhe. Waziri kutoa hoja ambayo serikali imeunga mkono jambo ambalo ni zuri lakini tunataka kuingia kwenye kamati ya Baraza zima ambao tunataka kuamua. Kwa mujibu wa kanuni ya 71 (1), (2), ili Baraza liweze kuamua basi tuweze kufikia japo nusu. Wajumbe waliomo ndani si zaidi ya Wajumbe 30, kwa hivyo hatujafikia nusu na kwa hivyo hatuwezi kuamua maamuzi ya mswada huu kwa mujibu wa kanuni hii.

Mhe. Mwenyekiti: Ni kweli kwamba kwa mujibu wa kanuni ya 72 kifungu kidogo cha kwanza hatutokuwa na uwezo wa kuliingiza Baraza katika kamati na kupitisha vifungu bila ya idadi ya Wajumbe nusu ya walengwa kuwemo ndani. Kwa msingi huo basi nitaomba kuliakhirisha Baraza hili kwa muda wa dakika 5 ili Wajumbe walioko nje waweze kurejea ndani na tuendelee na taratibu zetu.

Naomba kuliakhirisha Baraza kwa dakika 5.

(Saa 5:10 asubuhi Baraza liliakhirishwa kwa muda)
(Saa 5:25 Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa Baraza lako tukufu likae kama kamati ya kutunga sheria ili kupitia kifungu kwa kifungu.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kabla ya Baraza kama kamati kwanza tuwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale ambao wanakubaliana na hoja wanyooshe mikono, waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Meli Zanzibar
Kazi, Uwezo na Mambo mengine yanayohusiana na hayo

Sehemu ya Kwanza

Masharti ya Awali

Kifungu 1	Jina fupi na kuanza kutumika.
Kifungu 2	Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Pili

Kuanzishwa Malengo na Uwezo wa Shirika

Kifungu 3	Kuanzishwa Shirika pamoja na marekebisho yake
Kifungu 4	Muhuri wa Shirika
Kifungu 5	Makao Makuu ya Shirika
Kifungu 6	Malengo ya Shirika
Kifungu 7	Kazi za Shirika pamoja na marekebisho yake

Kifungu 8 Uwezo wa Shirika pamoja na marekebisho yake

Kifungu 9 Uwezo wa Kulazimisha pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tatu

Utawala na Uongozi wa Shirika

Kifungu cha 10 Bodi ya Wakurugenzi pamoja na marekebisho yake

Mhe. Hija Hassan Hija: Ninashukuru Mhe. Waziri kwa kutoa ufafanuzi na majibu ya hoja zetu vizuri sana, lakini inawezekana labda sikumfahamu, kwa hivyo naomba nipate ufafanuzi, niliomba kifungu cha 10 (4) kwamba mtu hatofaa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti isipokuwa awe na elimu na uzoefu katika mambo ya usafiri wa baharini, uongozi na utumishi wa umma. Nitoe wasiwasi kwamba ukisema awe na elimu tu wapo watu waliosoma elimu ya ngombaro na tunawatambua, kuna watu wamesoma elimu za madrasa tunawatambua na kuna elimu mbali mbali. Kwa hivyo ninapendekeza kwamba katika dunia ya leo na nchi inavyokuwa tuseme angalau awe na kiwango cha elimu ya Diploma badala ya kuweka wazi kwamba awe na elimu.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na hoja yake lakini hili ni Shirika sio taasisi kama ile tuliyoipitia juzi ya kitaalamu ya usafiri baharini, hili ni shirika ambalo linaweza kuwa mtu wa biashara, mtu wa *management*, mtu wa meli kwa hivyo elimu inakuwa ni kitu tofauti kidogo na ile taasisi ambayo ni ya kitaalamu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, tunataka kuchagua Mwenyekiti wa bodi ambaye anasimamia wataalamu wa shirika, ukiangalia Mkurugenzi na timu yake bila shaka watakuwa wataalamu na tumesema kule kwamba lazima shirika hili liende kitaalamu kulingana na mahitajio ya nchi yetu kwa hivyo lazima tuweke Mwenyekiti wa Bodi atakayefahamu na kusikia angalau lugha zinasemaje. Unaweza ukawa na wataalamu katika shirika lakini Mwenyekiti wa Bodi akawa haelewi lugha wanayozungumza wataalamu. Kwa hivyo mimi nashawishika sana kwamba tumuweke Mwenyekiti wa Bodi angalau mwenye elimu ya diploma ili angalau lugha za wataalamu kwa shirika aweze kuzisikia kwa karibu. Kwa hivyo hoja kwamba hili ni shirika sio la kitaalamu mimi naona ni hoja dhaifu; kwa hivyo tumuweke Mwenyekiti wa Bodi angalau awe na diploma na hivi ndivyo tunavyokwenda katika dunia ya leo, tusiwe nyuma kila siku.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Nakubaliana na hoja yake.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati jana nilipokuwa ninachangia nilizungumzia kuhusu huu muundo wa hii Bodi na kwa kweli leo naona hiki kipengele cha 10 kifungu kidogo cha 2 (d) miongoni mwa wajumbe ni kwamba inazungumzia mjumbe mmoja kutoka wizara inayohusika na masuala ya meli, sasa hii Mhe. Mwenyekiti naomba kipengele kiondoshwe kwa sababu itakuwa *interference* kwa sababu hii bodi inazungumzia mambo mengi sana yanayohusiana na shirika na itafanya maamuzi kwa hivyo itakuwa *interference* hapo kwa msingi huo anaweza aka-*create conflict of interest* ndani ya Bodi huyu. Kwa hivyo naomba Mhe. Mwenyekiti mjumbe huyu asiingie anayetoka Wizarani.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti kidogo mimi inanipa tabu kufahamu hii *concept* kwa sababu hili Shirika la Meli linataka kusimamiwa na maelezo mengi ya Wajumbe wetu jana walisema hili liliopo lilikosa usimamizi kwa hivyo meli zimeuzwa, zimeharibika zimefanya hivi. Sasa katika Bodi yule tuliyemkabidhi chombo ndio yumo Mkurugenzi Mkuu wa Shirika, sasa huu upande wa serikalini atakayesimamia ni nani kama si ile Wizara yenyewe. Pale kawekwa asimamie kile chombo kiwe kinakwenda katika malengo ambayo yanakubalika ndio kazi yake. Kwa sababu wajumbe wote hawahusiki na ile wizara. Kwa hivyo huyu kawekwa ili asimamie yale maslahi ya wizara na serikali kwa jumla katika kile chombo ambacho tunakiendesha wenyewe.

Hapa bila shaka atakuwa amepunguziwa uwezo kidogo yule Mkurugenzi Mkuu au Meneja Mkuu kwa kukiendesha kile chombo kwa namna ambavyo ilisemekana jana kwamba kilikuwa kinaendeshwa kwa ubinafsi zaidi. Kwa hivyo hapa ni *control factor* sasa kidogo inanichanganya kwamba akiondosha yeye kutakuwa na *control factor* gani ya hiki chombo. Kwa sababu Mkurugenzi atakayekuwa atakuwa na watu wengine ambao watakuwa hawamo katika ile wizara.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti nilichokizungumzia humu kwamba huyu ni vyema kumtoa kwa sababu anaweza aka-*create conflict of interest* ndani ya Bodi. Kwa hivyo katika hili mimi nilikuwa naomba maagizo ya Bodi yapelekwe katika shirika sio kwamba kuwe na mtu alinde maslahi ya shirika mule. Kuna wataalamu wa kutosha na Mkurugenzi kwa mujibu wa sifa ambazo tumezipendekeza ziwekwe ni mtaalamu aliyebobea katika masuala haya ya *navigation* na usimamizi wa mambo ya mashirika. Kwa hivyo mimi nadhani Waziri asiwe na wasiwasi katika hili. Mimi ningeomba amtoe huyu kusudi aipe nafasi bodi kufanya kazi zake kitaalamu kuliko kusimamia maslahi yao binafsi katika shirika. Hili bado naomba sana Mhe. Mwenyekiti kwa heshima kubwa na unyenyekevu wa hali ya juu huyu mjumbe tumtoe.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti baada ya kuzungumza mimi nataka ufafanuzi zaidi kutoka kwa Mwanasheria Mkuu lakini mimi nilivyosema katika maelezo yetu ya awali ya kuhudhurisha huu mswada tulisema umekuja kutokana na *transport master plan* yetu. Sasa nani atakayesimamia *transport master plan* ndani ya wizara kutokana na hili shirika ikiwa mjumbe wa wizara hayumo. Kwa hivyo huyu kawekwa makusudi kwa ajili ya kukidhi ile haja ya usimamizi na kupeleka zile *policy* za wizara katika shirika. Lakini ikumbukwe kwamba hii Bodi ina wajumbe wengi na yeye ni mmoja tu, kwa hivyo sidhani kama atakuwa na maamuzi ambayo yataweza kukiondoa kile chombo pahali pake. Lakini kwa ufafanuzi zaidi Mwanasheria atupe maelezo kidogo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani Mhe. Waziri katoa ufafanuzi mzuri kusema kweli sijui kama nitakuwa na ufafanuzi mzuri zaidi kuliko huo, na wasiwasi wa Mhe. Saleh Nassor inawezekana ni wa msingi, lakini msingi wake mkubwa ni kwamba asingependa *interference* ya wizara. Sasa sidhani kama waziri atapenda *interference* ya wizara. Kwa hivyo nadhani ni suala la kuchagua mtu gani ambaye atafaa katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na *coordination* baina ya wizara na shirika. Na mimi Mhe. Mwenyekiti naomba nikumbushe tu hapa kwamba ni sisi humu ndani ya Baraza tunakuwa wakali kwa Waziri, inapotokea shirika lake limefanya makosa.

Sasa nadhani anapokuwa na mtu wa kumsaidia kujua kinachoendelea ndani ya shirika yule mtu kutoka ndani ya wizara ndio madhumuni yake ya kusaidia hilo. Kwa sababu vyenginevyo tutakuja kumhukumu waziri bila ya kumpa nyenzo kuweza kusimamia lile shirika lenyewe, lakini anapokuwa na yule mtu anamsaidia yeye kulisimamia shirika kwa karibu zaidi.

Lakini la tatu, tukumbuke kwamba vikao vya bodi vinafanya maamuzi kutokana na *quorum* lakini kinafanya maamuzi kwa kuzingatia idadi ya wajumbe. Huyu mjumbe kutoka wizara haya kura ya *veto* ana kura ya kawaida katika maamuzi na ukitizama hii *composition* ya bodi yenyewe mjumbe wa wizara ni mmoja. Kwa hivyo, mimi sioni kama kutakuwa na hofu ya kwamba kutakuwa na shirika halitoweza kufanya kazi kwa sababu ya huyu mjumbe wa wizara, isipokuwa nadhani tukubaliane kwamba itamuwezesha waziri kufanya yale ambayo tunamuwajibisha ndani ya Baraza hili nao ni usimamizi wa shirika kwa karibu zaidi ili liweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Kwa hivyo, mimi nadhani Mhe. Saleh Nassor atakubaliana na mimi kwamba kuwepo kwa mjumbe wa shirika ni muhimu na katika kufanya maamuzi yeye hana kura ya *veto,* isipokuwa ana kura ya kawaida na sioni kama itaathiri ufanyaji wa maamuzi katika bodi. Ahsante sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, uzoefu wangu unaonesha kwamba wizara ipo njia ilikuwepo na itaendelea kuwepo, lakini wizara nzima kama imeshindwa kusimamia Shirika la Meli kupitia ile *Presidential Decree* ya mwaka 1983 na ikalifikisha mpaka lilipofika sasa, ikiwa wizara nzima ilishindwa kusimamia na kuli-*maintain* huyu mtu mmoja tutakaempeleka pale atasaidia nini. Mimi bado najenga hoja kwamba huyu atolewe na hawa wataalamu waliomo katika hii bodi wajumbe naamini ni wataalamu wataisaidia sana wizara na kulisaidia shirika kuweza kudumu kuliko kumuweka huyu, huyu ataleta maslahi ya wizara tu ambapo wizara imeshindwa kusimamia hili shirika mpaka limekufa tumeleta sheria hii Mhe. Mwenyekiti, ikiwa wizara nzima imeshindwa je mtu mmoja huyu jamani.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe mimi naona tufanye kitu kimoja katika kukisaidia kiti, kwa sababu inaonekana kwamba ni jambo la msingi kuwepo wakala au mwakilishi kutoka ndani ya wizara katika bodi ambayo itakuja pale kuja kuangalia utaratibu wa maendeleo ya wizara yenyewe. Lakini yule mwakilishi ambaye yuko pale ndio yule kwa mujibu wa maelekezo haya ambapo hata Mwanasheria Mkuu na Waziri alikuwa amezungumza ni yule Mkurugenzi mwenyewe wa wizara, yeye ataweza kujibu hoja ambazo ile bodi itakuwa inataka ufafanuzi wake, utaratibu wake au mambo yale yalikuwa yameendeshwa vipi. Tutakapokuwa tunasema kwamba hakuna mwakilishi wa wizara katika bodi ile wale watakaokuwa wanakaa pale zile taarifa watazipata wapi? Hili itakuwa ni tatizo.

Mimi naona kwamba Mhe. Mjumbe tukubaliane na hoja kwamba huyu mwakilishi ambaye atakuwa wa wizara anayekuja kuingia katika bodi ana umuhimu wake na yeye vile vile, naomba Mhe. Mjumbe tukubaliane hapo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, sisi Wapemba tuna usemi unaosema “La kuwa haliwanwa”, kwa sababu nimejitahidi sana kutetea hoja yangu na umeendelea kuning’ang’aniza katika hili basi tuendelee.

Kifungu 10 Bodi ya Wakurugenzi na marekebisho yake

Kifungu 11 Uwezo wa bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 12 Uteuzi na Uwezo wa Mkurugenzi Mkuu pamoja na marekebisho yake

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri na Mhe. Saleh Nassor kwa kukubaliana, lakini kifungu cha 12 (2) (a) sifa za kuwa Mkurugenzi wa Shirika naomba Mhe. Waziri akubaliane kwamba sasa hivi kimeandikwa kwamba, "Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa ni muhitimu kutoka Chuo Kikuu kinachotambulika au taasisi inayolingana". Nikasema kwamba hapa Zanzibar licha ya mbali SUZA, Tunguu na wengineo wanaanzisha *short courses* kama diploma ya *Islamic Bank* sio *degree*, lakini ni *short course* na cheti kinatoka kama ni kutoka SUZA au kutoka Tunguu.

Kwa hivyo, tuseme wazi hasa kwamba uhitimu huo angalau ahitimu katika shahada ya kwanza ya Chuo Kikuu. Kwa sababu tukiweka hivi ilivyo naweza mimi nikawa mwanafunzi wa SUZA lakini nimetiwa kwa *short course*, kwa hivyo tuweke angalau *degree* ya kwanza kutoka Chuo Kikuu kinachotambulikana ili tuwape nafasi Wazanzibari wetu wenye fani hizi na viwango vya elimu kuweza kupata ajira, tusiandae miswaada tu kwa kumuangalia mktu aliyepo, hii nchi ni ya Wazanzibari tuwape nafasi vijana wetu waweze kupata ajira na wanasoma na wanajifunza. Mhe. Mwenyekiti ndio ombi langu hilo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mjumbe lakini napenda nimuarifu tu kwamba hili neno muhitimu lina maana kubwa sana hapa. Kwa sababu hiyo anayozungumza yeye ni kwamba hivi vyuo baada ya kuona kwamba pengine wana wanafunzi ambao sifa zao si nzuri kwa hivyo wanaanzisha *pre-courses* ili kuweza kuwanyanyua wale wanafunzi kabla hawajaanza *degree*. Kwa hivyo, ukisema muhitimu wa Chuo Kikuu moja kwa moja ni yule ambaye atatoka na *degree* yake.

Kuna *equivalence* ambazo zinakuwa sawa sawa na hiyo *degree*, hivyo hizo huwezi kuzikataa. Sasa lililokusudiwa hapa ni hilo analolizungumza lakini limeandikwa katika lugha ambayo ya kawaida tu.

Pia kuna vifungu vyengine ambavyo vinaambatana navyo avisome kwa pamoja (b) na (c), sasa akivisoma kwa pamoja hivyo vitampa ule upeo hasa wa kuiona hiyo hali. Lakini hilo analolizungumza limezingatiwa kabisa kabisa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, leo waziri yupo Mhe. Rashid Seif dhamira hii aliyeiandika ndiye aliyeandaa mswada kesho nakuja kukaa mimi sikuwahi hata kuandaa, tusiangalie dhamira yake tuka-*support* kwenye tafsiri aliyoikusudia yeye, kuna ugumu gani wa kusema aliyehitimu angalau *degree* ya kwanza, kuna ugumu gani. Kama kakusudia hivyo basi aweke maneno, lakini asitafsiri dhamira yake akafikiria na Mhe. Hija akija akiwa waziri atakuwa na wazo hilo sio hivyo. Kama lengo ni *degree* ya kwanza angalau basi aweke maneno *degree* ya kwanza.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mjumbe afungue ukurasa wake katika ile sheria ya Kiingereza kifungu hicho hicho. Humu imeandikwa hivi, *"A person shall be qualified to be appointed as Management Director,*

- *He/she is a graduate from a recognized university or equivalent from recognized institutions"*.

Kwa hivyo, likisema tu neno '*graduate'* limekwisha hilo, imetoka hiyo, ndio nikasema hilo neno liwazi likisema tu muhitimu pale kakusudia hii *graduate* kaitafsiri hivyo. Sasa ikiwa ni Kiswahili kimechezana basi, lakini akiambiwa ni muhitimu wa Chuo Kikuu ni *graduate* huyo hizi *course* nyengine huwa zinawekwa ni kama *pre-courses* ambazo zinasaidia kile chuo kuweza kuwanyanyua wale wanafunzi wake. Namuomba sana Mheshimiwa atukubalie *Inshaallah*.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo na tafsiri ya *graduate, graduate* maana yake angalau ni *degree* ya kwanza. Kwa hivyo, madhali Kiingereza inasema *graduate* kwa maana ya *degree* ya kwanza basi na Kiswahili atuwekee *degree* ya kwanza kuna ugumu gani. Ikiwa Kiingereza ambacho Rais anasaini ni *graduate* kwa maana ya *degree* ya kwanza ndio tafsiri yake hiyo, kwa nini Kiswahili asiseme maneno hayo. Hivyo Mhe. Waziri hajapatapo kusikia mtu akiambiwa amehitimu kumbe ni *Quran Class*.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, tunakubaliana tuendelee.

Kifungu 12	Uteuzi na uwezo wa Mkurugenzi Mkuu pamoja na marekebisho yake
Kifungu 13	Uteuzi wa Afisa Mwandamizi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 14	Uwezo wa waziri pamoja na marekebisho yake

SEHEMU YA NNE

Masharti ya Fedha

Kifungu 15	Mfuko wa Shirika pamoja na marekebisho yake
Kifungu 16	Makisio
Kifungu 17	Mahesabu na Ukaguzi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 18	uwekezaji wa Shirika pamoja na marekebisho yake
Kifungu 19	Taarifa za mwaka

SEHEMU YA TANO

Masharti ya Jumla

Kifungu 20	Kitabu cha Orodha ya bei pamoja na marekebisho yake
Kifungu 21	Uhaulishaji miliki za meli
Kifungu 22	Umiliki wa mali
Kifungu 23	Bidhaa zilizo katika himaya ya shirika pamoja na marekebisho yake
Kifungu 24	Ushikiliaji ofisi mikataba
Kifungu 25	Kanuni za nidhamu pamoja na marekebisho yake
Kifungu 26	Makosa na adhabu pamoja na marekebisho yake
Kifungu 27	Kosa kwa shirika au kampuni
Kifungu 28	Makosa na adhabu ya jumla
Kifungu 29	Uwezo wa kutunga kanuni

Kifungu 30 Kufutwa kwa tamko la sheria Nam. 3 la mwaka 1983 na kubakiza.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na hoja wanyooshe mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Shirika la Meli ya mwaka 2012

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Shirika la Meli ya mwaka 2012 usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji la Zanzibar 2012

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny: Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Mswada wa Rasimu ya Sheria ya kuanzishwa Shirika la Utangazaji Zanzibar ya mwaka 2012.

Mhe. Mwenyekiti, matangazo ya Vyombo vya Habari hapa Zanzibar yalianza mwaka 1945 kwa utaratibu wa kutoa matangazo kupitia vipaza sauti. Matangazo ya redio yalianza rasmi tarehe 15 Machi, 1951 wakati huo ikiitwa Sauti ya Unguja. Matangazo ya mawimbi ya masafa ya kati yalikuwa yakisikika nje ya mwambao wa Afrika Mashariki kuanzia mwaka 1965 baada ya

kuzinduliwe kituo cha kurushia matangazo cha Chumbuni. Mitambo hiyo ya kurushia matangazo imekuwa ikibadilika kiuwezo kutoka KW 2.5 hadi KW 5 na KW 10 kulingana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya jamii.

Kwa upande wa matangazo ya televisheni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha kurusha matangazo ya televisheni ya rangi mwaka 1973 na kuzinduliwa rasmi mwaka 1974 ikiwa ni nchi ya kwanza katika nchi za Kusini mwa Bara la Afrika yenye televisheni ya aina hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, vyombo vya utangazaji vya Sauti ya Tanzania Zanzibar na Televisheni Zanzibar vimekuwa vinamilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vikiwa chini ya wizara moja inayohusika na habari. Ingawa vyombo hivi tokea kuanzishwa kwake vimekuwa vikisimamiwa na wizara inayohusika na habari, jina la wizara limekuwa likibadilika mara kwa mara kulingana na mtizamo wa serikali inayoingia madarakani.

Aidha, Sauti ya Tanzania Zanzibar na Televisheni Zanzibar mara zote zimekuwa zikiongozwa na Wakurugenzi tafauti zikiwa na madhumuni na malengo yaliyolenga jamii katika kutangaza sera za serikali, kuelimisha jamii kwa njia ya habari na kuburudisha umma na vile vile kutangaza matangazo ya biashara na mengineyo ya jamii kwa ajili ya umma.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais wa Zanzibar kwa mamlaka aliyoanyo kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ameunda Shirika la Utangazaji la Zanzibar mwaka 2011 linaloongozwa na Mkurugenzi Mkuu na hivyo Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo imeona ni vyema kuwasilisha Mswada wa Sheria ya kuundwa chombo hicho.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Habari inawasilisha Mswada huu wa Sheria ya Kuundwa kwa Shirika la Utangazaji la Zanzibar kutokana na haya yafuatayo:-

- Kwamba serikali imesisitiza hoja ya kuviunganisha vyombo vya utangazaji vya Televisheni Zanzibar na Sauti ya Tanzania Zanzibar kwa kuviwezesha kufanya kazi zake kwa ufanisi na kuviwezesha kusikika katika sehemu mbali mbali ndani na nje ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

- Kulipa Shirika la Utangazaji Zanzibar uwezo wa kisheria na kiutendaji katika kutoa huduma za habari, elimu na burudani kwa lengo la kuongeza nguvu ya kiutendaji ili kukabiliana na ushindani uliopo na hasa kwa kuwa shirika hili linaanzishwa kwa mswada huu chini ya sheria ya mitaji ya umma.

- Kulipa uwezo wa kisheria Shirika la Utangazaji Zanzibar ili kujiendesha kibiashara zaidi na kuliwezesha kukabiliana na mageuzi ya teknolojia ya utangazaji.

Mhe. Mwenyekiti, madhumuni makuu ya Mswada huu wa Sheria ni kuanzisha Shirika la Utangazaji Zanzibar kwa kuunganisha Sauti ya Tanzania Zanzibar na Televisheni Zanzibar. Madhumuni ya muunganisho huu ni kuwa na taasisi ya utangazaji wa umma itakayokuwa na nguvu katika kuimarisha utawala bora, uhuru, demokrasia na haki za binadamu kwa kupitia chombo hiki cha habari.

Mhe. Mwenyekiti, kuunganisha shughuli za redio na televisheni za taifa ni mfumo unaokubalika katika nchi zote za ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati. Vituo vya utangazaji vya televisheni na redio za kitaifa katika nchi hizo tayari zimeunganishwa katika mfumo wa Mashirika ya Utangazaji ya kitaifa. Mfumo kama huu pia upo katika mataifa mbali mbali duniani yanayoongoza katika shughuli za utangazaji wa redio na televisheni kama vile China, Uingereza, Ujerumani na kadhalika.

Mifumo kama hii ina tija kubwa katika kupunguza gharama za uendeshaji na watendaji wake wakiwemo maafisa uendeshaji, mipango, fedha pamoja na mafundi ambao wanakuwa katika shirika moja badala ya kila kitengo kuwa na watendaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, shughuli za utafutaji habari na utayarishaji wa vipindi ni msingi wa vituo vya utangazaji ambazo zikiendeshwa kwa pamoja zinapunguza gharama za utendaji. Sababu kubwa ni kwamba vitendea kazi vyote kama vile usafiri, kompyuta za kuhariri habari na vipindi vitatumika kwa pamoja. Hatua hii italeta ufanisi wa kisera wa kuwa na maudhui ya aina moja kwa wasikilizaji wa redio na watazamaji wa televisheni.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu unapendekeza yafuatayo:

Kwanza kukubaliwa mabadiliko ya kuunganisha Sauti ya Tanzania Zanzibar na Televisheni Zanzibar na kuwa na chombo kimoja kinachoitwa Shirika la Utangazaji la Zanzibar litakalosimamiwa na kuendeshwa chini ya Mkurugenzi Mkuu.

Pili, kuwepo na mhariri mkuu mmoja, mhandisi mkuu mmoja, meneja wa vipindi mmoja na meneja mmoja wa *program*. Na mwisho inapendekezwa kuwepo na kitengo cha utayarishaji vipindi na chumba cha habari kimoja kwa ajili ya kutilia mkazo misimamo ya kisera katika vipindi na taarifa mbali mbali zinazotolewa na chombo hicho kipya.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umepata baraka ya kuandaliwa na Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ambayo ilitoa mapendekezo kadhaa yaliyosaidia kuweka vizuri mswada huu. Miongoni mwa mapendekezo hayo Wizara ya Habari imeyakubali. Mapendekezo yote yaliyokubaliwa tayari yamewekwa kwenye jadweli ya marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 18 tumeamua kukifuta na kuandikwa upya ili kutoa fursa zaidi kwa shirika kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia mapendelezo ya Sera ya Habari ya mwaka 2006 na Sheria Nam. 2 ya mwaka 1997 ya Tume ya Utangazaji ya Zanzibar ambayo ndio inayosimamia na kuratibu shughli zote zinazofanywa na vyombo vya utangazaji vya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, rasimu hii ya sheria ina sehemu sita, sehemu ya kwanza inahusu utangulizi ikijumuisha jina fupi la mswada yaani tafsiri ya maneno muhimu na kutumika kwa sheria.

Sehemu ya pili inahusu uundwaji wa shirika, kazi na majukumu yake na mamlaka ya shirika. Sehemu ya tatu inahusu Bodi ya Wakurugenzi kazi zake, muda wa bodi, muundo wake na madaraka yake. Sehemu ya nne inahusu wafanyakazi wa shirika pamoja na Mkurugenzi Mkuu na majukumu yake na sifa za kuteuliwa kwake.

Sehemu ya tano inahusu masuala ya fedha, inazungumzia uwezo wa kukopa, utaratibu wa ufunguzi wa *account*, utaratibu wa manunuzi, utaratibu wa ukaguzi wa *account* ya shirika na utaratibu mzima wa uendeshaji na matumizi ya fedha za shirika.

Sehemu ya sita inahusu mambo mengineyo ikiwa ni pamoja na taratibu za uhakiki wa kisera, ripoti za mwaka na uwezo wa waziri kuunda sheria ndogo ndogo zinazoweza kuongeza ufanisi wa sheria hii.

Mwisho kabisa ipo jadweli inayohusiana na kipindi cha uteuzi na miongozo ya vikao vya bodi ya Wakurugenzi. Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe kujadili mswada huu na hatimaye kuyakubali mapendekezo yaliyomo katika mswada huu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ahsante sana.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Salum Abdalla Hamad (Kny: Mhe. Asha Bakari Makame, Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari naomba kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu mswada wa sheria ya kuanzisha Shirika la Utangazaji, kazi, madhumuni na utawala wake pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu na mwingi wa rehma kwa kutujaalia uhai, uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii ndani ya Baraza lako tukufu kwa madhumuni ya kujadili mswada wa sheria ya kuanzisha Shirika la Utangazaji Zanzibar, kazi, majukumu na utawala wake pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Pia nikushukuru wewe binafsi Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Katiba ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu mswada huu wa sheria wa kuanzisha Shirika la Utangazaji Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kutoa shukurani za dhati kwa wajumbe wa kamati, viongozi na watendaji wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo pamoja na wanasheria wetu wa Baraza na serikali kwa michango, miongozo na ufafanuzi wao juu ya mambo mbali mbali yaliyojitokeza wakati wa kuujadili mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na mashirikiano na bidii kubwa ya kazi inayooneshwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati, napenda kuwataja kwa majina wajumbe hao ili kutambua na kutathimini juhudi zao hizo muhimu kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Asha Bakari Makame	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Ali Mzee Ali	-	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Mansour Yussuf Himid	-	Mjumbe
4. Mhe. Assa Othman Hamad	-	Mjumbe
5. Mhe. Abdi Mosi Kombo	-	Mjumbe

6. Mhe. Kazija Khamis Kona	-	Mjumbe
7. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Mjumbe
8. Mhe. Salum Abdalla Hamad	-	Mjumbe
9. Ndg. Haji Khatib Haji	-	Katibu
10. Ndg. Asma Ali Kassim	-	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii adhimu kutoa pongezi na shukurani za dhati kwa wadau mbali mbali wakiwemo wadau wa sekta ya habari na utangazaji kwa michango yao mizuri waliyoitoa wakati kamati yetu ilipokutana nao kwa ajili ya kupata maoni yao ili kuufanya mswada huu uwe bora zaidi kwa maslahi ya nchi yetu na watu wake.

Aidha, pongezi na shukurani za dhati ziende kwa uongozi mzima wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kuona umuhimu wa kuleta mswada huu ambao kama utapitishwa unatarajiwa kuleta mabadiliko makubwa kabisa katika shirika muhimu hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyo katika nchi yoyote duniani sekta ya utangazaji ina wajibu mkubwa katika kuhamasisha jamii katika harakati za kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Hivyo ni matumaini ya kamati hii kuwa uwezo wa kisheria, kiutendaji na kiutawala utakaopewa shirika hili baada ya mswada huu kupitishwa utalifanya shirika hili kubadilika katika ngazi zote ili liweze kutekeleza wajibu wake kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Utangazaji Zanzibar ni shirika linalotokana na vyombo viwili vya serikali ambavyo ni Televisheni Zanzibar na Sauti ya Tanzania Zanzibar. Hivyo mabadiliko ya vyombo hivi kwenda katika muundo wa shirika na hasa katika nyanja hii ya utangazaji hayatokosa kuwa na changamoto mbali mbali zikiwemo upatikanaji wa fedha za kutosha kwa ajili ya uendeshaji wa shirika kibiashara na kiushindani, utoaji wa huduma bora za utangazaji zinazokidhi viwango vya kimataifa na mahitaji halisi ya rika mbali mbali hapa nchini pamoja na ukuaji wa kasi ya teknolojia ya kisasa inayotumika katika kazi za utangazaji.

Hivyo basi ni wajibu wa viongozi na watendaji wa shirika hili kuongeza ubunifu na uwajibikaji katika kazi ili kuzishinda changamoto hizo kubwa zinazohitaji juhudi na umakini mkubwa kuweza kukabiliana nazo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kufanikisha ushirikishaji wa jamii katika mswada huu, tarehe 7 mwezi wa kwanza mwaka huu 2013, Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ilipata fursa ya kukutana na wadau mbali mbali wa sekta ya habari na utangazaji ili kupata maoni yao kuhusu mswada huu.

Aidha kamati ilipokea maoni ya maandishi kutoka kwa mdau mmoja. Kwa ujumla Mhe. Mwenyekiti, wadau wote hao walitoa michango mizuri iliyolenga kuifanya sheria hii tunayoiandaa iweze kutekelezeka kwa kufuata misingi ya haki, usawa, ufanisi, uwajibikaji na utawala bora na kukidhi ipasavyo mahitaji halisi ya wananchi wa Zanzibar katika sekta hii muhimu ya utangazaji.

Wadau wenyewe ni Baraza la Habari Tanzania, Chama cha Wanasheria Wanawake Zanzibar, *Zanzibar Health Club*, Waandishi wa Habari za maendeleo Zanzibar, *Confederation of Informal Sector* na *Nationa Chamber of Commerce, Industry and Agriculture.*

Mhe. Mwenyekiti, katika michango ya wadau kwanza lilijitokeza Shirika la Utangazaji kuitwa shirika la umma kwa namna linavyotoa huduma zake. Hivyo kamati inaugana na wadau kuwataka watendaji wa shirika hili kutoa matangazo yanayowahusu zaidi wananchi wakiwemo wa kijijini.

Aidha kwa kufuata silka na utamaduni wa Kizanzibari, matangazo ya shirika hili yazingatie mambo halisi ambayo wananchi wenyewe ndio wanayoyapenda na sio kutangaza au kuonesha mambo wanayopenda watendaji wa shirika au kikundi fulani cha watu walio wachache.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo kutathibitisha kuwa Shirika hili la Utangazaji kweli ni shirika la umma. Aidha taarifa zinazotolewa na shirika hili hazina budi kufanyiwa utafiti wa kina ili wananchi waweze kufahamu ukweli wa mambo ulivyo juu ya matokeo mbali mbali. Kufanya hivyo Mhe. Mwenyekiti, kutawaongezea imani na matumaini wananchi wa Zanzibar kwa shirika lao hili muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, katika maoni ya wadau pia lilijitokeza suala la haja ya kushirikishwa kwa sekta binafsi katika nafasi za wajumbe wa bodi wa Shirika la Utangazaji. Kamati kimsingi imekubaliana na wazo hilo hasa kwa vile sekta binafsi inatoa mchango mkubwa katika kuendeleza na kufanikisha jukumu muhimu la sekta la utangazaji la kutoa habari na kwa kuhamasisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, wadau pia waliona pia ipo haja kwa Baraza lako tukufu, yaani Baraza hili la Wawakilishi kwa kujadili kwa upana zaidi maana ya maneno maslahi ya umma. Kwa muktadha wa sheria hii kifungu nambari 6 (e) ili kujua mipaka yake kwa ajili ya kuepuka kutumiwa kinyume na inavyokusudiwa kwani suala hili ni pana kimaana na kimatumizi.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu namna ya kumpata mkurugenzi mkuu ambaye ndiye mtendaji mkuu wa shirika, kamati ilikubaliana na wadau kwamba pamoja na kuwa Mhe. Rais aendelee kumteuwa mkurugenzi mkuu, lakini ni vyema kwa sasa serikali kuanza kufikiria utaratibu wa kuzitangaza nafasi kama hizo muhimu ambapo Mhe. Rais angepelekea majina yaliyochujwa kati ya majina yaliyoomba ili ateuwe mmoja kwa kadri mwenyewe atakavyoona inafaa. Utaratibu huu unaweza pia kuimarisha dhana ya uwazi, uwajibikaji na utawala bora kulingana na mabadiliko ya ulimwengu yalivyo hivi sasa.
Mhe. Mwenyekiti, pia kamati inaunga mkono maoni ya wadau juu ya umuhimu wa kutilia mkazo upatikanaji wa taarifa ya fedha kwa wakati ambayo inahusu mapato na matumizi ya shirika.

Taarifa hiyo kwa mujibu wa kifungu cha 15 (2) inatakiwa kuandaliwa na mkurugenzi mkuu si chini ya miezi 3 kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha na kuwasilishwa taarifa hiyo kwa waziri baada ya kuidhinishwa na bodi. Haja ya kutoa msisitizo juu ya suala hili linatokana na ukweli kuwa baadhi ya taasisi za serikali huwa zinachelewesha kuandaa taarifa zao za fedha kutokana na mapungufu mbali mbali ya kiutendaji.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu imeupitia kwa kina mswada huu ambapo kimsingi inakubaliana na mapendekezo ya mswada huu, hata hivyo kwa kuzingatia maoni ya wajumbe wenyewe wa kamati pamoja na yale ya wadau, kamati yetu imefanya mabadiliko kimsingi na ya kimaandishi kwa lengo la kuufanya mswada huu uwe bora zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nieleze baadhi ya marekebisho ya msingi ambayo kamati imeyaona yangefaa kufanyika kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza katika ukurasa wa 292 kifungu cha 3 (1) hakikueleza makao makuu ya Shirika la Utangazaji yatakuwa wapi. Hivyo basi kamati imependekeza kuwa makao makuu ya shirika hili yaelezwe wazi wazi kuwa yatakuwa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kukidhi masharti ya kifungu cha 6 (1) (b) cha Sheria ya Mitaji ya Umma kifungu nambari 4 ya 2002, kuhusu idadi ya wajumbe wa bodi na mashirika ya umma inayotakiwa isipungue watano na isizidi saba, na pia kwa kuiwezesha sekta binafsi ishirikishwe katika muundo wa bodi ya shirika hili, kamati imependekeza kifungu cha 8 (c) kifutwe na badala yake kiingizwe kifungu kipya kitakachomuwezesha mjumbe mmoja kutoka sekta hiyo binafsi kuteuliwa katika bodi hiyo hususan kutoka Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wenyeviwanda na Wakulima.

Aidha, kifungu cha 8 (f) kamati imeona ikirekebishwe na kumpa uwezo zaidi Mhe. Waziri kwa kuteuwa wajumbe wa bodi wasiozidi watatu wenye ujuzi, taaluma na uzoefu katika nyanja zilizotajwa kifungu hicho.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia ukuaji wa elimu hapa nchini na mabadiliko ya kitaaluma duniani pamoja na kuleta ufanisi zaidi kwa shirika, kamati katika kifungu cha 11 (2) (a) inapendekeza kuwa mkurugenzi mkuu wa shirika hili awe amehitami angalau shahada ya pili; yaani master degree kutoka Chuo Kikuu kinachotambulika.
Aidha katika kifungu cha 11 (2) (b) kamati inapendekeza kuwa mkurugenzi mkuu awe na kiwango cha uzoefu angalau wa miaka mitano katika moja au zaidi ya taaluma zilizotajwa katika kifungu hicho.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia kuwa Waziri ndiye msimamizi mkuu wa wizara, kamati imeona ni vizuri uwezo wa waziri katika shirika hili ukaekwa wazi wazi zaidi katika mswada huu. Hivyo kamati imependekeza katika ukurasa wa 296 baina ya kifungu cha 12 (2) na 13 (1) kiingizwe kifungu kipya cha 13 (1) (a), (b) na (c) kitakachoweka wazi zaidi mamlaka ya Mhe. Waziri wa kwa shirika hili.

Maelezo kamili ya kifungu hicho kipya yanapatikana katika karatasi ya mapendekezo ya marekebisho ya mswada huu yaliyofanywa na kamati.

Mhe. Mwenyekiti, marekebisho mengine yakiwemo yakimaandishi na uchapaji yameshachukuliwa na wanasheria wetu kama yanayoonekana katika karatasi ya marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inaunga mkono mswada huu asilimia mia juu ya mia na inaomba Waheshimiwa Wajumbe wote waungane na sisi kwa kutoa maoni yao kadri watakavyoona inafaa na hatimaye kuunga mkono na kuupitisha mswada huu muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho naomba kuwasilisha. Ahsante.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya mwanzo ya kuchangia na kutoa mawazo yangu katika mswada huu wa kuanzisha Shirika la Utanganzaji Zanzibar, kazi, majukumu, utawala pamoja na mengine yanayohusiana na hayo.

Kabla ya kutoa mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha mchana huu kusimama katika Baraza lako kuweza kutoa huu mchango wangu.

Pili nikushukuru wewe binafsi, nimshukuru waziri kwa uwasilishaji wake pamoja na watendaji wa wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukurani hizo nianze kwanza kwa suala dogo. Kwa hili shirika lipo zamani kidogo lakini kumbe ilikuwa hakuna sheria yoyote ambayo inaliongoza. Jee, shirika hili lilikuwa linaongozwa vipi na chini ya sheria gani, kwa sababu shirika lipo ilikuwa hakuna sheria yoyote ambayo inaliongoza kwa sababu sheria ndio inaanzishwa sasa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze mchango wangu na kifungu cha 5 (a) kwenye ukurasa wa 292, kutoa taarifa, elimu na burudani kwa jamii, hilo shirika maana yake ni kutoa mambo hayo. Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo la msingi na hili ndio jambo kubwa la wizara hii, kwa sababu ni shirika la serikali, hivyo huu utakuwa ndio mdomo wa serikali. Kwa hivyo kwa kuwa ni mdomo wa serikali ni lazima uweze kutoa hizo taarifa ambazo ni sahihi, elimu ya kuwaelimisha watu na burudani ambayo itakubalika kutokana na mila, silka, tabia, taratibu na tamaduni za Mzanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi shirika letu hili linakuwa nyuma katika kutoa hayo mambo ambayo yamekusudiwa kutolewa yaani taarifa na elimu. Kwa mfano kunapotokezea mambo kadhaa nchini hasa yale ya majanga ni vyombo vya habari vya watu binafsi ndivyo vinaanza kutoa taarifa kwa wananchi kuliko vyombo vyetu vya redio na televisheni.

Kwa hivyo kwa kuwa huu ndio mdomo wa serikali isifumbe mdomo wake wakaacha vyombo binafsi kutangulia kutoa taarifa hizo. Sisi kama serikali lazima taarifa zote muhimu tuwahi kuzitoa kabla ya kutolewa na vyombo vyengine ili tuonekane umahiri wetu, ujuzi wetu na maarifa yetu katika fani hii ya utangazaji.

Lakini mara nyingi hata zilizopozama hizi meli, watu wa vyombo binafsi ndio waliokuwa wakielimisha watu hatua juu ya hatua namna ilivyokwenda, wakati ambapo redio yetu ipo, televisheni yetu ipo inakodolea macho tu, vyombo vya habari vyengine ndio wanaofanya kazi hiyo.

Kwa hivyo naomba kwa kuwa hiki ni chombo cha serikali kitangulie kutoa taaluma za aina hiyo mapema kuliko kuviachia vyombo vya binafsi kutanglia. Kwenye kutoa elimu hizi au taarifa hizi

tujitahidi kutoa taarifa ambazo ni za ukweli na ambazo ni sahihi. Kama ni janga kumekufa watu kumi, tuseme kumi wala tusiseme wawili kwa sababu ya kuonesha tu kuwa hakuna ajali kubwa iliyotokea.

Kama hakuna aliyefariki, lakini kuna mmoja kasema wamekufa tukanushe kuwa hakuna aliyefariki lakini ukanushaji wetu uwe wa kweli wala sio wa kutetea tu. Kwa hivyo ni lazima tutoe taarifa iliyokuwa sahihi kuelimisha jamii matokeo mbali mbali ama mazuri au mabaya, ya msiba au ya furaha lakini yawe sahihi kama yalivyotokea.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutoa elimu kuna mambo kadhaa nchini ambapo tunataka watu wetu au wananchi wetu waelewe. Nchi ina matatizo kadhaa, ina magongwa kadhaa, kwa hivyo kuandaliwa vipindi maalum kama vipo viendelezwe vitakavyowaelimisha watu namna ya kutunza mazingira, kujikinga na magonjwa mbali mbali yale ya kuambukiza na yasiyokuwa ya kuambukiza, kuelimisha watu juu ya matumizi bora ya ardhi, kuelimisha watu juu ya ujenzi bora kwa kuzingatia sheria mipango miji na mengineyo ili nchi yetu hatimaye kupitia vyombo vyetu vya habari, watu wetu waweze kufahamu mambo mbali mbali ambayo wanatakiwa wayafahamu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutoa burudani lazima burudani hizi ziwe zinakwenda sambamba kama nilivyosema mwanzo na tamaduni zetu. Mimi sitoona vyema wala sitopendelea kuona pana kipindi pengine cha burudani ya muziki au onesho lolote ambalo msichana kahifadhi hapa kifuani pake na hapa chini yake lakini mwili mwengine wote upo wazi. Shirika letu vipindi kama hivi ningeomba wao wasivioneshe kwa sababu si lazima tuige kila ambalo wengine wanafanya, tuige linaloigika na tuache ambalo hatuwezi kuliiga.

Kwa hivyo vipindi vyetu kama hivyo vya burudani viwe vinamtia mtazamaji hata kama kakaa, baba, mama na watoto wao. Kisitoke kipindi baba au mama akajitia udhuru wa kuondoka kumbe kipindi ndio kilichomuondoa kutokana na ile hatua inavyokwenda kwenye kipindi kile. Kwa hivyo hapa naomba sana shirika letu lizingatie haya ya utamaduni, silka, taratibu na mila za Mzanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na vyombo vya habari vya serikali; yaani televisheni na redio lakini pia kuna vyombo vya habari kadhaa vya binafsi ambavyo vinachukua taarifa zetu, mambo yetu ya nchi na mengineo, navyo hivi ingawa havipo chini ya wizara lakini itakuwa vimesajiliwa viweze kufanyakazi, navyo pia viwe makini katika kufuatilia mambo na kufanya mambo yao kadhaa.

Hapa Mhe. Mwenyekiti, nina ukurasa wa gazeti fulani la Zanzibar Leo la Jumatano Oktoba, tarehe 24 mwaka 2012 likineonesha mimi Mohammed Haji Khalid, naomba ninukuu hili gazeti lilivyoandika. “Mwakilishi wa Jimbo la Matemwe CCM Mohamed Haji Khalid kushoto akibadilishana mawazo na Mwakilishi wa Jimbo la Wawi CUF Saleh Nassor Juma nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi jana, picha na Abdalla Masangu”.

Kwanza kuna makosa mawili yaliyofanywa. Mimi kwanza sio CCM, madhali sio CCM hivyo kafanya makosa makubwa mwandishi huyu. La pili mimi si mwakilishi wa Matemwe. Hivyo kachukua jimbo la watu kanipa mimi. Sijui kama Mwakilishi wa Jimbo la Matemwe ataweza

kuniachia, akiniachia nipo tayari niwe Mwakilishi wa Matemwe na Mtambile pindipo watu wa Matemwe wakikubali ni Mwakilishi wao. (*Kicheko*).

Kwa hivyo vyombo vya habari vinapokuja hapa visiwe na utashi wao tu watizame habari zilizokuwa sahihi na wasipotoshe. Mhe. Mwenyekiti, hata jana au juzi kuna taarifa ambayo vyombo hivi vilipotosha, Mhe. Jussa alikuwa anatoa msaada fulani pahala, wakasema anatoa msaada kwenye tawi la CCM.

Kwa hivyo ningeomba hivi vyombo viwe makini katika taarifa zao wasisukumesukume tu. Kama hawatujui bora watufuate watuulize kuliko kusukuma tu. Mimi hivi nikifika Mtambile nitaambiwa kuwa kumbe umeshatoka kwenye chama chetu, nishakuwa CCM na mwakilishi wa Matemwe.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti habari kama hizi ambazo ni muhimu kweli, kwa sababu mwanafunzi anamuamini mwalimu zaidi kuliko mtu mwengine yeyote, yaani mwanafunzi mdogo, wakati unapomsomesha mtoto kwamba kitu hichi kiko hivi na halafu nyumbani akaambiwa kinyume na vile anavyofundishwa basi ata-*argue* na wazazi wake, kwamba mama au baba hivyo sivyo kwa sababu mwalimu ameniambia hivi.

Kwa hivyo, na watu wetu wanaviamini vyombo vya habari, kwa maana hiyo chombo cha habari kinapotamka kitu basi wasikilizaji taarifa ile wanaipokea na kuifanya kuwa ni taarifa ya kweli. Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo vyombo vya habari kama mupo *please be careful,* tafadhalini jitahidini sana katika kuchukua na kutoa habari zenu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwenye kifungu hichi cha 5 niende kwenye kipengele cha ‘b’ na naomba nikinukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 5(b) kinaeleza hivi:-

> “Kutoa huduma za utangazaji za redio, televisheni na huduma nyengine zinazohusiana na hayo na vipindi ambavyo vitachangia maendeleo ya jamii kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni pamoja na kutilia mkazo umoja wa kitaifa katika upanuzi wa utamaduni”.

Kifungu hichi nacho ni muhimu sana, shirika hili ambalo tunalizungumza lazima lizingatie haya yote zaidi hili la kujenga umoja wetu wa kitaifa. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema kwa vile unayo televisheni ya serikali ndio mdomo wa serikali. Kwa hivyo, mara nyingi watu au wananchi na hata nje ya nchi wataiamini taarifa yoyote inayotoka kwenye serikali kuliko vyombo vyengine.

Mhe. Mwenyekiti, wanapotoa taaluma zao wahakikishe kuwa hawaleti mfarakano baina ya jamii na jamii au mtu na mtu na lengo ni kujenga uhusiano mwema baina ya mtu na mtu, kwa hivi sasa tumo ndani humu watu wawili CCM na CUF. Kwa hivyo, taaluma wanayotoa iwe inawakaribisha kujenga uhusiano mwema, ili kuendeleza huu umoja wetu wa kitaifa ambao umeanzishwa.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Mwenyekiti kwenye hichi kifungu cha 5(d) kuliendesha shirika katika shughuli za kibiashara. Kwa kweli ni sawa kwa sababu shirika ni lazima liweze kujitegemea, kwa hiyo shughuli zake lazima ziwe za kibiashara. Halikadhalika ni shirika la serikali, kwa hivyo huduma zake pamoja na kuwa liende kibiashara, lakini livutie watu kupeleka matangazo yao pamoja na mambo yao mengine mengi zaidi kuliko taasisi za kibinafsi.

Mhe. Mwenyekiti, nakusudia huduma zao ambazo zile za kuchangia au kutoa fedha basi ziwe na bei nafuu kidogo kuliko za vyombo vyengine, ili watu wakimbilie kwenye shirika hili letu la redio na televisheni katika kupeleka matangazo yao pamoja na mambo yao mengine mbali mbali.

Sasa naomba nizungumzie kidogo kwenye kifungu cha 8(1) (a) na (b) na hapa kuna jambo dogo tu ambalo nataka kulisemea. Mhe. Mwenyekiti, kuna neno ambalo limeandikwa kumuhusu mtu ambae na wala sina hakika Kiswahili cha siku hizi, lakini kwa Kiswahili nilichofahamu mimi zamani mwanadamu huwezi kumuandika ambae lazima umuandike ambaye, kwa hivyo iwe ni mtu ambaye. kwa maana hiyo, kwenye kifungu cha 8(a) na (b) kimetumika ambae na mimi ninapendekeza iwe ambaye badala ya ambae.

Vile vile kifungu cha 8(3) kuhusu Mwenyekiti anatakiwa awe na maarifa na uzoefu wa muda gani, maana yake ametajwa tu kwamba awe na maarifa na uzoefu kwa muda gani na maarifa gani hayo maarifa ambayo awe nayo na kwa nini tutumie neno maarifa badala ya kutumia kiwango maalum cha elimu.

Kwa hivyo, tumkabidhini mtu kazi anayoiweza na wala tusifanye kwamba mtu awe na maarifa kawa mtangazaji siku mbili tatu ndio tukasema tayari anayo maarifa, lazima tuweke kiwango maalum cha elimu na wala isiwe hivi tu kuwa anayo maarifa.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye kifungu cha 9(1) ambacho kiko katika ukurasa wa 295. Kifungu hichi kinazungumzia kuhusu bodi naomba kunukuu kidogo Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 9(1) kinaeleza hivi:-

> “Bodi itateua mtu mwenye taaluma katika fani ya sheria kwa kiwango cha angalau shahada ya kwanza na uzoefu wa kazi usiopungua miaka miwili katika fani hiyo kuwa Katibu wa Bodi”.

Kwa maana hiyo, Katibu wa Bodi atakuwa ni mwanasheria angalau mwenye elimu ya shahada ya kwanza.

Lakini kifungu hichi 9(3) nacho naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 9(3) kinaeleza hivi:-

> “Ikiwa Katibu hatakuwepo kutokana na ugonjwa au sababu nyengine yoyote hawezi kuendeleza majukumu yake, bodi itatoa mfanyakazi yeyote mwengine wa shirika kwa ajili ya kuendeleza majukumu ya katibu hadi hapo katibu atakapopatikana”.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili siliungi mkono kwa Katibu mwenyewe ni msomi tena ni mwanasheria huyo achaguliwe mtu mwengine yeyote yule kwa sababu ni mfanyakazi wa shirika awe katibu hii haiwezekani, siungi mkono Mhe. Mwenyekiti, samahani inawezekana kwa sababu wenyewe tayari mumeshapanga, lakini hii siungi mkono. Kwa kuwa katibu ni msomi tena ni mwanasheria kwa hiyo achaguliwe mtu mwenye sifa kama za katibu kwa ajili ya kukaimu ule ukatibu na sio mtu mwengine yeyote tu.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye kifungu cha 10(1) (d) pia naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 10(1) (d) kinaeleza hivi:-

> "Kuandaa na kusimamia kanuni za wafanyakazi, kanuni za fedha na muundo wa mishahara ya wafanyakazi pamoja na maslahi mengine".

Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba nizungumzie kuhusu mishahara na maslahi mengine ya wafanyakazi. Kwa kweli tunajua kuwa wafanyakazi wa shirika hili ambao ni wa redio na televisheni kwa upande mmoja wanafanya kazi kubwa tena ni muhimu sana kwa taifa. Kwa hivyo, lazima na Waswahili wanasema "*Mcheza kwao hutunzwa*". Kwa maana hiyo, na wao maslahi yao pamoja na mishahara yao basi ni vyema ikawa mizuri kidogo.

Kwa mfano, hapa tulipo sisi nadhani wafanyakazi waliomo ni wa Televisheni Zanzibar na wao wanasimama kwa kipindi chote ambacho sisi tupo hapa pengine na sisi tukae humu kwa kusimama kama wanavyosimama wao basi tungeli-*argue* kwamba hatuwezi kusimama muda wote huo, lakini wao wanasimama na kuchukua taarifa zetu katika hali hiyo.

Kwa hivyo, lazima wawe na maslahi bora tena mazuri ya mishahara pamoja na maslahi mengine, ili hii kazi pamoja na ugumu wake waipende na waithamini kwa ajili ya kuweza kuifanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye kifungu cha 11(2) (b) na naomba kunukuu kidogo.

Kifungu cha 11(2) (b) kinaeleza hivi:-

> "Mwenye uzoefu angalau katika moja au zaidi ya taaluma ya mawasiliano ya bahari, usimamizi wa biashara, habari na mawasiliano, utumishi wa umma".

Sasa hapa alikuwa anazungumzwa Mkurugenzi Mkuu, yaani awe mwenye uzoefu angalau katika moja au zaidi naye pia kama kule mwanzo hajatajwa awe na uzoefu gani au awe na elimu ya aina gani. Kwa hivyo, halikadhalika kama alivyo Katibu naye alikuwa awe angalau na elimu ya shahada ya kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye kifungu cha 13(2) pia hapa naomba ninukuu kwa sababu kidogo ni kikubwa.

Kifungu cha 13(2) kinaeleza hivi:-

> "Hakuna kitendo, kitu au jambo lolote litakalofanywa au kuachwa kufanywa na mfanyakazi wa shirika au mtu mwengine yeyote aliye chini ya maelekezo ya shirika kitakachomfanya ikiwa kitendo, kitu au jambo lolote hilo lililofanywa au kuachwa kwa nia njema katika utekelezaji wa Sheria hii, mfanyakazi au mtu huyo kutiwa hatiani binafsi kwa hatua zozote za kisheria au madai mengine".

Kwa hivyo, hapa inampa mfanyakazi nguvu ya kisheria kufanya vyovyote atakavyo na atakuwa hana kosa, kwa sababu hiyo nia njema tutaijuaje kama kafanya hivi kwa nia njema au mbaya. Kwa hivyo, kifungu hichi ningeomba kifutwe na wala hatuwezi kumuacha mfanyakazi akawa hana hatia kwa jambo lolote atakalofanya. Sasa kama hatachukuliwa hatua au asitiwe hatiani, basi hatiani atiwe nani.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hayo mafupi na machache naomba nimalizie hapo na ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake na kukupongeza wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii leo kuwa mtu wa pili baada ya Mhe. Mohammed Haji Khalid.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu nitaanza hapa kwenye kifungu cha 3 ukurasa wa 92 naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 3(1) ukurasa wa 92 kinachoeleza hivi:-

> "Kunaanzishwa Shirika la Umma la Utangazaji linalojulikana kama Shirika la Utangazaji Zanzibar kwa kifupi litajulikana kama *ZBC*".

Mhe. Mwenyekiti, *ZBC* ni Shirika la Utangazaji la Umma Zanzibar na utangazaji ndio kioo cha nchi. Kwa hivyo, Shirika la Utangazaji mimi naiomba Wizara kwanza iwatangazie wananchi, kwa sababu redio ni elimu kubwa kwa taifa.

Kwa maana hiyo, *ZBC* itoe elimu kwa wananchi tena kwa muda mrefu. Kwa mfano, ikiwa inatangaza kwa muda wa masaa 18, basi iwatangazie wananchi kwa muda wa masaa 24 tena kwa kupitia lugha tofauti, kama vile lugha yetu ya Kiswahili, Kiingereza, Kifaransa na nyengine, ili tuweze kuelewa na sisi kwa kupitia njia zetu za redio. *(Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti, redio yetu itutangazie mambo ya utamaduni wa Zanzibar. Kwa mfano, televisheni yetu ya Zanzibar ituoneshe vipindi vyetu vya utamaduni pamoja na mambo mbali mbali. Kwa kweli tunakosa sana na mara nyingi redio yetu huwa tunaikosa na kupata redio nyengine tofauti kuliko yetu ya Zanzibar hatuipati vizuri.

Kutokana na hali hii, naliomba shirika letu lijirekebishe sana kwa tatizo hili la kuyakosa matangazo yake kwa muda mrefu hatuyapati. Kwa mfano ukitaka kufungua redio ya Zanzibar hatuipati na wala hatujui sababu ni zipi. Kwa hivyo, nadhani Mhe. Waziri atakuja kutueleza kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, ni sababu gani Shirika la Utangazaji la Zanzibar matangazo au vipindi vyake hatuvipati.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti mimi nasisitiza sana tena naliomba sana shirika letu kwamba matangazo au vipindi vyake wakati wote tunapohitaji vipatikane.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mchango mkubwa naomba kumalizia hapa na ninaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutuletea mswada huu ambao ndio roho na kioo cha serikali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitakuwa na mengi isipokuwa naomba nizungumze kidogo, kwamba tunataka kuunda hili shirika. Shirika hili kama nilivyozungumza mwanzo kwamba ni kioo na roho ya serikali.

Kwa hivyo, ninaiomba sana serikali tutakapomaliza mswada huu na kugeuka kuwa sheria, basi tuhakikishe kwanza tunalilea shirika hili kikamilifu, ili kuhakikisha kwamba linakuwa shirika kweli.

Mhe. Mwenyekiti, tujue kwamba hivi sasa tuko kwenye wakati wa *science and technology* na hili tunaliunda shirika. Kweli tukubali kwamba baadhi ya mambo yatatokezea tu kwenye shirika hili.

Lakini kubwa zaidi nitilie mkazo Mhe. Mwenyekiti tena naomba sana tujitume, kwa sababu badala ya kupiga simu wewe unapigiwa simu wewe, kwa hivyo tujitume kutafuta taarifa ambazo zenye uhakika na tuwafikie walengwa. Kwa mfano, kilimo ama shughuli nyengine mbalimbali angalau wenyewe wenye shirika hili, kwa sababu hili litakuwa ni shirika la wananchi wajisikie na wao.

Kwa maana hiyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti tuachane na tabia ya kungoja kufuatwa wewe mwandishi wa habari, mtu wa kamera kwamba watu wakufuate wewe pale tunapotokewa na mambo mbali mbali, pia itokane ukiwa na jambo lako mpaka utoe gari ukawachukue.

Kwa kweli haya ni mambo madogo, lakini ni makubwa mno, kama tunaunda shirika hili Mhe. Mwenyekiti, basi tuhakikishe tunabadilika na tunaliweka shirika letu katika hali ambayo kama wenzetu mashirika mengine. Mhe. Mwenyekiti, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari na wizara hii inaniuma sana, kwa sababu ndio wizara niliyoanzia kazi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, niseme kwamba shirika hili liwe makini. Mhe. Mwenyekiti, kuna mtiririko kwenye mswada huu, basi naomba sana mtiririko huu tuufuate, ili tusije kujitia dosari ambazo si za lazima.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba na siku zote tunazungumza kwenye Baraza lako la Wawakilishi kuwa tuwe na wajuzi ambao wanajua na wala tusichukue tu. Kwa mfano, maana yake siku hizi ukiangalia kila mmoja anasomea uandishi wa habari, kweli ni matakwa

yako wewe mwenyewe unataka, lakini waandishi wengine hawaridhishi na wanajiandikia tu bila ya utafiti na mambo ambayo hayaridhishi katika nchi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana shirika hili na niseme kwamba ni imani yangu kuna vichwa kwenye televisheni na redio ambavyo vikikubali kujituma, basi vinaweza kufanya vizuri. Lakini serikali ijitahidi tena kusomesha ili tuwe na akiba, kwa sababu ninayoyajua mimi kama sikumfunza mwenzangu na leo Mwenyezi Mungu anaweza kuchukua roho yake.

Kutokana na hali hiyo, tusiwe wachoyo wa kufundishana kwamba wewe unajua, lakini unaona ukimfundisha mwenzako atakunyang'anya wadhifa wako. Kwa maana hiyo, tujitahidi kuelimishana pamoja kusaidia katika shirika hili. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, Mhe. Mwenyekiti niseme niwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba wauchangie mswada huu kwa uwezo wao, ili kupata maarifa ya kutosha. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaakhirisha kikao hichi hapa kwenye orodha nina Mhe. Mwakilishi mmoja tu ambaye ameomba kuchangia. Kwa hivyo, naomba tutakapomaliza *session* hii ya asubuhi basi jioni tuje mapema na tujitahidi kuomba kuchangia, ili tuweze kuupitisha mswada huu kama ambavyo tumeelekezwa kwa mujibu wa sheria.

Pili ningependa kutoa matangazo ambayo yameletwa hapa kabla ya kuakhirisha kikao hichi. Tangazo la kwanza linatoka kwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi, ambalo linaelekeza kwamba baada ya kumaliza *session* hii ya asubuhi tunajuilishwa kwamba wale Wajumbe walioalikwa kwenye uzinduzi wa kitabu hapo saa 7 mchana zoezi lile bado linaendelea kama kawaida kwenye ukumbi wetu hapo juu.
Tangazo jengine ambalo limeletwa hapa mbele limeletwa na wasaidizi wa Mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa na Mhe. Ali Salum Haji, ambalo linawakumbusha kwamba kesho baada ya kikao cha mchana tukutane kwa ajili ya kuendelea kuipitia kanuni.

Baada ya maelezo sasa kwa heshima na taadhima naomba kuakhirisha Baraza hili hadi saa 11:00 jioni. Ahsanteni sana.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi nichukue fursa hii kukushukuru kwa jioni ya leo kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa au kuchangia Mswada huu wa Kuanzishwa kwa Kushirika la Umma linajulikana kama Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC).

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze serikali kwa dhati kabisa kwa namna walivyoamua kutuletea Mswada huu wa Kuanzisha Shirika hili la Utangazaji, dhamira ni nzuri, wakati ni muafaka. Lakini niseme pamoja na dhamira nzuri yote ya kuletwa Mswada huu mimi nilikuwa nina michango kama miwili mitatu kuhusiana na Mswada huu.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 5(a) kutoa taarifa, elimu ya burdani kwa jamii. Mimi nilikuwa nahisi kuna haja ya kuongeza neno katika kifungu hichi. Kwa sababu tukiacha kutoa taarifa elimu na burudani sasa hivi imejengeka kwenye studio zetu za televisheni Zanzibar baadhi ya wakati kuna burudani au kuna vipindi ambavyo vinakuwa havitupeleki katika hali iliyokuwa nzuri. Yaani vipindi hivyo vinatutoa nje ya utamaduni wa Mzanzibari. Mimi nafikiri lingetafutwa neno zuri la kuongeza hapa jinsi ya hiyo kutoa elimu na burudani, inayoendana na silka ya Kizanzibari. Kwa sababu tukiacha neno burudani tu linaupana mkubwa sana. Sasa hapa Mhe. Mwenyekiti, lingetafutwa neno la kuongeza ikiwezekana hilo liwe neno silka ya Kizanzibari.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kuna kazi nane zimetajwa hapa za Shirika. Dhamira ni nzuri kazi za shirika zitakuwa kama kuanzisha mfumo endelevu na kukusanya, kuhifadhi na kuchambua na kusambaza habari za umma, kuandaa vipindi vya ndani vyenye ubora na kuchukua vipindi vya kigeni vinavyoendana na mahitaji ya wazawa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme kwamba pamoja na dhamira nzuri ya kuanzisha Shirika letu hili la ZBC pamoja na sheria nzuri ambayo tumeiyandaa mambo yote Mhe. Mwenyekiti, yanahitaji nyanja tatu. Tunahitaji kuwa na sheria lakini tunahitaji kuwa na watendaji au wasimamisi wa hiyo sheria. Lakini cha tatu tunahitaji hivyo vitendea kazi ambavyo vinafanywa vyende vikatendewe na hao ambao wanasimamia hii sheria.

Mhe. Mwenyekiti, ZBC iko taabani, pamoja na sheria nzuri yote, kama kuna mambo hayajafanyiwa kazi ya haraka basi sheria yetu na mambo mazuri yote ambayo tumeyaweka hapa yatakuwa hayasaidii hali yoyote. Kwa mfano mimi kuna sehemu kama mbili tatu nataka nizielezee. Sehemu ya studio ya kurushia matangazo (MCR). Kitengo hichi mashine zake ni mbovu, ile dhamira ya mambo manane ambayo tumeyaelezea hapa kama kituo cha kurushia matangazo hakina mashine zilizokuwa bora zaidi, sijui kama ufanisi utapatikana, *post production* vifaa vyake vichakavu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine kamera walizopewa ndugu zetu wa televishen ni vichache mno. Linaweza likatokezea tukio watendaji wapo wanataka kwenda kufanya kazi lakini wakashindwa kufanya kazi kutokana na ukosefu wa kamera kuwa chache, unaweza kuambiwa kamera hatuna pa kuazima hapaeleweki. Sasa haya ni mambo ambayo unaweza kusema yanaweza yakakosesha ufanisi wa zana nzima ya kuanzisha kwa sheria hii katika suala zima ya kutaka mabadiliko ya kwenda na wakati.

Mhe. Mwenyekiti, kuna jambo ambalo hili ndio zito kabisa kuliko yote, hata Mhe. Rais wetu huwa halimpendezi kabisa nalo ni suala la pale ambapo panapokatika umeme basi wananchi huwa wanakosa matangazo kupitia katika vituo vyetu vya televishen na hata redio. Pamoja na kwamba tuna majenereta katika kila kituo cha kurushia matangazo lakini bado ndugu zetu hawa wanakabiliwa na changamoto za mafuta.

Mambo haya Mhe. Mwenyekiti, kama hayakufanyiwa kazi ipasavyo nasema ile dhana nzima ya kuwa na sheria nzuri ambayo inaendana na wakati na itakidhi na haja ya matakwa ya wananchi basi kama hizi changamoto hazikufanyiwa kazi bado tatizo litabakia kuwa lipo pale pale, tunabadilisha sheria lakini utendaji haupo katika hali nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, katika Kifungu cha 18(a) katika masharti mengineyo kinasema katika kutekeleza majukumu yake kama ilivyoelekezwa chini ya sheria hii bodi itakuwa na sera ya uhariri ya kuhakikisha kila mwananchi ana haki ya kupata taarifa wakati wowote.

Mhe. Mwenyekiti, nasema dhamira ya sheria ni nzuri lakini bado kuna matatizo ambayo vituo vyetu vimekabiliwa na changamoto nyingi. Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mengi yaliyokuwa yanasikitisha tena yanasikitisha sana. Suala hili la kupata habari wakati wowote pale ambapo linatokezea tatizo katika nchi yetu ili wananchi wetu waweze kufaidika na hali hiyo. Hili bado linatusikitisha kuna wakati hata Rais wetu anakuwa anafanya ziara katika maeneo mbali mbali yaliyokuwa yana mahafali, lakini kitendo kinafanyika leo cha kusikitisha hapa hapa Zanzibar taarifa za Mhe. Rais zinatoka kesho. Kwa kweli hili jambo bado sisi wengine linatupa matatizo.

Niwaombe ndugu zangu baada ya kupitisha Mswada huu na baada ya kutengeneza mambo haya basi yale mambo madogo madogo ambayo tunahisi hayana ufanisi tunaweza kuyafanyia kazi. Chengine ambacho bado ni tatizo kwetu na katika eneo hili la masharti mengineyo ambalo limeelezewa katika kifungu cha 18(a) ambacho nimekisoma. Hebu tujiulize Mhe. Mwenyekiti, inakuwaje au kuna tatizo gani, tatizo linatokezea Zanzibar lakini taarifa zake unaanza kuzipata kupitia TBC. Hichi kitendo kwa kweli bado wananchi wa Zanzibar kinawasikitisha sana.

Nafikiri kuna haja ya kujipanga vizuri baada ya kutengeneza sheria zetu basi yale mambo ambayo nimejaribu kuyaelezea kwa haraka haraka, changamoto ambazo zinatukabili za vituo vya kurushia matangazo, uchache wa kamera, uhaba wa mafuta katika maeneo ya majenereta pindipo umeme unapokatika ni vitu ambavyo vinaweza vikaendana na wakati vikasaidia Mswada huu pale ambapo tutakuwa tayari tumeupitisha na kuwa Sheria na kuweza kufanya kazi zake katika ufanisi wa hali ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona na mimi nizungumze hayo machache na kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kwahani naunga mkono Mswada huu asilimia mia moja. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu katika Mswada wetu huu wa Kuanzisha kwa Shirika la Utangazaji Zanzibar Pamoja na Kazi zake, Majukumu na Utawala wake Pamoja Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kwa mara yengine tena tukaweza kufika hapa siku ya leo kwa ajili ya kuendeleza yale majukumu ambayo yanatukabili kuendelea nayo katika taasisi yetu hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kwisha kutoa shukurani zangu nije moja kwa moja katika kuushukuru uongozi wa Wizara kwa kukaa na kuweza kufikia maamuzi ya kutengeneza sheria hii ambayo leo hii tumeletewa hapa na ikawa sisi ni wajibu wetu kuweza kuangalia na kuweza kuzidisha chochote ambacho tutahisi kwamba kinafaa ili sheria hii iweze kuwa nzuri zaidi na iweze kutumika kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na timu ya wataalamu na watendaji wote wa shirika husika na wizara husika katika utaratibu mzima wa suala hili. Vile vile ningechukua fursa hii kuanza moja kwa moja na Shirika letu za ZBC, naanzia hapo kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika letu la ZBC kama walivyotangulia wenzangu kuanza kuchangia, kusema kweli linajikongoja, japokuwa mwanzo mgumu, mwanzo ilikuwa ni idara lakini sasa tunaelekea kwenye shirika. Lakini sote tunafahamu kwamba Zanzibar ni watu wa mwanzo katika Afrika hii kuanzisha hichi kitengo cha television, tukawa tunasuwa suwa, hatimae tukaweza kufikia pahala tukatoa maamuzi ya kwamba sasa tuanzishe na tulitangaze sasa liwe kama Shirika ili pengine linaweza likasaidia linaweza kuendelea vizuri kama ambavyo mashirika mengine yanakuwa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kinachotusikitisha mpaka sasa pamoja na kwamba si zamani sana tokea kuanza kwa shirika hili bado shirika hili linasuwa suwa sana. Linasuwa suwa katika masuala ya uongozi lakini vile vile katika masuala ya vitendea kazi vile vile. Ni jambo la kusikitisha sana kuona mpaka leo hii tumefikia hapa shirika hili linakamera zisizozidi tatu kuweza kufanya shughuli zote zinazoweza kuendeshwa katika nchi hii, hili ni jambo la aibu sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuondoka katika idara kuja katika shirika tulitegemea kwamba baadhi ya mambo kama haya madogo madogo yangeliweza kurekebishika, lakini mpaka leo hii wakati tunazungumza bado tuna tatizo ambalo linapelekea taarifa muhimu katika nchi yetu zinashindwa kupatikana kutokana na ufinyu wa vitendea kazi, sasa hili ni tatizo. Ningeliwaomba sana Waziri pamoja na watendaji na waanzilishi wa Mswada huu na sheria hii hili waliangalie. Na kwa sababu tunaelekea katika shirika mambo kama haya tuachane nayo. Kwa sababu si mambo ambayo yanaweza kutusaidia.

Mimi kama Mzanzibari na Mtanzania sifarijiki kila mara kuangalia vipindi vya nje ndani ya TV yetu, nafarijika sana kuangalia vipindi ambavyo vinatayarishwa ndani ya nchi yetu. Iwe Zanzibar au iwe Tanzania kwa ujumla na hata iwe Afrika. Lakini kila unapokwenda kutokana na vile vitendea kazi vyetu ni vichache mara nyingi imekuwa tuna vipindi vya nje ya kujirudi mara kwa mara vile kwa vile. Hili linatokana na *program* zenyewe pamoja na ufinyu wa vile vitendea kazi na ndio inasababisha kuwa na mtandao mzuri wa kuweza kufanya vitu vya kuwasababisha wananchi wa Zanzibar waendelee kuipenda TV yao ya ZBC.

Muelekeo wetu wa kupitisha sheria hii ya Utangazaji Zanzibar ningeliomba uongozi uliokuwepo madarakani ujitahidi na uhakikishe kwamba Zanzibar tunabadilika katika nyanja za utangazaji. Mimi Mhe. Mwenyekiti, nasikitika sana kila siku nikikaa nikimuangalia ndugu yetu Marini jinsi alivyoondoka hapa Unguja na Zanzibar visiwa vya Zanzibar na kwenda TV ya Taifa kwenda kuifanyia kazi katika mazingira ya kutatanisha.

Mhe. Mwenyekiti, ndugu yetu Marini ni hazina kwa Wanzanzibari, sasa hivi hazina ile si mbaya kwamba anatumia nafasi yake ya Utanzania katika kutumikia kule lakini kama tungekuwa naye hapa Zanzibar tungelinufaika zaidi. Lakini sasa hivi mtu kama yule ambaye alikuwa na uwezo wake mkubwa tu katika mambo ya habari tumemkosa na sasa hivi amekwenda kutumika katika upande wa pili wa Muungano japo kuwa kwa manufaa ya Watanzania wote kwa ujumla lakini sisi ambae tumepunguza yule tumehasirikiwa kwa ukweli.

Hili ni jambo ambalo linasikitisha sana. Sasa basi kwa kutumia fursa hii ningependa tusije tukasubiri Marini mwengine akaondoka akaelekea kwenye vyombo vyengine vya habari kwa sababu tu ya utaratibu wetu ambao haupo sahihi katika nyanja zetu za habari hapa Zanzibar. Ili tuweze kufikia mustakbali huo ni vizuri tuzingatie sana uwezo wa watendaji wetu na wafanyakazi wetu ambao tayari wana elimu, baadhi yao na wana ujuzi lakini wanashindwa kupewa dhamana ambazo zinalingana na uwezo wao wa kiutendaji ndani ya taasisi husika. Hili ni tatizo Mhe. Mwenyekiti.

Ningeliomba sana viongozi wetu tulionao katika taasisi hizi wasimuogope mtu kutokana na sera zake au kutokana na uwezo wake wa kuweza kufahamu mambo na kujua mambo, bali wamtumie mtu kutokana na uwezo wake na ufahamu wake ili kuweza kuleta ufanisi na maendeleo katika taasisi zetu. Ningeliomba sana uongozi wa Shirika la Utangazaji hili liondokane na mawazo potofu ya kuona kwamba sitaki kumsogeza fulani kwa sababu ana elimu anaweza kuja kuchukua kiti changu. Uwezo wako kwa wakati wako umepita, sasa ni wakati wa mwenzako, huna budi kukubaliana na ukweli kumuacha mtu ambaye ana uwezo wake aweze kufanya lile ambalo linastahiki kufanywa kwa wakati tulionao.

Nikija katika eneo la redio nalo vile mambo yako hivyo hivyo bado tuna matatizo, hebu tufanye wakati tumeondoka katika idara na tumeelekea katika Shirika tufanye watu wetu wa Zanzibar na nje ya Zanzibar waweze kupenda kusikiliza redio na kutizama TV katika Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba na Tanzania kwa ujumla. Uwezo huo tunao tukiamua tunaweza, tunaondokana na ubinafsi, tunaondokana na makundi, kuondokane na mambo ambayo hayana maana ili tuweze kuwatumia wataalamu wetu waweze kusaidia nyanja hizi ili tuweze kufanikiwa na redio yetu irejeshe ile hadhi kama vile tulivyokuwa tumeanzisha katika miaka ya 70.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimepatwa na masikitiko vile vile kuona kwamba ina maana kuna msemo ule wa kiiarabu unaosema *“alhimaru laa yamshi illa bil asaa”* ilikuwa kilasiku hapa tunakaa muelekeo wa TV zetu na redio zetu ilikuwa ni mashaka matupu na mitihani lakini tokea siku Mhe. Rais amesema kwamba badilikeni utaratibu huu sitaki kuuona tena sasa imekuwa vizuri.

Taarifa za habari unazisikia kwa wakati, mambo yanakwenda vizuri na kila kitu kinakwenda sawa sawa. Ina maana kwamba hatuna matatizo katika masuala ya kuweza kutekeleza majukumu ya kiutendaji kama serikali kutimiza wajibu wake kwenye Shirika. Isipokuwa matatizo yapo kwenye shirika lenyewe. Ni kipindi kifupi sana tokea Mhe. Rais ametoa kauli ile na utekelezaji wake bado unaendelea kutekeleza kwa ufanisi mkubwa tofauti na suala la ng’ombe lakini katika hili.

Ningelipenda kuchukua fursa hii kusema kwamba tusisubiri mpaka tuambiwe na Mhe. Rais tufanye mambo yetu kwamba ni wajibu wetu ili tuweze kutimiza yale malengo ambayo yametusababisha tuweze kufika pale. Nikiondoka hapo nakuja kwa wafanyakazi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kulifanya shirika hili liweze kufanya kazi zake vizuri kuna kilio cha wafanyakazi. Wafanyakazi hawa tumeondoka nao katika utaratibu wa Idara sasa tumekwenda kwenye Mamlaka, lakini bado wana matatizo yao na wana malalamiko yao na wana usumbufu wao ambao unawakabili. Ningeliomba uongozi wa Shirika hili wakati upo katika madaraka kwa sasa hebu ufanye taratibu za kukaa na hawa wafanyakazi, ili waweze kutatua matatizo yaliyokuwepo ili wawe tayari kuweza kutoa uwezo wao na ujuzi wao walionao kwa ajili ya manufaa ya Wazanzibari na Watanzania na Wafrika na dunia kwa ujumla.

Ningeliomba hilo lifanyike ili matatizo yaliyokuwepo ya wafanyakazi wa hapa na pale yaweze kwisha na waweze kufanywa kwamba wapende kazi zao na wafanyekazi kutokana na taaluma walizokuwa nazo.

Jengine ni kuhusu vitendea kazi, ningeliomba vitendea kazi navyo vipatikane katika taasisi ya ZBC na radio kwa ujumla. Jengine ambalo wafanyakazi huwa wanalalamika nalo ni suala zima la uwajiri katika taasisi hizi, wako watu wambao wanao uwezo, wako watu ambao wana ujuzi, wako watu ambao wanaweza kufanya mambo yakawa mazuri kweli kweli kupindukia kama hivi ambavyo tunawa *excess* lakini wanashindwa kuonesha uwezo wao kutokana na ubinafsi ambao umetutawala katika mamlaka haya.

Ningeliomba sana hili Shirika bado ni zuri, kuna watendaji ambao wana uwezo mkubwa ningeliomba watumike kwa manufaa ya Zanzibar na Watanzania wote kwa ujumla, bado uwezo tunao hata tukisema kwamba hawa hawa tunawatimizia masharti yao na matakwa yao wanayoyataka, basi mambo yatakuwa mazuri tu na tutajisahau hapa Zanzibar, tutaona kama tuko ulaya. Ile CNN pia utakuwa huna habari nayo, utaona bora utumie hii hii Zanzibar tu. Lakini ni jambo la kusikitisha kuona kwamba hata vipindi ndani ya TV zetu na redio yetu si vya kuridhisha, vipindi vingi vya kigeni. Sisi kama Wazanzibari hatupendi ile, tunapenda tuone mambo yetu, tuone tamaduni zetu, tuone muelekeo wetu, tuone taarifa zetu pia.

Mhe. Mwenyekiti, nchi za nje kule ukenda kama mfano Marekani zile taarifa ambazo sisi tunauwezo wa kuzitizama hapa za CNN ukiwepo ndani ya Marekani huzioni zile, unaoneshwa taarifa ambazo zimo katika majimbo yao tu. Lakini ili uweze kuzipata taarifa zile ina maana uwende katika *channel* maalum au utoke nje ya Marekani ndipo unaweza kupata taarifa kama hizi. Kwa nini na sisi tusifikie hapo, watu wetu wana shida ya kujua maendeleo yetu katika nchi yetu, Raisi, kafanya nini, Makamo wake kafanya nini, wananchi wamefanya nini, chama kimefanya nini, ndio watu wanataka kuyajua hayo, Wawakilishi wamefanya nini. Lakini tunapotoka ikawa kunawapa taarifa za nje tu za ndani watazijuaje, watajuaje umuhimu wa serikali zao pamoja na viongozi wao. Tunaomba sana Shirika lisione tabu kama ambavyo sasa hivi linapewa taarifa baadhi ya nyakati tunaambiwa hata unapopeleka taarifa kwamba zioneshwe, kuna viongozi wanasema kwamba taarifa zile haziwezi kuoneshwa ziwe ni taarifa za wakuu wawili tu wa nchi. Si utaratibu mzuri.

Viongozi wanaokwenda wawe Chama Tawala, wawe Chama cha Upinzani, wawe viongozi wa nyanja mbali mbali wanayo haki ya kuoneshewa taarifa zao kwa mujibu wa taratibu ziliopo. Kwa sababu wale ni watumishi wa wananchi, kama hukuonesha taarifa zake na mambo yake anayoyafanya wananchi watajuaje kama huyu anafanya jukumu fulani. Tungeliomba sana tusichague taarifa za kuzionesha tukaendeleza vipindi vya nje tukasahau mambo yetu ya ndani, yanaumuhimu ya ndani kuliko ya nje zaidi.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, hapa hapa nilikuwa nataka kusemea katika suala la taarifa ya habari kwa sasa hivi pamoja na matatizo yaliyokuwepo Wazanzibari wanapenda sana kuangalia taarifa ya habari, iwe za redio kusikiliza au ziwe za TV kuangalia. Kinachosikitisha ni kuona saa 2:15 taarifa ya habari inakuja kamili, lakini saa 4:15 taarifa ya habari inakuwa pungufu. Huu utaratibu wa wapi. Pale saa 4:15 ina maana mtu kakosa taarifa 2:15 saa 4:15 aweze kupata taarifa kwa ukamilifu. Hebu tuangalie wale wenzetu wa ITV pale Tanzania Bara. Taarifa ya habari ya saa 5:00 inakuwa ile ndio kubwa zaidi mambo yote ya kubwa nzima yanaoneshwa pale.

Leo sisi baada ya kutoa taarifa kwa urefu wakati ule wa saa 4:15 ndio tunazifinya zile taarifa tunaleta michezo haina maana yoyote. Sisi hatuna shida kuangalia TV kwa kuangalia michezo, tunachokitaka tunataka kujua taarifa kwa katika nchi yetu kuna nini, kumetokea nini na tufanye nini. Hilo ndio jambo la msingi tunalolitaka sisi. Lakini kuja kuangalia tuangalie mipira sijui mauwa, sijui china wanafanya nini, yamehusu nini haya. Pamoja na urafiki mzuri tulionao na wenzetu, lakini tunapokuwa na mambo yetu tunataka tuyaone vizuri zaidi kwa upana kwa uwelewano na kwa nafasi mambo yetu zaidi kuliko mambo mengine ya nje.

Baaa ya maelekezo hayo Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima kwa niaba ya wananchi walionileta humu wa jimbo la Kikwajuni naukubali Mswada huu na nawaomba Wawakilishi wenzangu tuupitishe Mswada huu ili tuweze kuufikia malengo ya serikali yaliyokusudiwa katika kuhakikisha kwamba tunaendesha mashirika haya kwa taratibu za kisheria na tuweze kuwaona na wao wafanyakazi wakiongozwa na Waziri wao ndani ya wizara hii husika wakibadilika wakifanya mambo kama ambavyo wenzetu nchi za nje wanafanya.

Baada ya maelekezo hayo Mhe. Mwenyekiti, Ahsante sana.

Mhe. Marina Joel Thomas: Asante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nina michango miwili ya kuweza kuchangia kwenye huu Mswada Kifungu cha 8(1)(1) amba kimerekebishwa kinasema kwamba Kifungu cha 8 Waziri atateuwa wajumbe wasiozidi watatu wenye ujuzi, taaluma na uzoefu katika nyanja ya utangazaji, teknolojia, utawala, Sheria ya Vyombo vya Habari, taaluma na biashara, fedha na uwandishi wa habari.
Hapa nilikuwa nina ushauri au pendekezo katika kifungu hichi, namuomba Mhe. Waziri katika kifungu hichi katika hao wajumbe watatu ambao atawateuwa nilikuwa namshauri angalau mmoja au wawili watoke katika asasi za kihabari mfano JAZ, WAHAMAZA, TAMWA huo ndio ulikuwa ushauri wangu.

Chengine ni Kifungu cha 8(3) ambacho kinasema:

Kifungu cha 8(3) “Mtu hataweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti isipokuwa awe na maarifa na uzoefu katika nyanja ya utangazaji, teknolojia ya habari, utawala wa sheria, vyombo vya habari, usimamizi wa biasahra,

mawasiliano ya umma na nyanja nyengine zinazohusiana na hayo."

Mhe. Mwenyekiti, sifa ya mwenyekiti wa Bodi kuwa na maarifa na uzoefu kwa kweli hazitoshi, lazima sifa ya elimu iwekwe wazi hasa elimu ya habari angalau ngazi ya diploma kwenda mbele. Mhe. Mwenyekiti, huu ni ulimwengu wa njia ya kisasa, sasa tupo katika mfumo wa *digital* ni vyema taasisi zetu kama hizi ziwe na viongozi wenye upeo wa kisasa, kitaaluma katika kuendesha taasisi.

Baada ya mchango huo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono Mswada huu.

Mhe. Abdallah Juma Abdallah: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru sana kunipatia nafasi hii ya kusema maneno mawili matatizo katika kuufanya Mswada huu uwe bora zaidi.
Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze kwenye kifungu cha 16 kimo sehemu ya Tano ya Mswada huu ambayo ni masharti ya fedha. Kifungu cha 16(2) kinaweka masharti ya ukaguzi naomba nikinukuu kidogo kinasema:

Kifungu cha 16 (2) "Ukaguzi wa taarifa za fedha na vitabu vya hesabu za fedha za shirika utafanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au Mkaguzi mwengine aliyeidhinishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali."

Sasa kifungu kinachofuata cha tatu kinasema shirika si zaidi ya miezi 6 baada ya kumalizika mwaka wa fedha, litawasilisha taarifa za ukaguzi wa hesabu na taarifa ya kazi zake za mwaka kwa Bodi kwa mazingatio na Bodi itawasilisha kwa Waziri. Sasa kuna jambo moja muhimu sana hapa Mhe. Mwenyekiti limesahauliwa, kwamba hesabu za shirika kwa mujibu wa sheria ya fedha zilitakiwa zipelekwe kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali si zaidi ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha.

Sasa hilo sharti hapa halikuwekwa na kwa sababu halikuwekwa basi shirika kama hawatakuwa waangalifu wanaweza wakachelewesha hesabu na taarifa nyengine za fedha kuzipeleka kwa mkaguzi na matokeo yake wakachelewesha ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Sasa nilikuwa naomba baada ya kifungu cha pili kiongezwe kifungu cha tatu kama hivi nitakavyokitaja, na hichi cha tatu hatimaye kiwe cha nne. Kiongezwe kifungu cha tatu ambacho kitasomeka hivi:

Shirika si zaidi ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha, litawasilisha taarifa za fedha na vitabu vya hesabu za fedha kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Sasa hichi kiwe cha tatu ambacho kitalilazimisha shirika kupeleka hesabu zake kwa Mkaguzi kwa wakati. Na kifungu cha tatu hiki kiwe cha nne. Nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri afanye marekebisho haya ili masharti ya fedha katika sheria hii yawe yamekamilika.

Mhe. Mwenyekiti nikimaliza pendekezo hilo, naomba sasa nizungumzie sehemu ya sita ambayo pale pana masharti mengineyo. Na hapa kuna sera za uhariri kifungu cha 18. Sasa kifungu cha 18 kifungu kidogo (b) kinasomeka hivi:

Kuhakikisha taarifa na burudani zinachangia kulinda maadili ya jamii kwa kuzuia matumizi yote ya habari na vipindi yanayotumia lugha chafu, picha za ngono na mambo mengine yanayokera ambayo hayana nia ya kuelimisha.

Mhe. Mwenyekiti mimi ninashukuru sana kifungu hiki kuwekwa na nakifurahia kweli kweli kwa sababu Mhe. Mwenyekiti huku tunakotoka kwa kweli na niliwahi kusema siku nyingi sana kwamba vipindi vyetu vyengine vinatufanya sisi wengine tushindwe kuangalia TV na familia zetu pale ukumbini, kutokana na vipindi ambavyo vinatolewa mule wanajaribu kutoa vipindi ambavyo vitakuwa hivi vipindi alivyovizungumzia Mhe. Mahmoud, pengine ni michezo lakini michezo yenyewe haina maadili. Badala ya kuelimisha jamii inapotosha jamii kuna picha ambazo huwezi kuzitizama ukiwa wewe na watu wako wa karibu pale ukumbini. Sasa nilikuwa naomba sana kifungu hiki kifanyiwe kazi kwa dhati sio kibakie kwenye makaratasi tu. Hatupendi hata kidogo sisi wengine kuona jamii inapotoshwa kwa kutumia chombo chetu wenyewe cha utangazaji.

Nikimaliza hilo au nikiendelea nikiacha kifungu hicho (b) sasa niende kifungu (f) ukurasa wa 298. Katika nia yake njema ya kujaribu kujenga maadili ya jamii yetu kifunguu (f) kinasema hivi:

Kuheshimu na kuhamasisha umoja wa kitaifa wa wazanzibari na kujenga misingi imara kwa maslahi ya umoja huo, bila kuathiri umoja huo. Mhe. Mwenyekiti kifungu hiki nacho ni muhimu. Unajua chombo cha utangazaji iwe TV, radio, gazeti au hata mabango ya barabarani ni mambo muhimu sana katika jamii yetu kwa sababu ni mambo ambayo yakitumika vizuri yanaweza yakaelimisha sana, lakini yakitumika vibaya yanaweza yakavuruga sana. Kwa hivyo hichi kifungu ni muhimu sana na mimi nataka niseme Mhe. Mwenyekiti tena kwa masikitiko sana tulipokuwa tunakaribia kwenye sherehe za Mapinduzi mwaka huu, kulikuwa na nyimbo ikiimbwa ndani ya radio na ikisema hivi nitakavyosema. Aliyekuwa hataki Mapinduzi arudishe king'ora, sasa mimi nikawa ninajiuliza waliona ving'ora katika nchi hii ni watu watatu tu.

Kwanza ni Rais wetu Mhe. Dr. Shein nikajiuliza hivyo Dr Shein hataki mapinduzi, nikapata jawabu si kweli. Halafu nikajiuliza mwengine ni Makamu wake wa Kwanza Maalim Seif, nikasema aa tuseme Maalim Seif hataki mapinduzi nikaona si kweli. Na wa tatu ni Mheshimiwa Balozi na yeye pia nikawa naamini ni mwana mapinduzi kweli kweli. Sasa ni hao watatu Mhe. Mwenyekiti waliokuwa na king'ora. Sasa kutia nyimbo hii asiyetaka mapinduzi arudishe king'ora maana yake nini. Pengine nikajiuliza labda wanamkusudia Maalim Seif hawa, lakini Maalim Seif mapinduzi anayataka. Mimi nadhani *concern* ya Maalim Seif ni mapinduzi hasa kwa sababu hata baada ya mapinduzi kwa sababu *concept* ya mapinduzi ilikuja Mhe. Mwenyekiti kwa kuondoa dhulma na kuwapatia watu haki zao na mamlaka yao. Hilo ndilo lililokuwa wazo kubwa la mapinduzi. Na hilo naona Maalim Seif ni mdau sana katika suala hilo. Nina hakika Mhe. Balozi mdau sana katika suala hilo na Dr. Shein ndio kabisa. Sasa ukitia nyimbo ile maana yake unakusudia nini?

Na jambo la kusikitisha zaidi mimi nilidhani labda kama kuna watu ni hamasa zao tu wale wanaotayarisha vipindi ni hamasa zao pengine hawaoni mbali sana inaweza pengine ikatokea kitu kama hicho, au hawajui athari ya maelezo kama hayo kuyatoa kwa jamii. Nilifikiri sana

Mkurugenzi angechukua hatua ya kuzuia lile kwa sababu halijengi linabomoa. Mhe. Mwenyekiti tumo katika serikali ya Umoja wa Kitaifa Mhe. Mwenyekiti tumeacha yale malumbano yote ya kisiasa. Sasa ukisema uchukue vionjo vya namna hii ukivitia hapa sasa hivi tukuulize madhumuni yako nini, ndio unajenga umoja wa kitaifa au unakusudia kubomoa umoja wa kitaifa. Na jana unakusudia kubomoa Umoja wa Kitaifa hivi wewe kweli ni mtu unayetufaa katika jamii hii? Nilikuwa nadhani Mhe. Mwenyekiti mambo haya yasiruhusiwe kufanyika huu sio wakati tena wa kufanya mambo ya namna hii, hebu twendeni mbele tusirudi nyuma.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, niligusie kidogo tu muda wa utumishi wa vikao vya Bodi hii ni jadueli liliomo katika huu mswada. Ukisoma kifungu nambari 2 ambacho kinazungumzia kutohudhuria kikao hii ni kwa wajumbe wa Bodi, kimesema hiki kifungu iwapo mjumbe yoyote atashindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya kuwa na sababu za msingi, Bodi itatoa taarifa kwa waziri na waziri atafuta uteuzi wake na atateua mtu mwengine ambaye atakaa ofisini kwa muda uliobakia.

Sasa pana tatizo dogo tu hapo, kwamba Waziri siye anayeteua wajumbe wote wa Bodi, kuna wajumbe wa Bodi anateua waziri, lakini kuna wajumbe wa bodi wanaingia kwenye bodi kwa nafasi zao ndivyo ilivyotueleza hii sheria. Na pengine uteuzi wao hautokani na waziri. Sasa kifungu hiki kinampa waziri kumuondoa kila mjumbe wa Bodi aliyekuwa hakuhudhuria vikao vitatu mfululizo bila ya taarifa inayokubalika. Lakini hawa ni kwa wale ambao waziri alikuwa na uwezo wa kuwateua. Lakini iwapo kosa kama hili litafanyika kwa mjumbe ambaye waziri hakuwa na uwezo wa kumteua hii sheria haikusema atachukuliwa hatua gani na nani atakayemchukulia hatua. Nilikuwa naomba hili Waziri alizingatie na ikiwezekana basi kiwekwe kifungu kitakachotoa adhabu ya namna hii kwa wale wajumbe ambao hawako mikononi mwa waziri.

Mhe. Mwenyekiti nikiondoka hapo nizungumzie jambo moja ambalo ninashukuru sana Mhe. Mahmoud alikuwa analizungumzia sana na alipokuwa anazungumza nilikuwa ninampigia makofi sana kumuunga mkono.

Mhe. Mwenyekiti tunapojaribu kutunga sheria madhumuni yetu ni kuleta ufanisi zaidi kwamba sheria zilizopo zilikuwa na mapungufu fulani Fulani, kwa hivyo tunajaribu ama kurekebisha au kutunga sheria mpya kwa ajili ya kupata ufanisi katika ile taasisi ambayo tunaitungia sheria.

Sasa miongoni mwa mambo yanayoleta ufanisi, ukiacha hii sheria lakini ni ile nguvu kazi ya watu walipo pale kwenye taasisi yenyewe wanatakiwa wawe makini, wawe na taaluma za kutosha, wawe wanaipenda kazi yao, wanafanya kazi kwa bidii lakini pia wawe wanatendewa vyema maslahi yao yazingatiwe. *Treatment* zao ziwe za kuwapa moyo sio za kuwavunja moyo. Sasa Mhe. Mwenyekiti, jana Mhe. Ali Mzee hapa alisema sana kuhusu *management* ya Shirika la Meli, na akasema ile sheria itakuwa haina maana ikiwa ile *management* haitafanyiwa marekebisho nayo alisema sana.

Sasa na mimi nasema katika Shirika hili la Utangazaji sheria hii Mhe. Rais akishaitia saini, itakuwa sheria nzuri sana lakini ufanisi wa sheria ni mdau namba moja. Na mdau namba mbili wa ufanisi huu itakuwa ni *management* yenyewe. Kwa masikitiko Mhe. Mwenyekiti *management* ya Shirika la Utangazaji ZBC ina matatizo, na kwa kweli wafanyakazi wa ZBC

wamekuwa wakitulalamikia mara nyingi kwamba hawatendewi vizuri. Mara nyingi walikuwa wakimsakama Mkurugenzi wao kwamba hawatendei vizuri watumishi wake pale na hasa suala la malipo, kuna wengine wanafika kutwambia hata kama malipo yameidhinishwa lakini yanatolewa visivyo yaani, kama imeidhinishwa mtu apewe *allowance* ya shilingi elfu kumi anapewa elfu tano nyengine zinakokwenda hazijulikani. Hapa wapo wafanyakazi wa shirika wanafanya kazi siku nyengine inaweza ikafika mwaka hawajapewa *allowance* zao hawa. Ukiuliza kwa nini tatizo ni Mkurugenzi wao.

Sasa mimi nilikuwa ninashauri sana *management* inayohusika tukishaitengeneza hii sheria vizuri basi kuna haja ya *management* nayo kuitengeneza vizuri ili *management* pamoja na sheria wakishirikiana tunaweza tukapata ufanisi mzuri. Lakini kutengeneza sheria halafu tukabakia na *management* iliyokuwa hai-*encourage* watumishi wake, hii sheria haitofanya kazi na inaweza ikabakia kwenye makabati tu. Aligusia hapa Mhe. Mahmoud yule mtangazaji ambaye kwa kweli alikuwa hodari kweli kweli Marin, Marin aliondoka kwa sababu za namna hiyo, kenda zake TBC na kweli ni *star* kule TBC ni mbunifu sana, hodari wa kazi ile TBC imepanda chati sana kuwepo Marin pale. Sasa hofu yangu tusipowatendea vyema watumishi wa ZBC na tabaan wengine ni watu na taaluma zao Mhe. Mwenyekiti watatoka wataingia kwenye viboti wavuke wende zao kwa wenzetu kule waende wakafanye kazi, jambo ambalo ni hasara kubwa kwa sababu tumewasomesha kwa pesa nyingi tena pesa za walipa kodi wanyonge. Ikiwa manufaa hatutoyapata sisi itakuwa ni hasara kubwa. Kwa hivyo nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri ajitahidi sana kurekebisha *management* ili wafanyakazi wapate moyo wa kutufanyia kazi.

Baada ya kwisha sema maneno hayo Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi naunga mkono sana sheria hii, na nawaomba wenzangu pia wajitahidi kuichangia na hatimae kuiunga mkono ili tupate ufanisi katika masuala mazima ya utangazaji. Ahsante.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia kidogo mswada huu wa Shirika la Utangazaji. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu pamoja na kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote kuandaa mswada huu ambao ni mzuri lakini Mhe. Mwenyekiti, nikianza mwanzo tunaelekea katika kupitisha mswada huu kuanzisha Shirika hili la Utangazaji.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi katika mchango wangu niseme kwamba Shirika hili la Utangazaji lianze vizuri liandae katika kuboresha vitendea kazi, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, tukianzia na Shirika letu la Utangazaji ZBC Televisheni. Mhe. Mwenyekiti televisheni yetu kama alivyoeleza Mhe. Mahmoud kwamba wananchi wa Zanzibar wote huwa wanapenda sana kuangalia televisheni na kujua matukio mbali mbali yanayotokea nchini pamoja na ya kimataifa, lakini bado ZBC yetu haijajipanga vizuri katika kuwapa matokeo ambayo yanafanywa na viongozi mbalimbali akiwemo Rais, wasaidizi wake, Mawaziri, Wawakilishi. Kwa hivyo iko haja kujipanga vizuri kwa kujiandaa na kuboresha vitendea kazi.

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti ZBC pale katika masuala ya vitendea kazi utakuta pale kuna jambo la kusikitisha sana kuona ZBC nzima ina kompyuta moja. Halkadhalika waandishi wa habari wa ZBC wana kamera moja, kukitokea tukio Amani au jengine limetokea Darajani basi kamera ile basi inafanya kazi kwa upande mmoja tu. Lakini likitokea jengine basi inakuwa ni tabu na mashaka makubwa kuweza kupata taarifa kwa sababu ya kukosekana kamera, au kama

kamera imepatikana basi itakuwa ya mwandishi mwenyewe binafsi. Lakini ZBC yenyewe kamera ni moja.

Mhe.Mwenyekiti mbali ya tatizo la kamera ZBC kuna tatizo pia la usafiri, nimekusudia usafiri wa gari kunapokuwa na matukio mbalimbali, kuna wapeleka taarifa pale basi kubwa utaambiwa usafiri hatuna. Juzi kulitokea tukio la moto katika Jimbo la Rahaleo, Shehia ya Muembeladu maeneo ya pale Mitiulaya. Kwa bahati nzuri mimi nilifika katika tukio lile tukawasiliana na waandishi wa habari wa ZBC lakini majibu kwamba kamera haipo imeenda katika msafara wa Rais, gari hatuna, sasa Mheshimiwa tunaanzisha shirika hili ni zuri lakini tujipange na kujiandaa kwa vitendea kazi muhimu kwa waandishi wetu.

Mbali haya hayatoshi Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa ZBC inakwenda masaa 24, lakini wafanyakazi wetu wa ZBC wanafanya kazi masaa 24 lakini posho hawana, vitendea kazi hawana mashaka matupu. Kwa hivyo ningeliliomba shirika hili linalokuja lijiandae vizuri ili kuweza kuboresha na kuendana na wakati kwa sabaabu Mhe. Mahmoud alizungumzia TBC, Mhe. Mwenyekiti mimi ni mtazamaji mkubwa wa TBC asubuhi, kwa sababu wanajipanga vizuri, wanaleta habari ambazo ni nzuri za wakati huo huo. Nnasikitika kuona kwamba ninaangalia TBC kuliko kuangalia ZBC. Wana kipindi chao sasa hivi ZBC wanaita *Amka na ZBC* ni kipindi kizuri ninawapongeza sana waanzishaji wa kipindi kile, lakini Mhe. Mwenyekiti, kipindi kile na ukiangalia na kile cha wenzao cha TBC utakuta tuko mbali sana kutokana na ufinyu wa utendaji kazi. Kwa hivyo ningewaomba sana wizara pamoja na hili shirika ambao wameteuliwa katika kusimamia shirika hili kuhakikisha kwamba vinapatikana vifaa vya kutendea kazi katika kuendesha ZBC yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika eneo la redio, hali ya redio yetu sasa hivi ni tofauti na ile ya miaka 10, 15 iliyopita au 20 ninakumbuka wakati nikiwa mdogo miaka 10, 15 kulikuwa na vipindi vizuri mbali mbali ambavyo vilikuwa vinaendeshwa na redio yetu ya Zanzibar. Lakini leo kipindi kilichobakia ni kipindi cha mawio. Mhe. Mwenyekiti mimi ujue ni mwanamichezo na ni mpenzi sana kusikiliza vipindi vile vya michezo. Lakini leo kipindi cha michezo cha ZBC redio hakuna mzanzibari au mpenda maendeleo yoyote anasikiliza kipindi kile, kwa sababu waandishi hawana nyenzo unapopigiwa simu na mwandishi wa habari yoyote ikiwa wa michezo au wa mawio basi anakwambia Mheshimiwa hebu nipigie nataka unipe taarifa hii na hii. Badala ya yeye akupigie ili apate taarifa wewe ndio umpigie.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, huwa ninapigiwa simu na redio mbali mbali mpaka za Mwanza. Juzi tulipokuwa tunaendesha mashindano ya Mapinduzi ilikuwa simu zinatoka Mwanza, zinatoka Dar es Salaam, zinatoka Arusha wanakupigia simu kupata taarifa za mashindano yale yanayoendelea. Lakini mwandishi wa ZBC redio anapokupigia Mheshimiwa nipigie unipe taarifa. Sasa tuwaandae kuwawezesha waandishi wetu wa habari ili waweze kupata habari, mimi nitampigia lakini mwengine atakuwa hana kwa hivyo zile taarifa watakuwa hawapati. Kwa hivyo wajiandae vizuri kuhakikisha kwamba wanawafanyia, wanawapatia vitendea kazi waandishi wetu wa habari.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika mswada huu katika kifungu kile cha 8(f) ambacho katika mswada huu mama kuna kifungu ambacho kinaeleza hapa, wajumbe wengine wasiozidi wawili kutoka kwa watu maarufu Zanzibar ambao watateuliwa na Waziri wenye ujuzi, taaluma na uzoefu katika nyanja za utangazaji, teknolojia, utawala, sheria na vyombo vya habari,biashara,

fedha na uandishi wa habari. Lakini katika marekebisho hapa nimeona kwamba katika kifungu hicho cha 8(f) kinarekebishwa kama kinavyosema:

‘Waziri atateua wajumbe wasiozidi watatu wenye ujuzi, taaluma, uzoefu wa nyanja za utangazaji teknolojia, utawala wa sheria wa vyombo vya habari, taaluma biashara, fedha na uandishi wa habari.’

Sasa hapa kwamba tunampa Waziri ateue wajumbe watatu, huku kuna wajumbe wasiozidi wawili. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja anipe sababu au uhalali wa kumpa wajumbe watatu badala ya wawili. Kwa hivyo hili Mheshimiwa wakati waziri atakapokuja atueleze umuhimu na sababu za msingi ambazo zilizofanya badala ya kupewa wawili apewe watatu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nifikie hapo kwa sababu mengi yameshazungumzwa na mama yangu Bi. Asha yeye ana mengi na anasubiri kwa hamu katika kuchangia mswada, kumbe ameshachangia anasema. Kwa sababu yeye ndie Mwenyekiti wa Kamati hii ya Habari, Utalii na Kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Rahaleo niunge mkono mswada huu kwa asilimia mia moja, nawatakia kila la kheri shirika hili ili twende na wakati na teknolojia. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kunipa nafasi hii nikazungumza machache kuhusu mswada huu mzuri kabisa wa kuanzishwa kwa Shirika hili la Habari pamoja na majukumu yake, utawala wake pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kwa kuanzia nataka nimpongeze sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuona umuhimu wa zilizokuwa idara zetu za habari na televisheni kwa kuona umuhimu wa kuanzisha shirika na tamko lake. Mhe. Mwenyekiti, vyombo hivi tunavyo muda mrefu na tumeona katika utekelezaji wa majukumu yake kwa kweli vimekuwa vikisuasua. Kwa kuwa vilikuwa vikisuasua inaonesha kulikuwa kuna baadhi ya mapungufu na mapungufu hayo dawa yake ilikuwa ni kuanzishwa shirika. Kwa hivyo, ndio manaa nadhani Mhe. Rais akaona pamoja nakwamba lilikuwa halijaanzishwa shirika kwa kutungiwa sheria, lakini atumie nguvu yake ya ziada aliyopewa na wananchi kwa kutamka rasmi kwamba au kwa kibali chake mwenyewe kuanzisha hili shirika.

Sasa namshukuru sana Mhe. Waziri, Katibu Mkuu pamoja na wasaidizi wao wote kwa kuitikia wito wa Mhe. Rais, kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kututungia sheria na leo hapa tunakuja kuijadili.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze kwenye hiki kifungu cha 3 ambapo kwenye *heading* sehemu ya pili kinasema kwa kuanzishwa kwa shirika na majukumu yake. Mhe. Mwenyekiti, naomba ninukuu kifungu hiki,

Kifungu cha 3(1) kinasema kwamba:

> "Kuanzishwa Shirika la Umma litakalojulikana kama Shirika la Utangazaji Zanzibar kwa kifupi (ZBC)".

Lakini vile vile Kifungu cha 3(2) kinasema kwamba:

> "Shirika litakuwa ni mrithi wa vyombo vya habari vya serikali vinavyojulikana kama Televisheni ya Zanzibar na Sauti ya Tanzania Zanzibar".

Kwa hivyo, ina maana sheria hii au shirika hili litakuwa ni mrithi wa hivi vyombo viwili, tunapongeza sana. Sasa kifungu cha 3(3) naomba niendelee kinasema kwamba,

> "Kwa kuzingatia sheria ya mitaji ya umma shirika litakuwa ni chombo kinachojitegemea na cha kudumu chenye muhuri wake wenyewe kwa kutumia jina lake kwa kuwa na uwezo wa kushtaki na kushtakiwa kumili mali inayohamishika na isiyohamishika, kuingia mikataba na taasisi mbali mbali, kukopa kiasi chochote cha fedha kinachohitajika kwa ajili ya shirika".

Sasa hapa kidogo ndio kwenye maneno yangu katika hivi vifungu vitatu. Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakuja kuwa mgumu sana wa kupitisha mswada huu, pamoja na pongezi zote nilizozitoa hapo mwanzo na nina sababu zangu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa shirika hili tunalolianzisha linarithi yaani Redio pamoja na Televisheni na shirika linaweza kukopa, linaweza kushtaki na kushtakiwa. Sasa shirika hili linaanzishwa na deni la wafanyakazi, katika bajeti wakati wa mwezi wa Juni tulipokuwa tukichangia Bajeti Kuu ya Serikali nilizunguzma hili. Mhe. Naibu Waziri kaingia huku katoka huku, kaja waziri kaingia huku katoka huku hakunijibu. Sasa leo namkamata wafanyakazi wa shirika wanajitahidi kwa huo uwezo wao na nyezo ndogo tunazowapa wanajitahidi sana, lakini leo inapofika pahala wanafanya kazi wanapata viji-*trip*, *exposure* tena *exposure* zenyewe mtu anaweza akapiga miaka sita, saba au kumi kapata mara moja, lakini kile kinachomfanya aende kule aweze kuishi asiadhirike hatuwapi na wengine tunapowapa hatuwapi chote kuna nini.

Mhe. Mwenyekiti, kuna waandishi walikwenda Uholanzi huko wakenda wakajifunza wamekuja huku wanatumia taaluma yao vizuri mpaka lana ya leo hawajalipwa pesa zao. Mimi kama kweli shirika kama sheria inavyosema litarithi basi na hili naomba walirithi na kulirithi kwenyewe wawalipe. Kwa sababu mtu anapokwenda safari sawa sawa na sisi tunapokuja Barazani, unakuwa una mambo mbali mbali unapiga mahesabu unasema ngoja nikirudi, sasa na wao pengine walipokwenda hiyo safari walikuwa washajua mimi posho yangu itakuwa kiasi gani anapiga mahesabu, wengine wanakwenda kukopa hasa kabla hawajenda safari leo karudi hakulipwa mpaka leo. Sasa kama sheria inavyosema mnarithi basi naomba hayo muyarithi na Mhe. Waziri ukija ili uniridhishe, unikune basi nataka uje uniambie na hayo umeyarithi na utaweza kuyatimizia.

Vile vile ukiacha Uholanzi wengine wamekwenda safari juzi tu ya China hakuna *formular* nzuri ya kulipwa, wengine wamelipwa zote, wengine wamelipwa wanavyotaka wao hawajui kama watamaliziwa au vipi na kwa kuwa wenzao wa miaka mingi iliyopita hawajamaliziwa na hawa wa juzi hawategemei kama watalipwa. Sasa je, utegemee ufanisi gani kwa wafanyakazi hao.

Mimi nadhani Mheshimiwa kuwaboresha, kuwapembejea wafanyakazi wetu wa vyombo vya habari ndio watakapokuwa na wao na bidii ya kufanya kazi kama alivyosema Mheshimwa mwenzangu hapa Mhe. Nassor Salim Ali. Kweli waandishi wengi wanapokupigia simu anataka taarifa anaku-*beep,* akiona hujamjibu anakutumia *message* mheshimiwa mimi mtangazaji naomba taarifa moja, mbili, tatu sasa ndio wanatwambia Waheshimiwa bajeti mliotupitishia ndogo kwa hivyo muikamilishe nyinyi. Sasa kweli ukiangalia bajeti tunayoipitisha kwa Wizara ya Habari kwa Televisheni na Redio kwa kweli ni ndogo na ndio maana unakuta kila siku tunalalamika hawana *camera*, hawana kompyuta, *camera* na kompyuta sio mchicha kama ukiutilia maji utaota hizi uwe na fedha, ukishakuwa na fedha utakuwa na kompyuta, *camera* na kila kitu.

Sasa mimi nadhani kwa kuwa tunaanzisha shirika tuipe nguvu na nguvu yenyewe sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ndio hii nguvu ya sheria tunayoitunga hapa. Sasa nakuja kwa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, shirika hili tulitumie kama shirika tusilitumie kama idara ya serikali, tukilitumia kama shirika hili shirika litaweza kujiendesha, tutalipa ruzuku lakini litaanza kujiendesha baadae wanaweza kuingizwa katika pahala wakajitegemea. Leo shughuli nyingi za taasisi za serikali wanachukuliwa hawa bure, sasa kama shirika lishaambiwa linaweza kukopa na kudaiwa, sasa kama unataka kuboresha huduma zao wakati sheria tumeshapitisha wanaweza kukopa watakwenda. Sasa hivi kuna makampuni mbali mbali ukiwaambia nataka kamera 20 anakuletea zote baada ya mwezi mmoja, tunatoa *tender*, tunataka kompyuta, sijui tunataka *scanner*, tunataka *photocopy* na vyenginevyo wewe baada ya mwezi mmoja pale *Karume House* patajaa kila kitu, kwa sababu nini sheria tumepitisha unaweza kukopa. Sasa je, vile vitu vyote kwa sababu katika kuboresha. Mkurugenzi tukishampa mamlaka atataka kuboresha taasisi yake. Mhe. Haroun Ali Suleiman ukisema kuboresha huwa tumbo linamuuma lakini ndio utustahamilie.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa tunapowatumia waandishi wa habari tutaweza kuwalipa kwa sababu wake waandishi wa habari wanakuja kutoa taarifa ya kwetu. Mfano kama mimi nikimwita jimboni kwangu basi kutokana na hali yangu anajua aah Mheshimiwa mfuko wenyewe wa jimbo haumtoshi basi japo pesa ya mafuta na kadi ya simu, lakini katika taasisi za serikali tunapitisha hapa vifungu mbali mbali kwenye bajeti. Kwa hivyo, tutumie vifungu hivi tunavyopitisha kwenye bajeti na hao muweze kuwalipa na hili narejea tena leo kwa bahati mbaya hajakaa Spika lakini Mwenyekiti nakuletea wewe. Hata sisi safari hii tunapokwenda kupanga bajeti ya Baraza la Wawakilishi lazima tuingize fungu la vyombo vya habari, haiwezekani hawa wakaja hapa kazi yao ni kutuonesha sisi tu huko, lakini kumbe wakiondoka hapa hamna kitu, vyombo vinachakaa hivi vitu vya *electronic* hivi vinafika pahala kama sasa hivi kila wakati teknolojia inabadilika.

Leo ukiangalia katika chombo Mhe. Mwenyekiti, kinachotumia sana *media* ni Baraza la Wawakilishi. Kwenye wakati wa bajeti ule mwezi mzima na siku kumi hawaondoki hapa. Je, Baraza linatoa kiasi gani kuvilipa vyombo vya habari. Sasa mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, mimi na wewe ni Wajumbe wa Kamati ya Uongozi tunaopitisha bajeti ya serikali na bajeti ya Baraza la Wawakilishi safari hii ni lazima. Kwa hivyo, Katibu wa Baraza kupitia Mhe. Spika, muanze kufanya mazungumzo na Mkurugenzi wa TBC na ZBC ni kiasi gani wataweza

kutuhudumia vyenginevyo wakisema hawa hawatuoneshi, hatusikilizwi haya wananchi watajua tumesema nini, tumetunga sheria gani.

Kwa hivyo, mimi nadhani ndio maana nikasema kwa kuwa hili shirika tumeshalipa meno sasa hivi tena yale mambo ya bure yamalize, kwa sababu kila taasisi tunaipitishia bajeti yake, sasa safari hii wizara kuna kifungu kwa kuwa tumeweza kuweka vifungu vya vitafunio mpaka tukavipunguza basi tusione tabu kuweka vifungu vya matangazo. Sasa hili ndio jambo ambalo litakaloweza kufanya hizi lawama tunazozitoa hapa aa halina kamera, halina gari haya yatawezsa kupungua na wao wenyewe wataweza kujifanyia mambo yao mengine mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie na uhuru wa vyombo vya habari. Mhe. Mwenyekiti, chombo chetu hichi hii sheria tunayoipitisha hapa watakuwa na uhuru wa kufanya kazi zao, lakini unajua chombo kinachomilikiwa na serikali basi ule uhuru wake unakuwa sio mpana wa kutosha kama vyombo vyengine vya habari. Lakini pamoja na hivyo, waandishi wetu msione tabu kutoa yale mambo ambayo si mazuri na hayapendezi kwa jamii.

Kwa mfano, kuna safari moja kuna mtangazaji mmoja wa televisheni alikwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja kuna mende wanatambaa utafikiria panya akawaonesha kwenye televisheni baada ya wiki hatukumuona tena, sasa kama Hospitali ya Mnazi Mmoja kuna mende tena akaoneshe kitu gani, ina maana akionesha pale sio kuikashifu Hospitali ya Mnazi Mmoja anaonesha kwamba hospitali haipuliziwi dawa. Pamoja na kwamba aliondoshwa lakini mende mbona hawakuonekana tena.

Wenzetu Uingereza kule sasa hivi wameanza kuvipa jina wanaita muhimili wa nne wa dola vyombo vya habari. Katika taasisi ambazo zinaibua mambo mengi hata Wabunge wenzetu wakule Uingereza basi kuna baadhi ya mambo wanayapata kupitia vyombo vya habari, inakuwa ni *source* ya taarifa zao na wanakuja wanazifanyia kazi serikalini na unapatikana ukweli na ndio maana utakuta watendaji wanakuwa na heshima kubwa sana katika taasisi zetu mbali mbali. Kwa sababu anajua nikifanya utumbo fulani vyombo vya habari vinanianika kwa hivyo mtu anaanza kuwa aste aste. Sasa kuna jambo moja nataka hebu lifanyieni kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka watangazaji na wapiga picha wa ZBC hebu wajitahidi ndani ya mwezi huu wawe kila wakati wanapita barabara ile ya Uwanja wa Ndege mpaka kule Mtoni (garagara) watupigie picha za ng'ombe tu, mbuzi na kondoo walioko barabarani, kila siku. Sasa hii ndio itaonesha kwamba alaa! Kumbe hata kauli ya Rais katika nchi hii haina nguvu, leo Rais keshafika pahala anasema sitaki niwaone ng'ombe.

Jana mimi na mwenzangu tulipita sehemu tukawakuta kondoo tukawahesabu 23, sasa labda ng'ombe tu hawatakiwi kuonekana lakini kondoo wanatakiwa waonekane barabarani. Sasa mimi nadhani mtusaidie hasa katika haya maagizo ya viongozi, mnapohisi kwamba watendaji hawayashughulikii basi chukuweni kamera yaonesheni kila siku nadhani wataweza kufahamu.

Sasa mimi nashukuru Mhe. Rais wetu siku aliokuja kuzungumza na nyinyi kule alisema anaangalia sana taarifa za habari na akakutoeni makosa kweli kweli na pale mlipofanya vizuri akakupongezeni. Sasa mkimuonesha ng'ombe kila siku na kondoo basi mimi nafikiri kuna mambo yataweza kutokezea. Mimi nadhani ndio pale tunaposema vyombo vya habari vinasaidia

sana yaani ndio muhimili wanne, lakini vile vile kunapotokezea baadhi ya mambo hasa ya ubadhirifu wa mali za umma kama rushwa na mambo mengine msione tabu kuyazunguzma haya. Kwa sababu haya kama hayakuzungumzwa yakiwa kifichoficho hivi yataendelea kuwepo, lakini mkiwa mnayazungumza kwa kweli yataweza kujitokeza na wale ambao wanafanya vitendo vile watapunguza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nizungumze na kitu chengine katika kifungu cha 5 malengo ya shirika. Kifungu hiki kinasema kutoa taarifa, elimu na burudani kwa jamii. Mhe. Mwenyekiti, na mimi naungana na Mhe. Abdalla Juma, kuna hivi vipindi vya muziki Mhe. Mwenyekiti, unajua unapokuwa mtu mzima halafu watoto wako wanapoanza kulingana na wewe kidogo inakuwa na matatizo yake. Mhe. Mwenyekiti, kuna hizi ngoma nyengine za *Bongo Flavor* na hii miziki mingine ya nje hebu ianzeni kuanzia saa nne ya usiku na kuendelea wale watoto wameshalala.
Kwa sababu unajua kuna kipindi kinakuweko kwenye saa moja hivi au moja na nusu, kuanzia saa kumi na mbili na nusu yaani wakati mwengine unatupa jicho moja huku na jicho moja unamtizama mwanao kama pana mkweo au unaweza ukakimbia. Kwa sababu chombo hiki ndio kama nilivyosema, vyombo vya habari ni huru lakini hiki chombo cha umma uhuru wake una mipaka tena una mipaka mikubwa. Sasa mimi nadhani wajitahidi sana, tunajua wanaboresha ili rika zote ziweze kutizama, lakini mimi nadhani katika ule muda wa mapema tutilieni hizo hizo taarab na vitu vingine lakini sio zile taarabu za mambo yako huku aa, zile kidogo pia kwa wakati huo inakuwa sio nzuri sana. Kwa hivyo, nilikuwa najaribu kuzungumza maadili katika vyombo vyetu vya habari basi viweze kutusaidia saidia.

Mhe. Mwenyekiti, zamani kulikuwa na utaratibu mzuri, zamani ilikuwa vipindi vya watoto vikishamaliza tunaambwia uhuru ni wetu, uhuru ni wetu, hii sauti kidogo siku hizi imeshakauka kauka lakini ingekuwa kama ya zamani Mhe. Mwenyekiti, ningeiimba yote mpaka mwisho, lakini nakusudia ukishafika ule wakati wa watoto kwenda kulala basi kuna wimbo pale tena zamani mnafukuzwa haya haya kalaleni mnaondoka mkitaka msitake, lakini siku hizi ngoma mtindo mmoja kuanzia mwanzo hadi mwisho na sasa hivi tena kuna masaa 24 kwa hivyo mtoto aamue yeye mwenyewe. Kwa hivyo mimi nadhani ile ilikuwa inaonesha kwamba sasa hivi uhuru wenu umeishia hapa uhuru uliobakia tena wa wenda usiku yaani watu wazima.

Lakini jengine mhe. Mwenyekiti, nakuja katika majengo. Mhe. Mwenyekiti, sijui tulikuwa tunaendeshwa kama idara au nini, lakini kwa kweli majengo yetu hasa jengo la Rahaleo *Studio* haliridhishi hata kidogo. Wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China wamekuja pale wakatusaidia wakatujengea jengo tena la *design* yake hasa kama koa kule juu limeviringana viringana vile, lakini jengo lile halina huduma zile za *maintenance*, halipakwi rangi kwa wakati, leo inafika pahala mpaka linaota mwani, mheshimiwa ukienda humo katika *studio* vumbi tupu sijui hivyo vyombo vya *digital* mtaviweka wapi. Kwa sababu *digital* ni vitu ambavyo vya *electronic* na havitaki vumbi, leo uikienda katika *studio* zetu mule siku unayobahatika utawaonea huruma labda ndo kwa kuwa tunaendesha kama idara hakuna fedha, leo vitasa vibovu yaani lile jengo kwa kweli unaweza ukasema humu mnakaa watu humu.

Sasa hebu tuliboresheni na kwa kuwa sasa hivi tunaunda shirika Mkurugenzi hapa pamoja na bodi tunaipa mamlaka ya kuweza kutafuta nyenzo wao wenyewe pahala popote ili waweze kuboresha lile jengo liweze kuvutia.

Mhe. Mwenyekiti, *studio* zetu za Rahaleo kuna mtaalamu mmoja alitoka Uingereza katika hawa watu wa sanaa aliranda katika nchi zote za Afrika, anasema katika nchi zote za Afrika alikuta *studio* mbili tu zenye ubora wa kimataifa, Ghana na Zanzibar tena Rahaleo. *Studio* ya kurikodia mziki anasema *studio* ile iliyojengwa na Wachina kama unaurikodi mziki anasema unapata sauti safi naya kimataifa kabisa. Lakini *studio* ile tumeshindwa kuitumia kwa muda mrefu pengine tumeshindwa kuitunza mpaka Mhe. Rais akatangaza kwamba ataanzisha *studio* katika ile kuwapa moyo wasanii akasema ataanzisha *studio*. Mimi nilimwambia Mhe. Waziri wakati wa bajeti mbona tuna studio nzuri ambapo hawa wataalamu wa masuala ya media wamesema kwamba katika nchi alizotembea Muingereza yule kasema Zanzibar na Ghana ndio peke yake wenye studio ambayo iko *standard* ya kimataifa.

Kwa hivyo, labda ndio ile tunayosema kwamba tuna majengo lakini wataalamu hatuna, manaake studio ile wangekuja wanamuziki mpaka kutoka Kenya wakaja wakarikodi hapa Zanzibar, lakini tumeshindwa kuitunza, tumeshindwa kuiboresha, pengine tumeshindwa kutia vifaa vya kisasa matokeo yake ndio imekuwa ipo tu.

Mhe. Mwenyekiti, hapa ndio inakuja na ule utaalamu, tunaweza tukawa na majengo mazuri, tunaweza tukawa na shirika na nini lakini kama wataalamu tutakuwa hatuna wa kutosha kwa kweli bado mambo yetu yatakuwa hayatokwenda vizuri.

Lakini jengine lakini hili linahusika moja kwa moja na wizara. Mhe. Mwenyekiti, leo katika kuingia ulimwengu wa *digital* Zanzibar tumekuwa tiro, tiro mnaijua? Hata Mhe. Rais anaijua hiyo mana aliwaambia hataki tuwe tiro, lakini ndio tushakuwa tiro, mana wenzetu wameshaingia katika ulimwengu wa *digital* sisi bado tuko katika analog na kama ingelikuwa hatukupewa muda ule wa ziada sasa hivi kungekuwa hakuna televiseni Zanzibar tungekuwa tupo tupo tu, tunabakia bakia sijui TBC, *Channel Ten* ndio hayo. Sasa jamani hiki chombo cha serikali tukashindwe na vyombo binafsi.

Mimi nadhani tena kuna Mhe. Waziri simuoni hapa lakini naibu waziri naona yupo. Mhe. Waziri alikuwa anamsifu siku ile siku ya uzinduzi, akamwambia Mhe. Rais tunakushukuru pesa tulikuwa hatuna lakini umetoa shilingi bilioni nane kama sikosei zile ili tuweze kuwa na fedha za kuingia. Sasa ile Idara ya Mipango na Sera na ina Mkurugenzi ilikuweko wapi tulipokuwa tunaandaa bajeti hapa na hawakujua kwamba ikishafika mwaka 2013 analogi yote inafungwa tunaingia katika *digital*, akaleta hoja hapa waziri akasema naomba shilingi bilioni nane za ziada leo mpaka mnamuachia Mhe. Rais anakwenda kutikisa mfuko anatia mkono kwenye hazina. Mimi nafikiri hizi Idara za Mipango na Sera na Utafiti hizi tumeziweka makusudi na Mhe. Rais kazianzisha kwa makusudi ili waweze ku-*forecast* mambo yanayokuja. Lakini leo kama Mhe. Rais angeligoma akasema bwana mimi hizi katafuteni pahala popote hata hiyo Febuari nafikiri tuliahidiwa kwamba tutaweza kupatiwa angalau hivyo ving'amuzi tuingie na sisi katika *digital* basi sijui ingekuwaje.

Sasa mimi naomba sana watendaji wetu na kama kwa kuwa sasa hivi kutakuwa kuna hili shirika litakuwa na bodi yake wataweza ku-*forecast* mambo yajayo ili chombo chetu kiweze kwenda na wakati.

Mhe. Mwenyekiti, suala la maslahi ya wafanyakazi, kwa kuwa tunaondoka katika idara tunakwenda katika shirika lazima tuiangalie upya *scheme of service* ya watendaji. Kwa sababu unapolifanya shirika inabidi kazi zinakuwa kubwa zaidi, uboreshaji unakuwa mkubwa zaidi kwa hivyo lazima tuangalie na maslahi. Leo Mhe. Mwenyekiti, hakuna posho rasmi linalojulikana kwa kulipwa hawa watendaji wetu. Kuna matukio mengine ya kitaifa wanakwenda kuanzia asubuhi anaanza kufunga mitambo mpaka sisi tunaondoka yaani wao wanafika mwanzo na wanaondoka mwisho ili habari ziweze kufika kwa wakati, lakini posho haina uhakika. Leo anaweza kulipwa shilingi elfu tano, elfu kumi, keshokutwa halipwi kabisa, yaani kwa kifupi wanaishi katika maisha ya kubahatisha, sasa hatuwezi tukawa na waandishi wanaishi katika maisha ya kubahatisha.

Kwa hivyo, mimi nadhani kuwekwa mpango wa kazi utakaojulikana mfanyakazi anafanya kazi kwa masaa mangapi, tunajua kazi za kawaida mtu anafanya kwa muda wa masaa manane, lakini anapofanya kazi za *overtime* ni nini kitaendelea. Haya lazima yawemo katika mpango vyenginevyo watu tutakuja kuendelea kuwalaumu bure. Kwa sababu leo mtu anapiga kazi pale kuanzia asubuhi mpaka saa 12 jioni, leo mtangazaji anatangaza pale anakwenda miyao aibu mtangazaji kwenda miyao, lakini hukumtibu pale angalau akaingia pahala akapata chipsi akala na wenzake. Sisi tunakotoka huko saa tatu ndo tunaingia tunaondoka saa kumi yeye kaingia pale saa 12. Mhe. Mwenyekiti, anakwita pale Mheshimiwa aaa anakwenda miyao aibu. Sasa hii itatokezea kwamba hakuna *incentive*, sasa lazima kuwe kuna muongozo mtu anafanya kazi kwa muda wa masaa fulani yakizidi apate chochote ili tusijekuwaona waandishi wetu wanakwenda miyao.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kuna kifungu cha 7 cha sheria hii kinasema “Kuzingatia sheria zinazotumika shirika linaweza kufanya kazi zake zote zitakazopelekea kurahisisha au zinazotokea au kupeleka wafanyakazi wake kufanya kazi zake vizuri katika kutekeleza majukumu yake bila ya kuathiri masharti ya jumla ya shirika litakuwa na uwezo ufuatao, kumiliki, kukodi, kununua, kumiliki mali za kuuza na vyenginevyo na kuuza mali ambayo lazima ithibitishwe na bodi”.
Mhe. Mwenyekiti, halafu kuna kifungu cha (b) kuanzisha na kuendesha, mimi hapa kitu nilichokusudia kukisema kwamba hivi sasa mamlaka ya haki miliki. Mamlaka hii ya haki miliki inasajili kazi za sanaa, yaani ubunifu wa aina mbali mbali.

Kwa hivyo katika kazi hizo za sanaa vimo hivi vikundi vya nyimbo mbali mbali, taarab, bongo fleva, zenj fleva na vitu vyengine. Sasa mimi nadhani sijui utaratibu wa hizi nyimbo hivi sasa, kama zile kanda munanunua au munagaiwa tu au munatumia utaratibu gani kwa sababu linapokuwa shirika sasa na wewe inabidi unakusanya fedha, kwa hivyo na wewe lazima ujiandae vile vile katika kununua kazi za watu. Sasa sijui katika masuala mazima ya burudani hizi hasa hizi za muziki, sijui utaratibu mumeuandaa vipi katika kuangalia zile nyimbo zinazopigwa, sijui makubaliano yenu yanakuwa vipi na wasanii.

Lakini nikija kifungu cha 8 kinasema kuanzishwa kwa bodi ya wakurugenzi, kazi na majukumu yake. Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha (a) kinasema mwenyekiti atateuliwa na Rais na wengine mkurugenzi wa shirika ambaye atakuwa ni mjumbe, wakuu wa idara, mwanasheria kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu, mjumbe mmoja kutoka wizara inayohusika na mambo ya fedha, wajumbe wengine wasiozidi wawili kutoka kwa watu maarufu wa Zanzibar ambao watateuliwa

na Waziri wenye ujuzi, taaluma, uzoefu katika nyanja za utangazaji, teknolojia, utawala wa sheria, vyombo vya habari, taaluma, biashara, fedha na uandishi wa habari.

Sasa mimi hoja yangu inakuja kwenye hiki kifungu cha 8 (3), kinasema mtu hatoweza kuteuliwa kuwa mwenyekiti isipokuwa awe na maarifa na uzoefu katika nyanja ya utangazaji, teknolojia, habari, sheria, utawala, vyombo vya habari, usimamizi wa biashara, mawasiliano ya umma na nyanja nyengine kuhusiana na hayo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa ulimwengu tunaokwenda nao na hasa katika chombo hiki kwenye ulimwengu wa digital, hapa lazima tuweke sifa katika kumpata huyu mwenyekiti. Sifa bado hapa zinahitajika. Hizi sifa tulizozitaja bado ni sifa za juu juu tu, hapa hatujaweka kiwango cha taaluma, kwa sababu huyu mwenyekiti atakuwa anawasimamia watu wenye taaluma zao, kwa hivyo nadhani na yeye ni vizuri tukamuweka akaweka na taaluma ambayo hata wale wajumbe wake wa bodi wataweza kumuheshimu.

Sasa mimi nilikuwa napendekeza basi alau angelikuwa na digrii katika fani hizi zilizotajwa hapa. Lakini kuiweka tu hivi hivi, mim nafikiri bado hasa katika ulimwengu wa hivi sasa elimu imeshika nafasi kubwa sana na ukisema uzoefu tu kuna mambo ya mabadiliko makubwa yanakuja kwa teknolojia ya sasa hivi. Kwa hivyo ule uzoefu hauendani na teknolojia ya sasa.

Mwenyekiti atakuja kudanganywa hapa, atakuja kuambiwa mambo kumbe wala sio na hayapo duniani. Sasa mimi nadhani ni vizuri tukaweka sifa pale, basi alau awe na digrii katika fani hizi zilizotajwa.

Mhe. Mwenyekiti, hapa ilikuwa inazungumzia bodi itamteuwa mwenye taaluma katika fani ya sheria, hii kuwa Katibu wa Bodi. Mhe. Mwenyekiti, hii mimi sina pingamizi nayo lakini vile vile hapa katika kifungu cha 3 kinasema ikiwa Katibu hatokuwepo kutokana na ugonjwa au kutokana na sababu nyengine yoyote, hawezi kutekeleza majukumu yake bodi itateuwa mfanyakazi mwengine yeyote wa shirika kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya katibu kwa muda ambao katibu hatokuwepo mpaka nafasi itakapojazwa.

Sasa hapa mimi Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa kidogo nna mashaka, kwa sababu hapa katika kifungu cha 9 kinasema bodi itamteuwa mtu mwenye taaluma katika fani ya sheria mwenye kiwango angalau shahada ya kwanza na uzoefu wa kazi usiopungua miaka miwili katika fani hiyo ya katibu wa bodi.

Sasa mtu mwenye taaluma kama hii, leo inapokuwa amedharurika aidha kuumwa au kupata dharura yoyote kwamba bodi iweze kumteuwa mfanyakazi yeyote tu, mimi nadhani hapa kidogo tuangalie upya kwamba hapa katibu wa bodi ametajwa kwa sifa, kwamba alau awe na shahada ya kwanza katika uzoefu wa kazi usiopungua miaka miwili katika fani hiyo kuwa katibu wa bodi.

Sasa anapokuwa amedharurika hayupo na dharura zipo nyingi, ugonjwa, safari za muda mrefu na mambo mengine. Sasa leo ikiwa katibu hatokuwepo kwamba bodi itamteuwa mfanyakazi yeyote tu mwengine wa shirika kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya katibu wa bodi kwa muda huo, mimi nadhani lazima huyu katibu wa muda basi alau angekuwa sifa vile vile zingelitajwa.

Kwa sababu anaweza akaja akafanya kazi nzuri katibu wa bodi lakini kile kipindi ambacho atakachokuwa hayupo kwa dharura, huyu atakayemkabidhi au atakayekabidhiwa hana sifa zile kazi anaweza akaja akazivurunda.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu ya nne ya sheria hii "Uongozi na wafanyakazi wa shirika". Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 11 (2) (a) kinasema kwanza hiki mabano moja kinasema kuwa kutakuwa na mkurugenzi mkuu wa shirika ambaye atateuliwa na Rais, halina tatizo. Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa mkurugenzi ikiwa atakuwa amehitimu katika chuo kikuu kinachotambulika au kutoka katika chuo kinacholingana na hicho, hicho kipi? Maana yake hapa hakijatajwa hicho chuo chenyewe, amehitimu katika chuo kikuu kinachotambulika au kutoka katika chuo kinacholingana na hicho. Maana yake kama chuo kinacholingana na hicho sio kitakuwa ni hicho hicho chuo kikuu au kuna chuo kinacholingana na chuo kikuu ambacho sio chuo kikuu. Sasa hapa kidogo nije nisaidiwe maelezo.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki hiki cha 2 (d) kinasema sifa nyengine, huku samahani ilikuwa inaendelea katika mtu yule atakayekuwa na sifa za kuteuliwa kuwa mkurugenzi mkuu atakuwa imeekwa (a), (b), (c) na (d). Sasa hii (d) inasema sifa nyengine yoyote kama itakavyoamuliwa na Rais.

Sasa leo kama huku tumetaja sifa zote amehitimu katika chuo kikuu kinchotambulika au katika chuo kinacholingana na hicho, baada ya marekebisho nitafahamu halafu (b) mwenye uzoefu angalau katika moja au zaidi ya taaluma ya mawasiliano na habari, usimamizi wa biashara, habari, mawasiliano na utumishi wa umma. Kifungu cha (c) mwenye uzoefu wa maarifa ya kutosha katika sekta ya utangazaji, halafu hiki (d) kinasema sifa nyengine yoyote kama itakavyoamuliwa na Rais

Sasa kama tumeweka hizi sifa, halafu hizi sifa zote, halafu tukaja tukaweka sifa nyengine yoyote itakayoamuliwa na Rais, kwa hivyo ina maana kama sifa nyengine yoyote itakayoamuliwa na Rais, ina maana hata Mhe. Rais na yeye hatoona umuhimu wa kuangalia sifa zote hizi zilizotajwa katika kifungu cha (a), (b) na (c).

Anaweza akaja akamteuwa mtu …

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza malizia na wenzio wachangie.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Kwa hivyo, hapa kidogo nitataka ufafafnuzi kwa sababu unaposema sifa nyengine kama itakavyoamuliwa na Rais, kwa hivyo ina maana bila ya kuzingatia hizi sifa katika kifungu cha (a), (b) na (c).

Sasa mimi nadhani mapendekezo yangu hiki kifungu cha (d) kiondolewe kabisa, kwa sababu kinaharibu uzuri wote mulioweka huku mwanzo kwenye kifungu cha (a), (b) na (c).

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nakuja mkurugenzi mkuu atateuliwa kwa kipindi cha miaka mitano. Yaani hiki nakusudia ni kifungu cha 11 (4) ambacho kinasema mkurugenzi mkuu atateuliwa kwa kipindi cha miaka mitano na kutokana na utendaji wake bora anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine cha miaka mitano.

Sasa mimi nadhani kwa kuwa mkurugenzi anateuliwa na Rais na kazi hizi za habari zinataka pamoja na elimu lakini na uzoefu, kwa hivyo ina maana kama mkurugenzi ameteuliwa kipindi cha miaka mitano, halafu inasema anaweza kuteuliwa miaka mitano mengine, kwa hivyo ina maana hapa tumeshamfunga Mhe. Rais kama atahisi yule bado ana uwezo wa kuendesha hii idara, ina maana asiweze tena kumteuwa katika kipindi cha tatu, kwa sababu mkurugenzi yeye sio mjumbe wa bodi, yeye mjumbe wa bodi kwa ukurugenzi. Lakini ukurugenzi bado uwe kama ukurugenzi ili kama atakuwa mzoefu na ile kazi yake ataifanya vizuri, ina maana ukishaweka atateuliwa katika miaka mengine mitano, ina maana itakuwa ni vipindi viwili.

Kwa hivyo, ina maana hatoweza tena kuteuliwa tena katika kipindi chengine cha tatu lakini vile vile mkurugenzi unaposema atateuliwa kwa miaka mitano ukurugenzi, mimi nafikiri tusiuwekee kikomo kwa sababu mkurugenzi tukisema atateuliwa kwa miaka mitano, kwa hivyo ina maana mfano hata kama mtu kaboronga, lakini kipindi chake bado hakijesha.

Sasa mimi nadhani hebu tujaribu kuangalia. Mimi nafikiri kwa kuwa huu uteuzi wa ukurugenzi upo chini ya mamlaka ya Rais, mimi nafikiri tusiwekee kipindi, wale wajumbe wa bodi sina matatizo nao, wanaweza kuekewa kipindi lakini mkurugenzi asiwe na *limitation* katika suala hili.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kwa sababu naona unanitizama mpaka unanitizama kwa shingo upande, kwa kumalizia nawapongeza sana ZBC kwa kuweza kutuwekea lugha ya alama. Wenzetu walemavu siku zote na mimi katika kamati yangu ndio Mhe. Mwenyekiti, tupo pamoja walalamika sana kwamba wakati mwengine wanashindwa kupata taarifa mbali mbali za umma, tunawashukuru sana kwa kutuwekea yule mkalimani.

Lakini kwenye taarifa za habari aliekwa siku mbili tatu kwenye sherehe za mapinduzi mpaka leo hakuna. Kwa hivyo hawa wenzetu wenye ulemavu wa masikio wasikilize Baraza la Wawakilishi, taarifa za habari ambayo ni matokeo ya kila siku wasiweze kusikia. Sasa mimi nilikuwa naomba sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ili kuweza kutoa taarifa kwa umma wote wa Wazanzibari na Watanzania wengine, mimi nadhani mpaka kwenye taarifa zetu za hahari hawa wakalimani wawepo ili na wenzetu waweze kufaidika.

Lakini kwa kumalizia kabla sijaunga mkono hii hoja nataka nisema, kwa nini TVZ haionekani mpaka Mwanza, inakuwaje leo Star TV iko Mwanza tunaiona mpaka Zanzibar au ndio tulikuwa hatujaingia kwenye ulimwengu wa *digital*. Sasa mimi nafikiri Mhe. Mwenyekiti, aje atueleze Mhe. Waziri kama tukiingia kwenye ulimwengu wa *digital* tutaonekana mpaka Mwanza lakini vile vile tutaonekana katika mitandao kama zinavyoonekana televisheni nyengine.

Sasa hivi hizi *channels* za redio watu wapo Marekani, Uingereza wanafungua tu wana-*click dot dot* ngapi, *dot com* basi anaona. Sasa mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache baada ya kuambiwa kwamba shirika litarithi madeni ya wafanyakazi na litalipa nitaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja.

Nashukuru, ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Muumba wetu Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kuwa hai na wazima wa afya na jioni hii tukiwa tunaendelea na shughuli zetu katika Baraza hili la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia katika mjadala huu wa mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Utanganzaji Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Tatu Mhe. Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mhe. Waziri na Kaimu wake Waziri aliyewasilisha mswada huu kwa niaba yake kwa kuuleta mswada huu katika Baraza hili. Katika shukurani nisiwe mwizi wa fadhila niwashukuru vile vile na kuwapongeza Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Mifugo, Habari, Uwezeshaji na Kazi ambayo ndio iliyopitia mswada huu kwa marekebisho waliyoyafanya.

Mhe. Mwenyekiti, tunajadili mswada muhimu sana katika nchi yetu. Tunaujadili huu nasema ni muhimu kwa sababu kazi ambayo zinakusudiwa kufanywa na chombo kinachotakiwa mswada huu kinakwenda sambamba na haki ya msingi kabisa ya binadamu ambayo imo ndani ya Katiba yetu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ibara ya 18 (1) ya Katiba ya Zanzibar inasema, “Bila ya kuathiri sheria za nchi kila mtu yupo huru kuwa na maoni na yoyote na kutoa nje maoni yake na kutafuta, kupokea na kutoa habari kupitia chombo chochote bila ya kujali mipaka ya nchi na pia uhuru wa mawasiliano yake kutoingiliwa kati”

Lakini ibara 18 (2) kinasema “Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wowote kuhusu matukio mbali mbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii”. Hii ni ibara ya 18 ya Katiba ya Zanzibar 1984.
Mhe. Mwenyekiti, ukiisoma ibara hii hasa ibara hii ya 18 (2), inadhihirisha wazi wazi kwamba ili raia wa Zanzibar aweze kufaidi haki ya kupewa taarifa wakati wowote ni muhimu mno kuwa na vyombo vya habari ambavyo vinafanyakazi kwa ufanisi na ambavyo vinaweza kumtimizia haki yake hii raia wa Zanzibar. (Makofi).

Mhe. Mwenyekiti, nimeona nikinukuu kifungu hicho kwa sababu labda mara nyengine tunadhani kwamba masuala haya labda tunapofanyakazi katika taasisi fulani, labda unafanya kazi kwa taasisi nyengine tu, hizi taasisi zinapitana katika umuhimu wake, haidhuru zote zinawatumikia wananchi wa Zanzibar.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mbali ya kuzungumzia umuhimu wa mswada huu kwamba kwa kuugemeza kwenye Katiba ya Zanzibar, mswada huu una umuhimu wake kwa sababu unaendeleza historia ya Zanzibar kama moja wapo katika nchi kongwe kwenye bara hili la Afrika ambalo limekuwa na utamaduni wa kuanzisha na kuanzisha vyombo vya habari kwa muda mrefu sana kwenye historia yake.(Makofi).

Zanzibar yenyewe Mhe. Mwenyekiti, yenyewe katika kumbukumbu za maandishi inaweza kuivuta kwa ukaribu zaidi basi ni miaka elfu mbili na mia tano iliyopita katika kitabu kiliandikwa na wasafiri wa Giriki walipotembelea ukanda huu.

Kwa hivyo Zanzibar si nchi ya kuchezea chezea tu ina historia yake na mizizi yake katika dunia hii. Lakini Mhe. Mwenyekiti, historia hiyo kongwe haikuishia katika kuwepo kwa Zanzibar na watu wa Zanzibar, lakini pia katika ustaarabu wake. Moja katika ustaarabu unaopimwa wa mwanadamu ni uwezo wake katika kuwa na vyombo vya kutoa na kupokelea habari.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar katika huu ulimwengu wa kileo ilikuwa na sheria ya magazeti tangu mwaka 1938. Katika kitabu cha *index* namshukuru Waziri wa Katiba na Sheria tulimuomba na akatupatia, ukenda ukiangalia utavikuta pale. Kuna sheria za *newspaper decree* ya tarehe 17 Disemba, 1938.

Lakini la kufurahisha zaidi katika historia yetu ni kwamba hata hii sheria tunayotaka kuipitisha mswada huu, kwa maana ya *Zanzibar Broadcasting Corporation* basi ipo sheria iliyopitishwa tarehe 6 Disemba, 1961 ambayo inaitwa *Zanzibar Broadcasting Corporation Decree.*

Kwa hivyo Zanzibar ina historia yake na ukitizama haikuwa kwenye sheria tu lakini sheria zilitekelezwa mpaka mabadiliko makubwa ya kisiasa yaliyotokezea mwaka 1964 kutokana na mapinduzi, Zanzibar ilikuwa na magazeti yasiyopungua 17. Lakini katika historia hiyo hiyo ya utangazaji tunaambiwa kwamba redio Zanzibar iliyokuwa ikiitwa Sauti ya Unguja ilianza kusikika katika mwaka 1951.

Lakini fahari ya Zanzibar Mhe. Mwenyekiti, haishii hapo. Kama tunazungumzia dhana ya utangazaji kwenye ulimwengu wa Kiswahili, nakusudia matangazo kwa kupitia lugha ya Kiswahili basi huwezi kukwepa kuihusisha na Zanzibar, sio kuwa tu ilikuwa kwa sababu Sauti ya Zanzibar ilianzishwa mwaka 1951, lakini hata idhaa za nchi kubwa kubwa duniani zilikuwa zikitangaza kwa Kiswahili basi watangazaji wake maarufu walikuwa ni Wazanzibari, wametoka na kufunzwa hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika historia hiyo majina kama ya Bibi Saluma Shakshi, Bibi Zeyna Seif hawa marehemu lakini yupo bibi Aisha Yahya, yupo marehemu David Wakati, yupo marehemu Joseph Asama, haya ni majina maarufu kabisa ambayo huwezi kuyatenganisha katika ukuaji wa utangazaji kwenye lugha ya Kiswahili.

Lakini hata hii leo pamoja na kuwa tumerudi nyuma, ukenda ukisikiliza redio kwa mfano Idhaa ya Kiswahili ya Ujerumani kuna watangazaji wamestaafu karibu pale kama Othman Miraji, Ramadhan Ali, hata kama Bibi Umi Ulkheir ambaye watu wanasema ni mtu wa Commoro lakini amezaliwa Zanzibar kwenye mtaa wa Vikokotoni pale kwa Sheikh Omar Yussuf Mzee. Wapo kama Mohamed Abdulrahman, Charles Hilary, hivi sasa yupo Mohamed Abdulrhaman, hiyo ndio Zanzibar Mhe. Mwenyekiti, katika historia ya utangazaji.

Lakini hata katika miaka hii, baada ya mapinduzi Zanzibar imekuwa ni nchi ya mwanzo katika Afrika kuanzisha televisheni ya rangi. Aliasisi Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Zanzibar

Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, hakuwahi kushuhudia ikianza kazi imekuja kuzinduliwa na Mzee Aboud Jumbe mwaka 1974, lakini lile wazo lilitokana na yeye.
Na watanganzaji mahiri waliotoka katika TVZ wakati ule. Zilizopoanzishwa televisheni upande wa Tanganyika, watangazaji wake hata mafundi na wataalamu wengi walichukuliwa kutokana na watu waliopo kutoka TVZ. Mmoja kati ya watangazaji wa awali kabisa kwenye ITV tunakumbuka sote ilipoanzishwa alikuwa ni Bibi Fauzia Ismail. Alikuwa ni mtangazaji wa TVZ hapa.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nasema Zanzibar ina utajiri wa historia lakini tatizo letu lipo pale pale. Niliposema juzi nilipokuwa nikichangia mswada ule wa sheria ya marekebisho ya usafiri wa baharini kwamba tatizo letu ni utunzaji. Sasa utunzaji sio katika vyombo tu hata kulea watu na kuzalisha watu wapya ambao wana viwango kama hivi Zanzibar ilivyokuwa ikitajika.

Mhe. Mwenyekiti, katika lugha ya kiingereza kuna maneno mawili. Kuna kitu kinaitwa *progress* na kuna kitu kinaitwa *reprogress*. *Progress* ni kwenda na *reprogress* ni kurudi nyuma.

Sasa sisi tulikuwa na kipindi katika historia yetu tulikuwa tuna-*progress* na Zanzibar ikawa tumekwenda kwa kiingereza tumesema ilikuwa ina-*beat head line*, kila pahala Zanzibar ya mwanzo. Lakini bahati mbaya wakati dunia inasonga mbele katika miaka nafikiri ishirini nyuma hivi, sisi tumekuwa tuna-*reprogress* tunarudi nyuma.

Na eneo moja ambalo tumerudi nyuma sana Mhe. Mwenyekiti, ni eneo hili la utangazaji na sekta nzima ya habari. Mhe. Mwenyekiti, mimi nakumbuka, sizungumzii zama za akina Mhe. Ali Mzee, nazungumzia zama zetu sisi tu na Mhe. Hamza Hassan Juma alizozitaja.

Nakumbuka matangazo ya TVZ wakati mimi mdogo na yalivyo leo basi kwa viwango tofauti ni mbingu na ardhi. Si kwa ubora ni kwa kurudi nyuma. Moja katika chombo cha habari *serious* utakipima basi ni uwezo wake wa kuweza kupanga vipindi vinajulikana kama ikifika saa fulani siku fulani kuna kipindi fulani, na huko tulikotoka ndio tulivyokuwa.

Ilikuwa siku fulani ikifika hukosi unajua leo kuna Dr. Ayoub, ilikuwa siku ya Jumamosi unajua leo kuna mpira kutoka Ujerumani, wakati kwenye ukanda huu kulikuwa kuna kiza hakuna vitu kama hivyo Zanzibar watu wanaona au tukiona. Vipindi vya watoto vile unajua kwa kila siku ni muda gani mbali ya kila siku katika wiki unajua Jumatatu kuna nini, leo kuna mjomba tukijua hivyo. Leo yote yameondoka Mhe. Mwenyekiti, imekuwa TV ya kuvizia, hakuna cha kubandika inatafutwa mchezo wa kihindi onesha watu, ndio linavyofanya kazi Shirika la Utangazaji.

Mhe. Mwenyekiti, mambo ya kutia aibu na kuhuzunisha baada ya ku-*progress* tuna-*reprogress*. Mhe. Mwenyekiti, mfano tu wa ku-*reprogress* umetokezea leo wakati tunaingia hapa Baraza la Wawakilishi jioni hapa, sijui kama Mhe. Mwenyekiti, ulikuwa una habari wakati tunaanza Baraza la Wawakilishi TV zilikuwa kiza, kwa sababu wafanyakazi wameshindwa kufika hawana usafiri, hivyo wameshindwa tumeanza Baraza la Wawakilishi bado matangazo hayapo hewani.

Mhe. Ali Salum Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani alichangia hapa kuwa wananchi wake hawamsikii. Hiyo ni *reprogress* tunarudi nyuma Mhe. Mwenyekiti. Sasa mtu angeweza kusema kwamba ni kwa sababu labda uwezo ndio kila siku chaka letu tunalojifichia hilo.

Lakini mimi Mhe. Mwenyekiti, siamini, naamini ni kwa sababu ile ile kama ilivyozungumzwa kuwa kila tukizungumza Shirika la Meli hapa ilipofika, kwamba watu wamefanya Shirika la Utangazaji ni miliki yao binafsi yao ni hodhi yao, wanaendesha wanavyotaka wao, ni pahala pa kuvuna wao, kwa hivyo hawajali na matokeo yake wamewavunja moyo wafanyakazi wote. Kama yupo mtu ni kwa sababu ya uzalendo au hana budi hana pahala pa kwenda tu.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wametaja hapa mfano wa watangazaji ambao hata kipindi hichi wameondoka, lakini nilikuwa nakumbushwa hapa hivi sasa mmoja katika watangazaji wa *ZBC* anayesifika na si kwa sababu ameandaliwa, isipokuwa anajituma tu mwenyewe, maana yake ile kuandaliwa na kupewa mafunzo imepotea hakuna ni kijina anayeitwa Juma Mmanga anayetoa dondoo za magazeti.

Lakini maslahi yake ni aibu hata kusema na kwa zile sifa anazopewa tusije tukashangaa kesho kutwa akaondoka *ZBC* akachukuliwa sehemu nyengine, kwa sababu kama sisi hatuthamini uwezo wa watu na kuna watu wanaona vipaji vyao na watawachukua tu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti kwa bahati mbaya sana tunarudi nyuma. Mengine yametajwa hapa ni aibu kwamba wafanyakazi hawana huduma zozote za msingi, yaani hawana posho wanapokwenda kufanya kazi zao, hawana usafiri na hata vivazi vya kuwafanya waonekane vizuri katika matangazo yale.

Mhe. Mwenyekiti, hata *quality* mimi tulipopata mitambo tukaambiwa ya *digital* nilitegemea *quality* ya picha ile itabadilika na itakuwa nzuri kabisa. Sasa najiuliza sisi hasa tumerogwa na nini maana yake unafungua TV na wala siendi za mbali za hapa hapa.
Kwa mfano, *ITV, Star TV, Channel Ten, TBC* ya *quality*, yaani kiwango cha picha unayoiona pale ni nzuri na ukifungua *ZBC* picha kiza na sote ni mashahidi hapa na hasa wakati wa Taarifa ya Habari ndio kabisa, yaani ukiondoa yule mwenye kutangaza yule akikuunganisha na tukio basi hakuna kiwango.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika dunia ya leo sharti ukifungua *TV* na hizi zilizoanzishwa juzi tu miaka ya 1990 upande wa pili wa bahari, leo wanajua kwamba akitoa taarifa fulani basi kile kipande cha picha kinakwenda sambamba na lile analokutangazia, lakini si kwa *ZBC*, yaani habari inahusu kitu fulani na kilichobandikwa ni kile kilichoweza kupatikana na kubandikwa pale na wala hakihusiani kabisa na ile habari. Kwa kweli mifano mingi Mhe. Mwenyekiti na wala hatumalizi. *(Makofi)*

Kwa kifupi Mhe. Mwenyekiti, kama paliambiwa Shirika la Meli limeoza basi *ZBC* kunanuka uvundo harufu. Kwa kweli kama nilivyosema kwamba siwalaumu watumishi wanaofanya kazi zikawa hivi, isipokuwa nalaumu *management* ndiyo iliyowafikisha pale na ikaliua *ZBC* na kabla *ZBC* ni *TVZ* na Redio ya Sauti ya Tanzania Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, tunasema haya kwa uchungu tena yanasikitisha sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasema tumetoka kwenye ufahari wa kujinasibisha na kutoa majina makubwa makubwa Zanzibar ikitajika na leo tumefikishwa hapo leo. Mhe. Mwenyekiti, nasema kuna haja wakati tunajadili mswada huu kuzingatia vile vile haja ya kulitazama shirika hili hasa

management yake kwamba liko kwa maslahi ya nani, lipo kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar au lipo kwa maslahi ya mtu mmoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri maswali haya serikali itakuja kujibu, kwa bahati nzuri kuna mtu alizungumza hapa kwamba haya maswali haya hayamaliziki leo yatakuja kuhojiwa wakati wake ukifika kuhusiana na utendaji mzima wa serikali tunapimwa kila baada ya miaka mitano, basi yatakuja kupimwa haya. Kwa hivyo, nasema serikali iyatazame vizuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye mswada kwa maana ya vifungu na hiyo ilikuwa ni bashrafu tu, naam. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika mswada kuna jambo moja ambalo nataka kulizungumzia la jumla pia ni la mswada kabla kuingia kwenye vifungu. Ukizungumzia vyombo vya habari kama vilivyo chini ya *ZBC*, kwa maana ya vyombo vya habari vinavyomilikiwa na umma.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nitofautishe kuna tofauti ya kusema chombo cha habari cha serikali na chombo cha habari cha umma. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilibahatika kupata mafunzo ya sheria na mwaka wa mwisho kwenye yale maeneo ambayo unaambiwa uchague unalotaka basi mimi nilichagua kusoma juu ya mambo ya *media regulations*.

Kwa hivyo, tunatofautishiwa kusema chombo cha habari cha serikali na cha umma. Sasa unaposema chombo cha habari cha serikali maana yake ni kiilinde serikali iliyopo madarakani ndio maana yake, lakini ukisema chombo cha habari cha umma maana yake kinaendeshwa kwa fedha za walipa kodi kitumikie maslahi ya umma na ndio wanaunganisha wataalamu wa fani hii kitu kinachoitwa *Public Broadcasting* na *Public Interest.*

Mhe. Mwenyekiti, hii tunayoitungia sheria hapa ni *Public Broadcasting Services* ni kwa ajili ya umma na ndio maana inaendeshewa fedha za walipa kodi, kwa hivyo inatakiwa ilinde *Public Interest*. Sasa hili nimesema niliseme Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu nitaliunganisha baadaye katika mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema katika mswada naomba nianze kwenye eneo la kwanza kabisa kifungu cha 2 linalohusu ufafanuzi. Mhe. Mwenyekiti, nimelitaja hilo maslahi ya umma kwa sababu katika mswada huu kwenye kifungu cha 6 neno maslahi ya umma linajitokeza. Lakini neno zito kama hili ambalo lilipaswa liwe ndio msingi na maudhui ya mswada wenyewe katika ufafanuzi halina tafsiri, sasa neno maslahi ya umma akatafsiri anavyotaka yeye.

Kutokana na hali hiyo, tulipaswa katika sheria tuseme tunaposema maslahi ya umma katika mswada huu tunakusudia nini, ili wale wanaofanya kazi ya kuliendesha shirika hili, basi wajue wanapofanya kazi wanapoambiwa wanalinda maslahi ya umma wajue ni maslahi gani hayo ya umma yanayolindwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2002 nilibahatika kuteuliwa na Mhe. Rais wa wakati ule Rais Mstaafu Mhe. Dkt. Amani Abeid Karume kuwa mmoja miongoni mwa Makamishna watano waliotoka Chama cha *CUF* walioungana na wengine watano kutoka Chama cha Mapinduzi kuunda tume iliyokuwa ikiitwa Tume ya Rais ya Pamoja ya Usimamizi wa Muafaka.

Katika maeneno yaliyokuwemo mule moja lilikuwa ni marekebisho ya vyombo vya habari, kwa bahati mbaya kuna baadhi ya watendaji walikuwa wanakwaza baadhi ya mambo. Lakini Tume ya Rais ya Pamoja ya Usimamizi tuliandika waraka huu na leo nimekwenda kuutafuta mpaka nimeuona, yaani tuliandika waraka huu mwaka 2003 nakumbuka kuhusu Majukumu ya Vyombo vya Habari vya Serikali katika Utekelezaji wa Muafaka.

Wakati ule tulizungumza suala la maslahi ya umma na tukasema tafsiri yake nini kwa sababu ile ile ya kutomuachia mtu mmoja akatafsiri anavyotaka yeye. Kwa bahati nzuri kwa sababu tulikuwa tunazungumzia hili katika muktadha wa Muafaka ule wa mwaka 2001, tukasema ule Muafaka wenyewe ulikuwa umetafsiri nini maslahi ya umma. Mhe. Mwenyekiti, katika utangulizi wa Muafaka wa pili wa mwaka 2001 kwamba na naomba ninukuu Mhe. Mwenyekiti.

"Kwamba katika kufikia makubaliano yenye lengo la kuupatia ufumbuzi wa kudumu mgogoro wa kisiasa ulioikumba nchi yetu, vyama vyetu viwili vitaongozwa na maslahi ya taifa na humu ndio imezungumzwa maslahi ya taifa, ambayo inazingatia umoja wa kitaifa, amani na utulivu wa nchi, maendeleo ya wananchi katika uhuru wa demokrasia na utawala wa sheria na haki".

Mhe. Mwenyekiti, hayo ndiyo yaliyotafsiriwa kuwa ndio maslahi ya taifa na wala sidhani kama itapishana sana na maslahi ya umma. Ninachotaka kusema Mhe. Mwenyekiti nimenukuu hii kwa sababu na nafurahi kwamba Mhe. Mwanasheria Mkuu amefika, nilikuwa nadhani kwenye ufafanuzi kuna haja ya kutafsiri maslahi ya umma katika muktadha za mswada huu tunakusudia nini, iwaongoze watendaji hawa.

Mhe. Mwenyekiti, ukisomeshwa dhana ya *Public Broadcasting* na *Public Interest* unaambiwa, basi unaambiwa *Public Interest* kubwa kuliko yote ni kulinda demokrasia kwa maana ya kuwapa wananchi uhuru na sauti kupitia vyombo ambavyo wao wanavilipia kodi na ndivyo wanavyoviendesha kwa jasho lao. Kwa hivyo, nasema hilo naomba lijitokeze.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba niende kwenye sehemu ya pili kuanzishwa kwa shirika kazi na majukumu yake. Hapa Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anisadie ikiwa yeye au mwengine kwa niaba ya serikali, katika kifungu cha 3(3) naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 3(3) kinaeleza hivi:-

> "Kwa kuzingatia Sheria ya Mitaji ya Umma Shirika litakuwa ni chombo kinachojitegemea na cha kuduma na chenye muhuri wake wenyewe na kwa kutumia jina lake, kitakuwa na uwezo wa kushtaki na kushtakiwa, kumiliki mali inayohamishika na isiyohamishika, kuingia katika mikataba na taasisi mbali mbali, kukopa kiasi chochote cha fedha kinachohitajika kwa ajili ya Shirika".

Mhe. Mwenyekiti, nilipo mimi ni hapa kukopa kiasi chochote cha fedha, nilikuwa najaribu kutizama kwamba je kuna pahala popote ambapo pamewekwa ku-*qualify* kuweka masharti au angalau kutatakiwa kushauriana na mamlaka fulani kabla ya kuamua huo mkopo hasa kwa kusema kiasi chochote cha fedha.

Mhe. Mwenyekiti, nalisema hili, kwa sababu humu Barazani tumezungumza mara nyingi kwamba mashirika haya yamekuwa ni mzigo kwa serikali na i/naendelea kutoa ruzuku tu kwa sababu yanashindwa kujiendesha. Sasa mara nyengine suala la kukopa fedha na mzigo baadaye unakuwa na shirika lakini ni wa serikali kwa sababu shirika ni la serikali na mwenye mashirika tumeambiwa hapa ni Mhe. Waziri wa Fedha katika nchi yetu.

Kwa hivyo, hili naomba hatuoni haja ya kui-*qualify* hii kwamba kutahitajika kupata *approval*, yaani ridhaa ya mamlaka fulani hasa kwa kiwango cha fedha kilichofikia kiwango fulani. Hilo moja.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti liko kwenye kifungu cha 5 cha mswada huu kuhusu malengo ya shirika na hapa naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 5(b) kinaeleza hivi:-

> "Malengo ya Shirika yatakuwa ni:
>
> (b) Kutoa huduma za utangazaji za redio na televisheni na huduma nyengine zinazohusiana na hayo na vipindi ambavyo vitachangia maendeleo ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kitamaduni pamoja na kutilia mkazo umoja, na kamati ikaongeza na mshikamano wa kitaifa katika upanuzi wa utamaduni".

Mhe. Mwenyekiti, nimeona nikinukuu kifungu hichi kwa sababu hadi hivi tunavyozungumza kwa bahati mbaya utendaji wa shirika hili hauakisi matakwa haya. Siku moja alisema mama yangu namheshimu na kwa sababu ya kutotafuna maneno katika kusimamima ukweli Mhe. Asha Bakari Makame, alisema hapa na kumuonya waziri wa wizara hii kwamba usipoangalia watendaji wako watakuangusha. *(Makofi)*

Sasa na katika chombo hichi Mhe. Mwenyekiti, kuna watu dhana ya Umoja wa Kitaifa ambayo ni maamuzi ya wananchi wa Zanzibar kwa asilimia 66 waliopiga Kura ya Maoni tarehe 31 Julai mwaka 2010 bado hawajaikubali wao. Kwa hivyo, sasa wewe inawezekana hujaikubali na wala si tatizo katika demokrasia kila mtu ana uhuru wake. *(Makofi)*

Lakini hasira zao za kukataa maamuzi ya watu usizitumie katika chombo cha umma ulichowekwa kukiongoza. Kwa kweli hichi chombo cha umma kinapaswa kilee ile dhana ya Umoja wa Kitaifa ambayo imeamuliwa na wananchi wa Zanzibar kwa Kura ya Maoni tena kwa gharama kubwa wananchi wameamua.

Mhe. Mwenyekiti, mkuu wa chombo hichi anataka kuleta fitna katika nchi hii amethubutu kumtia adabu na kutaka kumuhamisha mfanyakazi kwa sababu tu ametoa habari inayomuhusu Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na huyu ni kiongozi wa nchi kwa mujibu wa Katiba iliyopitishwa na Baraza hili na baada ya maamuzi ya wananchi. *(Makofi)*

Kwa kweli mpaka mwenyewe akenda kujihoji Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais wakati alipokuwa akifanya ziara Wizara ya Habari akalihoji, sasa inafika aibu mambo haya yanatangazwa hadharani kwamba kuna mfanyakazi amehamishwa kwa sababu na zikaletwa fitna kwamba huyu amezidisha dakika kuliko mwenzake na alipoambiwa thibitisha, kumbe ni uongo mtupu unaundwa, ili watu kudhihirisha chuki zao walizonazo kwa sababu tu wananchi wa Zanzibar wameamua jambo ambalo yeye anaona hana maslahi nalo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nafurahi kwamba kifungu hichi kimo ndani ya sheria hivi sasa. Kwa hivyo, ninachosisitiza hapa ni utekelezaji wa vifungu hivi na kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan Juma mara nyingi naweza kuwa na sheria nzuri, lakini utekelezaji wake je, na hilo ndilo tunalosema kila wakati tutafika pahala tufanye sherehe za kuzitia moto kwa sababu hazitekelezwi. Kwa maana hiyo, nilikuwa nataka nikinukuu hichi, ili tuone utekelezaji wake.

Katika kifungu cha 6 kazi za shirika kifungu b hapa kidogo nimepata wasi wasi na naomba nitahadharishe Baraza naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 6(b) kinaeleza hivi:-

> "Kuandaa vipindi vya ndani vyenye ubora na kuchukua vipindi vya kigeni vinavyoendana na mahitaji ya wazawa".

Sasa nimeona Kamati katika marekebisho waliyofanya ni kama vile hawakukifahamu kwa hivyo wamerekebisha ambayo inapotosha kabisa ile dhamira iliyokuwemo kwenye mswada wa kiingereza ambao mara nyingi ndio unaokwenda kutumika kama ni sheria.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani ile tafsiri kwa jumla haikuwa mbali sana, lakini hapa lile neno vipindi vya kigeni limeondolewa kabisa, sasa ukiondoa kwa mujibu wa marekebisho ya kamati maana yake tunasema vyombo vya utangazaji vya Zanzibar visitangaze kabisa vipindi vya kigeni wakati sidhani kama ni malengo. Kwa hivyo, kilichokusudiwa ni kwamba vitangaze lakini viwe vinavyoendana na mahitaji ya wananchi wa Zanzibar.

Sasa hapa kilichoharibika ni kwamba kamati imefuta wazawa na kusema jamii, lakini ukisema jamii hata jamii ya Uingereza ni jamii. Kwa maana hiyo, nafikiri kungeweka hasa na wala hakuna ubaya wowote kusema hasa vinavyokwenda sambamba na maadili na utamaduni wa Mzanzibari, kwa sababu hivi vyombo vya umma vya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuombe Mhe. Waziri wakati atakapokuja turekebishe kwenye Kiingereza imekaa vizuri na inahitajika kubadilishwa tu pale iliposema *local needs*, basi iseme hasa *local needs of the people of Zanzibar*, napendekeza ikae hivyo.

Vile vile kwenye kifungu cha 6(d) naomba tuongeze neno dogo tu Mhe. Mwenyekiti na naomba kunukuu.

Kifungu cha 6(d) kinaeleza hivi:-

> "Kudumisha uhuru wa wahariri, kuwajibika na kuweka viwango vya kitaifa vya utangazaji kwa ajili ya utendaji bora".

Mhe. Mwenyekiti, hapa nilisema kwamba kulikuwa na haja ya kufanya *reference* kusema kwamba kulingana na Sera ya Taifa ya Habari, kwa sababu Zanzibar imepitisha sera ya habari na haya masuala ya uhuru wa wahariri na mambo yanayotajwa hapa ni roho ya sera ya habari. Kwa hivyo, nadhani kifungu hichi cha 6(d) kitamke hapa hilo suala la sera ya habari.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Mwenyekiti na hili nimuombe Mhe. Mwanasheria Mkuu hasa kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti kama ndivyo ilivyokusudiwa kifungu cha 7(e) naomba kunukuu.

Kifungu cha 7(e) kinaeleza hivi:-

> "Kuingia katika ubia au ushirikiano na serikali, taasisi binafsi au shirika lolote linalotekeleza majukumu yanayohusiana na utangazaji".

Sasa nilikuwa najiuliza serikali hapa ukisoma inafahamika kwamba ni serikali ya nchi za nje. Kwa hivyo, hivi shirika lenyewe tunaliruhusu kwa sababu hii ipo chini ya kifungu kinachozungumzia uwezo wa shirika, je tunataka kusema shirika lenyewe linaweza likaingia makubaliano na serikali bila ya kuishirikisha serikali na serikali, na nikisema serikali hapa nakusudia Mhe. Waziri kwa sababu waziri katika wizara ndio msimamizi wa sera kwa niaba ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja anitolee ufafanuzi, ili niridhike kwamba kifungu hichi hakitaweza kutumika vibaya na watu kutafuta maslahi yao kuliko kuangalia maslahi ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nipongeze sana marekebisho ya kifungu cha 8 ambayo yalianzishwa na kamati, lakini baadaye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kushirikiana na Mhe. Waziri husika wa mswada huu wamefanya marekebisho mazuri katika *schedule of amendment* ambayo wametupa, kwa sababu hata mwanzo kilikuwa kinanikwaza na wenzangu ambao wamechangia hapa wamekitaja na nikawaambia kwamba hivyo kimesharekebishwa kwenye *schedule of amendment*.

Kwa kweli nilikuwa ninapata tabu nilipokuwa nikisoma kwamba kwenye bodi waingie wakuu wa idara, ambapo ukija kusoma huku mbele inasema wakuu wa idara hao watachaguliwa na bodi na halafu wao wenyewe wanakuwa wajumbe wa bodi ikawa inaleta mashaka kidogo. Lakini baadaye nimefurahi kwamba kumefanywa marekebisho.

Kwa hivyo, kwenye haya marekebisho yaliyofanywa kwenye kifungu cha 8(f) mimi naomba moja tu, ambalo limekaa vizuri kabisa naomba katika wale, ambapo naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 8(f) kinaeleza hivi:-

"Waziri atateua wajumbe wasiozidi watatu miongoni mwa watu maarufa wa Zanzibar wenye ujuzi, taaluma na uzoefu katika nyanja za utangazaji, teknolojia, utawala, sheria ya vyombo vya habari, taaluma ya biashara, fedha na uandishi wa habari".

Mhe. Mwenyekiti, hapa naona ni vyema tungebakisha watatu, lakini wawili waachiwe uhuru huo na mmoja atajwe kwamba atatoka katika Jumuia za Waandishi wa Habari nafikiri alilizungumza Mhe. Marina Joel Thomas, tena nataka nimuunge mkono sana katika pendekezo lake hili alilolitoa, kwa sababu hapa tunazungumzia bodi ambayo inazungumza fani hii na hawa wanazo taasisi zao hapa zipo.

Kwa mfano, kuna WAHAMAZA, *Press Club* ya *Zanzibar*, *Press Club* ya Pemba, *JAZ* huko nyuma zilikuwako nyingi na zimepata ulemavu wa hapa na pale, lakini ziko jumuia. Kwa hivyo, nadhani kama ilivyotajwa kwa mjumbe mmoja atateuliwa na waziri kutokana na Jumuia ya Wafanyabiashara, Wakulima na Wenye Viwanda Zanzibar, basi si vibaya kwa huyu mmoja kutaja *specifically* kwamba atateuliwa kutoka kwenye jumuia hizo zao.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo kifungu cha 9 sina tatizo, isipokuwa nataka kusema tu kwamba kwenye kifungu cha 10(2) vile vile hichi nataka nisaidie kwamba hii ndio dhamira ya serikali katika mswada huu, naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 10(2) kinaeleza hivi:-

"Bodi inaweza kukasimu uwezo na mamlaka yake kwa mjumbe yeyote kufanya kazi kwa niaba yake, isipokuwa mamlaka iliyopewa chini ya kijifungu cha 1(c),(d) na (e) ya kifungu hiki".

Sasa maana yake yasiyokuwa (c), (d) na (e) bodi nzima inaweza kukasimu madaraka yake kwa mjumbe mmoja tu wa bodi kufanya maamuzi. Kwa kweli mimi nimeshtuka Mhe. Mwenyekiti, katika kazi za bodi kwamba tunatoa uhuru mpana kama huu hasa katika nchi zetu, ambapo tumeshaona watu wanaokabidhiwa madaraka wanavyotumia vibaya madaraka yao na hasa kwenye eneo kama hili linalohusu *Public Broadcasting*.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti nasema hebu hiki tukitazame tena kweli tunataka kutoa mamlaka haya makubwa kiasi hichi kwa mjumbe mmoja tu, kwamba bodi inaweza kumwakilisha mmoja tu akenda kufanya maamuzi kwa niaba ya bodi, mimi hapa kidogo inanipa mashaka.

Kifungu cha 11 Mhe. Mwenyekiti nataka niunge mkono mapendekezo ya kamati yaliyosema badala ya Mkurugenzi Mkuu anatajwa angalau awe shahada ya kwanza basi itajwe awe na shahada ya pili nakiunga mkono hichi. Lakini kuna suala moja la jumla nataka kulisema hapa siku moja tulivutana sana, naomba nisitumie neno kuvutana, isipokuwa tulikuwa tunapingana kwa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, naomba ujumuishe ili tupate mchangiaji wa mwisho.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ahsante namalizia nafikiri nimebakisha vifungu viwili kwenye mswada tu. Katika hili nasema siku moja tulikuwa tunabishana kwa hoja na Mhe. Mwanasheria Mkuu juu ya suala zima la Mhe. Rais kuwa na madaraka makubwa katika kuteua

na Mhe. Mwanasheria Mkuu akasema kama hatujabadilisha Katiba ibara ya 53 basi bado mwenye mamlaka ya kuanzisha ofisi na kuchagua wakuu wake atabakia kuwa ni yeye.

Sasa hili sitaki kulizungumza kwenye mswada huu, isipokuwa nataka kutumia mswada huu kupendekeza kwa serikali. Kwa hivyo, nafikiri wakati umefika kuangalia tena *policy* hii na kuweza kuifanyia marekebisho, ili tuangalie kwamba je katika vyombo kama hivi bado kuna haja ya wakuu wote wa taasisi zote hizi wakachaguliwa na Rais au kama wanaendelea kuteuliwa na yeye si vibaya.

Lakini kupata idhini ya vyombo kama hivi kwa sababu katika nchi za wenzetu zinafanya hivi kwamba Rais anateua kwa mapendekezo yatakayopendekezwa na Waziri husika. Kwa mfano, Baraza la Kutunga Sheria la nchi ile linaidhinisha uteuzi na sio wa kila kitu kwa zile baadhi ya taasisi ambazo zinaonekana zina umuhimu. Kwa hivyo, nilikuwa nasema hili labda tulitazame kwa mapana yake.

Vile vile kifungu hicho cha 11(3) ambacho kinazungumzia uwajibikaji, naomba kunukuu.

Kifungu cha 11(3) kinaeleza hivi:-

> "Mkurugenzi Mkuu atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa Shirika na atawajibika katika utekelezaji wa kazi za kila siku za Shirika".

Mhe. Mwenyekiti, hakuna kwenye kifungu hichi wala popote inaposema kwamba atawajibika kwa nani. Sasa ndipo pale nikajiuliza anawajibika bila ya shaka moja haina shaka atawajibika kwa Rais kwa sababu ndiye aliyemteua, lakini je anawajibika kwa bodi au waziri na hii pia nadhani iwekwe wazi kwa sababu limetajwa hapa.

Mhe. Mwenyekiti, umenihimiza kwa muda na mimi sitaki nitofautiane na wewe, ili wengine wapate muda.

Vile vile nataka niunge mkono yale marekebisho mengine ambayo yameletwa na serikali hapa hasa kwenye kile kifungu cha 18 ambacho kilikuwa kirefu na Waheshimiwa Wajumbe wengi wamekichangia wakenda kwenye kitu kimoja kimoja, kumbe vile wangeangalia marekebisho haya tayari kimeshafupishwa na kufanywa kuwa kidogo tu, ambacho kimejielekeza kwamba Sera ya Uhariri itazingatia Kanuni ya Maadili iliyoelezwa kwenye Sera ya Habari na Sheria ya Tume ya Utangazaji. Mhe. Mwenyekiti, nataka niunge mkono kwa sababu hiyo itatupa nafasi nzuri ya kuyatumia yale ambayo yamo katika Sera ya Habari.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kama nilivyosema mwanzo kwamba naiunga mkono sheria hii na bila ya shaka tutaipitisha. Lakini nilikuwa nadhani kama nilivyosema mwanzo kwamba waliochangia jana walizungumza juu ya Shirika la Meli. Kwa hivyo na mimi niiambie serikali kwamba kwa shirika hili kuleta sheria ni hatua ya kwanza.

Lakini linahitaji marekebisho makubwa katika *management* yake, uongozi uliopo kwa kifupi Mhe. Mwenyekiti umeoza, unanuka na wala haufai, kwa sababu haiwezekani watu ambao walikuwa sababu ya uozo niliouzungumza mapema na kila mmoja ameuchangia hapa, wakawa

wao ni sehemu ya utatuzi wa yale, kwani mtu mwenye kuunda tatizo hawezi kulitatua tatizo, yaani aliyekuwa *part of the problem can't be part of the solution*.

Kutokana na hali hiyo, tunahitaji kutafuta *management* mpya ambayo ni makini itakayoweza kufanya kazi nzuri ya kulisarifu vizuri shirika hili pamoja na kulisimamia, ili liweze kufanya kazi zake vizuri kwa maslahi ya wananchi na hilo linawezekana Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tumeona.

Kwa mfano, kwa wenzetu upande wa Bara alipoteuliwa Tido Mhando tumeona mabadiliko makubwa ambayo ameyaanzisha *TBC* mpaka leo anakumbukwa. Kwa hivyo, *management* ni kitu muhimu sana, lakini Mhe. Mwenyekiti tukiendelea kurudufisha hayo kwa hayo tu, basi tutaendelea kupata hayo kwa hayo.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono mswada huu, lakini nitahitaji majibu kwa yale mambo ambayo nimeyatolea hoja. Nakushuku sana kwa kunipa fursa hii.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Allah kwa kunijaalia jioni hii katika hali ya uzima wa afya nzuri. Pili nikushukuru na wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mawazo yangu katika Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Utangazaji Zanzibar.
Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba hili ni wazo zuri kuwa na Shirika la Utangazaji katika Zanzibar yetu na mashirika mengine kwenye wizara mbali mbali. Lakini Mhe. Mwenyekiti, wazo si kuwa na shirika, kwa sababu tunaweza kuwa na mashirika mengi, lakini ufanisi wa mashirika hayo ukakosekana, japo kuwa tumejitungia sheria tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa suala hili tunashukuru sana kwamba Zanzibar tunasifika kwa sheria, tatizo letu kubwa ambalo linatuathiri ni kutozifuata hizo sheria ambazo tumejiandikia wenyewe.

Kwa kweli hili ni tatizo Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, kwa hili naiomba sana serikali vile vyombo ambavyo vimewapa mamlaka ya uendeshaji, basi serikali ijaribu kukunja kucha zake, ili watendaji wetu waweze kuonesha zile fani pamoja na elimu zao walizonazo kwenye mashirika yao.

Lakini leo unaanzisha shirika na kutunga sheria na wala hukubali mpaka uingize mikono ndani yake. Kutokana na hali kama hivyo, itakuwa watendaji wetu hatujawapa nafasi yao ya kutenda haki kwenye mambo yao haya. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ili mashirika yetu haya yawe na nguvu na yaweze kujituma basi serikali wajaribu kuwapa uwezo wa nyenzo na wao waweze kufanya kazi ili kuwatumikia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nizungumze katika malengo ya shirika kifungu cha 5(a) kutoa taarifa elimu na burudani kwa jamii. Suala hili la utoaji wa taarifa kwa kweli ni vyema shirika letu libadilike na liendelee kubadilika. Hivi sote ni mashahidi ndani ya mwaka uliopita Zanzibar tulipata ajali ya meli mbili lakini tuzungumzie ile ajali ya mwanzo ya MV. Spice Islander taarifa ya meli ile mnamo saa 6 za usiku zilianza kutolewa katika vyombo vya habari mbali mbali. Lakini katika vyombo ambavyo serikali imemiliki basi taarifa hizi zilishindikana kutolewa mpaka asubuhi.

Mhe. Mwenyekiti, baadhi ya wananchi wengi taarifa kutoka vyombo vyengine vya habari kuamini kwao kunakuwa ni kudogo, kama hawajasikia taarifa kutoka ZBC au Redio Zanzibar kama hazijatoka hapo basi kuamini kwao ni kudogo. Hasa zikija taarifa za muandamo wa mwezi pia wananchi wetu wanakuwa wagumu kusikiliza redio nyengine kama hawajasikia redio yao ya Sauti ya Zanzibar na TV Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, suala kama hili kutokana na hapo nyuma vyombo vyetu vilikuwa vinafungwa ilikuwa ni kikwazo kikubwa na inakuwa ni tatizo hata zile taarifa zipatikane basi hawana uwezo ule wa kurudi tena studio wakafungua idhaa ili kuzitoa taarifa zile.

Mhe. Mwenyekiti, katika kumbukumbu zangu nakumbuka miaka ya 80 - 90 kuna kipindi kimoja tu ndio Sauti ya Tanzania Zanzibar kwa wakati ule ilipotoa taarifa za muandamo wa mwezi saa 9 za usiku. Suala hilo lilikuwa ni geni kabisa. Matokeo mara nyingi yanapokuwa yanatokea basi ni vyema kwa sauti zetu hizi au televisheni kutoa matokeo kabla ya vyombo vyengine vya habari havijatoa.

Lakini pia tatizo moja katika habari mara nyingi kuzithibitisha habari katika vyombo vyetu kunakuwa kuna mlolongo mrefu, mpaka habari zile kwenye vyombo vyengine wanakuwa wameshazisema mara nyingi lakini televisheni na redio wanashindwa kuthibitisha. Kwa hivyo kama hawajapata thibitisho ya matokeo kama yale basi waseme tu kuwa habari tulizozipokea ambazo hazijawa na uhakika. Lakini watakuwa tayari wameshaanza kuzisema taarifa zile, kwamba tayari kumetokea hili na hili lakini ule uhakika bado haujapatikana. Lakini taarifa itakuwa tayari ipo hewani na wananchi wameshaanza kukaa *attention*. Kwa hivyo ningeliwashauri sana kuko kuchukua muda mrefu taarifa haijatolewa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna masuala mazima ya burdani kwa jamii, tulikotoka ni kuzuri kalini kila hatua tunapokwenda mbele mambo haya ya burudani yanazidi kuongezeka sukari. Lakini na sukari inapokuwa nyingi saa nyengine inakuwa chungu. Itakuwa kile kitu hakinyweki. Burudani tulizonazo za leo mambo ya mipasho na mambo mengine inamfanya msikilizaji wa kipindi kile afahamu kuanzia a – z, kwa hivyo inakuwa sasa hapaimbwi panasemwa mambo ya akina rusha roho haya ni mambo yanaudhi saa nyengine. Kwa hivyo ni vyema sheria hizi ziweze kuwabana wote wale wanaokwenda kinyume na maadili ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika Sehemu ya Sita kuna Masharti Mengineyo. Katika masharti mengineyo nataka nizungumze kidogo katika (b) na (c) hapa inasema kuhakikisha taarifa na burudani zinachangia kulinda maadili ya jamii kwa kuzuia matumizi yoyote ya habari na vipindi vinavyotumia lugha chafu, picha za ngono na mambo mengine yanayokera ambayo hayana nia ya kuelimisha.

Mhe. Mwenyekiti, hichi kifungu ni kizuri mno unapokisoma lakini nahofia uzuri huu wa kifungu ukabakia katika sheria. Kifungu hichi kama kweli bodi itasimamia vizuri basi tunaweza tukapiga hatua na tukaondosha yale yote yanayokera na ni machafu na lugha mbaya. Katika ushindani ya hivi vyombo vya habari kwa kweli ili habari ziwe nzuri basi kwanza ni kuwa na uhakika nazo kwamba hili ninalolisema ni kwa ukweli.

Mhe. Muhammed Haji Khalid hapa asubuhi amesoma habari ambazo yeye kaitwa ni mwakilishi wa jimbo la Matemwe CCM, habari zimeandikwa na muhariri na ni mtu ambaye ana fani. Kwa hivyo hapa tayari habari kwa Mhe. Muhammed Haji Khalid ni Mwakilishi wa Matemwe anabadilisha mawazo na Mhe. Mwakilishi wa CUF wa Wawi, tayari hizi habari zimeshaanza kutumiwa vibaya. Hili ni kosa kama ni kosa na waliokosea ni wahariri wetu, wajaribu kuwa na uhakika na kile wanachokiandika ili msomaji anapopata habari ile aweze kuridhika kesho au keshokutwa aweze kununua gazeti la mwandishi yule. Lakini ikiwa habari zake ni za kutatanisha hazileti uwelewano mzuri, kwa kweli tutakuwa hatujafikia malengo na mara nyengine hatua za kinidhamu zinaweza kuchukuliwa kwa mhariri yule.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha (c) kinasema kwamba kukusanya, kutafuta, kuchambua na kutangaza habari na kutoa maoni ya ukweli, uaminifu na kwa haki, bila ya kuhatarisha amani na utulivu wa nchi.

Mhe. Mwenyekiti, wengi ni mashahidi vyombo hivi vya habari baadhi ya nchi nyingi vimesababisha vita vya wenyewe kwa wenyewe kwa kutumia habari na kama hatutojipanga vizuri kwa siasa tulizonazo, kwa dini tulizonazo, kwa mambo mengine tuliyonayo na kama waandishi wetu hawatokuwa makini basi mambo kama hayo pia yanaweza yakajitokeza katika nchi yetu ya Zanzibar.

Hapa tumeona mfano wenzetu wa Burundi redio yao INTARAHAMWE iliingizwa siasa, chafu, mbaya ni makabila mawili tu ikabidi kugombana. Kugombana kule ikawa ni vita vikubwa ambavyo vilipoteza roho za Wanaburundi wengi mno kwa kuvitumia vibaya vyombo vya habari. Ili tusifike huko mimi hichi kifungu nimekijali kweli kweli na kuwe na uaminifu na haki. Haki ni nini?

Tuna taasisi mbali mbali, tuna taasisi za kidini wanapokuwa na mihadhara yao basi chombo hichi na wale ni walipaji wa kodi wanakiendesha hichi chombo kwa hivyo waende kutoa habari zile. Lakini isiwe habari za wanasiasa tu lakini taasisi za dini na taasisi nyengine hazina haki na chombo hichi. Kwa hivyo itakuwa bado hii haki iliyoandikwa hapa haijatendwa. Kwa hivyo ili haki ipatikane kila mlipa kodi wa chombo hichi basi wanapokihitaji chombo hichi waweze kutenda haki ili kila mmoja afaidike na matunda haya.

Mhe. Mwenyekiti, ule uchukuaji wa picha imeonekana kwamba kuna baadhi ya viongozi hutolewa sehemu ya kichwa tu na maneno machache mno. Lakini wengine hutolewa habari zao ukamilifu na mwili mzima, hii haijawa haki kabisa. Mimi narudia kusema kwamba tusiandike tu sheria lakini tukawa wagumu wa kutenda. Tujaribuni sana kuyatenda yale ambayo tumeyaandika.
Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, hebu tubadilikeni na tutakapobadilika kweli kidhati kabisa mbona Zanzibar ni nchi moja wapo ambayo itaweza kupiga hatua ya mambo ya maendeleo zaidi kulikoni nchi nyengine na kupata ustawi wa hali ya juu. Lakini baada ya kwishakupewa majukumu ikawa kuna vikao vyengine pembeni ili maisha daima milele tutakuwa tunasema tu, tutatoka hapa tutakwenda nchi za watu, mtakuja hapa mkitusifia tu, China kuko hivi, Japani kuko hivi, lakini Zanzibar je, tuko wapi? Na watu wanahamu waje Zanzibar wachukue ya Zanzibar wapeleke kwao. Isiwe sisi tu tunahamu ya kutoka hapa Zanzibar kwenda kujifundisha kwa wenzetu tukija hapa tukisifiana, sifa haitusaidii kitu. Utendaji ndio unapofika pahali ambapo

yakajenga matumaini ya nchi. Kinyume na utendaji itabakia historia tu kusoma hatima yake tutatia mafaili haya iwe hakuna lolote lile ambalo linapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hichi kimehimiza sana amani na utulivu wa nchi. Amani na utulivu unapatikana pale tunapojali haki kwamba mimi nina *issue* yangu vyombo vya habari hivi navialika vinakuja na vinatoa taarifa yetu vizuri na mwengine taarifa yake chombo cha habari kinakuja kinatoa taarifa zake vizuri, kama kila mmoja anapata haki hiyo basi mimi naamini amani na utulivu wa nchi unapatikana.

Lakini ikawa kaka ndiyo anayejaliwa ndugu hajaliwi, mjomba hajaliwi, shangazi hajaliwi basi amani na uvulivu itakuwa ni ndoto. Hili ni muhimu sana kusimamia maadili na haki katika Zanzibar kwa kupitia chombo chetu hichi cha habari.

Mhe. Mwenyekiti, umenipa dakika nyingi lakini kutokana na hali yangu kidogo sio nzuri ya mafua mafua. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono Mswada huu mia fil mia. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa wajumbe nakushukuruni sana kwa utulivu na mashirikiano yenu naakhirisha Kikao hadi kesho tarehe 23/01/2013 nakushukuruni.

(Saa 1:40 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 23/01/2013 saa 3:00 asubuhi)